KCSE 2026 TOP SCHOOLS MOCKS

KISWAHILI

(JARIBIO 1-10)

Imarisha maandalizi yako ya KCSE ya 2026 kwa mkusanyiko huu wa mitihani ya kina ya majaribio ya kina uliokusanywa kutoka shule bora za kitaifa nchini Kenya. Karatasi hizi zimepangwa kwa kina na kwa kina, zimeundwa ili kuakisi mazingira halisi ya mitihani ya kitaifa, kuhakikisha wanafunzi wanajenga ujasiri na usahihi unaohitajika kwa matokeo ya daraja la juu. Hii hutoa ramani ya wazi ya umilisi wa kitaaluma na kuwapa watahiniwa zana zilizopangwa na za kina za kusahihisha zinazopatikana.

CONFIDENTIAL!

Ukihitaji majibu, Pigia

Bw. Isaboke 0746 222 000 / 0753 222 000

NJIA YA MAFANIKIO

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA KWANZA)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1

INSHA

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Andika insha **mbili**. Insha ya **kwanza** ni ya **lazima.***
b) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*
c) *Kila insha isipungue maneno **400.***
d) *Kila insha ina alama **20.***
e) *Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
f) *Karatasi hii ina kurasa mbili zilizopigwa chapa.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. LAZIMA

Wewe ni mwanahabari katika Gazeti la Tujuze. Andika mahojiano kati yako na waziri wa Kilimo nchini kuhusu athari za baa la njaa na hatua zinazochukuliwa na serikali katika kukabili tatizo hili.

(alama 20)

2. Andika insha mojawapo kati ya insha hizi tatu. **(alama 20)**

a. Michezo na shughuli nyinginezo nje ya darasa zinawapotezea wanafunzi wakati wa masomo na zinafaa kupigwa marufuku. Jadili.

Au

b. Andika insha inayothibitisha ukweli wa methali:
Usipoziba ufa, utajenga ukuta.

Au

c. Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:
Nilitoa simu yangu mfukoni na kuipokea bila kuangalia ni nani alikuwa akinipigia. Nilipoipokea ilinidondoka …

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.

KILA LA HERI!

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA KWANZA)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2 (LUGHA)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Jibu maswali **yote** .*

b) *Majibu yote yaandikwe katika **nafasi** ulizoachiwa katika kitabu hiki cha maswali.*

c) *Majibu yote ni **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

d) *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii **zimepigwa chapa** sawasawa na kuwa **maswali yote yamo.***

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

1. UFAHAMU **ALAMA 15**

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

Katini alinitazama kwa muda alinijibu, 'Ndio alioa. Lakini unajua wanawake wa siku hizi walivyo; hawana moyo wa kumlea mwana wa mwenzao. Wanachelea kwamba ule ugwe uliowaunganisha baba na mama mtoto utamea tena. Wanasema kwamba kumlea mtoto wa mwanamke mwingine ni kuhatarisha masilahi yao katika ndoa.'

"Usimulizi wa Katini ulinikatisha tamaa zaidi. Nilijua kwamba hata nikamtafuta mama, huenda naye ameolewa na katika jamii yetu nasikia mtoto ni wa baba. Kwa hivyo, hata huko alikoolewa mama sitakuwa na hadhi yoyote, nikaona nitachukuliwa kama mpitanjia aliyekuja kuvuruga utulivu wa familia yao. Moyo uliniambia niende kwa shangazi yangu, lakini nilijikanya. Nilijiuliza, 'Ikiwa baba na mama hawawezi kunilea, sembuse shangazi? Haihalisi kumwongezea Shangazi Waridi mzigo. Hapo alipo hata ndiye anayegharamia masomo yangu kwa kidogo anachokipata kutoka kwenye vikataa vyake.

Nilipiga moyo konde, nikazidi kujiambia, ' Binadamu aliumbwa kupambana na ulimwengu na kutumia rasilimali aliyopewa na Mungu kuyaboresha maisha yake, najua nimepewa akili razini, nina azma ya kujiendeleza masomoni. Najua nitahitimu masomo yangu siku moja na kurudi hapa hapa petu kupajenga upya. Sitarajii kutatokea mtu kunyakua ardhi hii ambapo nimemzika mpenzi nyanya yangu.

Ari hii ilinifanya nijitome kwenye njia nisiyojua kikomo chake. Akili na miguu yangu ilinielekeza katika kijiji kimoja wanakoishi wafanyakazi wa shamba la chai la Shirika la Chai la Tengenea. Kiwanda hiki kinamilikiwa na Mzungu mmoja aliyekuwa mlowezi nchini. Mzungu huyu kwa jina Richard aliaga mara tu baada ya Uingereza kuikabdhi nchi hii uhuru. Hata hivyo, familia yake bado inamiliki shamba hili, kama Wazungu wengine wanavyomiliki mashamba ya michai na mibuni, pamoja na mashirika mengi ya utengenezaji wa mazao ya mimea hii nchini. Kining'inya ya Richard ndiye Afisa Mkuu Mtendaji wa shirika hili hivi sasa.

Ukiniuliza ni kwa nini niliamua kuja hapa nitakwambia kwamba nilijua pana shule hapo hapo shambani. Pili, nilijua kwamba iwapo ingetokea kwamba singekuwa na wa kuyakidhi mahitaji yangu ya kimsingi, nyanya yangu alikuwa amenifunza umuhimu wa kufanya kazi. Hapo shambani ningeweza kuchuna majanichai Jumamosi na hata wakati wa likizo ili kujikimu.

Asubuhi moja ilinipata ndani ya ofisi ya mwalimu mkuu wa shule ya Msingi ya Kilimo. Mwalimu Mkuu Bi. Tamasha, alisikiliza **kadhia** yangu kwa makini . Hakuonyesha kushtuka kwa yaliyonipata katika umri wangu mdogo hivi. Aliniambia kwamba ningeweza kuanza masomo katika darasa la pili. Aliniahidi kuwa angemwomba mzazi mmoja anipe hifhadhi. Huo ukawa mwanzo wa maisha yangu mapya katika makao ya wafanyakazi wa mashamba ya chai. Nilichukuliwa na familia ya Bwana Tenge na mkewe Kimai na kunilea pamoja na watoto wao watano. Wenzangu, nyinyi hamjui adha zinazowapata wafanyakazi wa kima kidogo. Mtajuaje na hamjawahi kukilalia kitanda hiki mkawajua kunguni wake? Chumba cha wafadhili wangu kilikuwa hichohicho kimoja; ndicho cha malazi, mapokezi na ndicho jikoni. Sebule na chumba cha malazi viligawanywa na shuka moja nyepesi. Usiku sisi watoto tulilala juu ya vigodoro ambavyo ni kama viliwekwa mvungni mwa kitanda cha wazazi.

Nilianza kuchuna majanichai kwa malipo kidogo nikiwa katika darasa la tano. Wakati mwingine ningerauka alfajiri na mapema kabla ya kwenda shuleni saa kumi na mbili asubuhi. Jioni nilipita huko huko. Nyakati nyingi nililala humo humo katikati ya michai, wakati mwigine kwa marafiki wangu, kwa Bwana Tenge, na juu ya uchaga mkubwa wa saruji uliotumiwa kama karo na wauza chakula sokoni. Hakuna hata mmoja kati ya walimu wangu aliyejua mabadiliko haya hadi pale nilipounfanya mtihani wangu wa darasa la nane na kufuzu vyema.

Maswali

a) Eleza kwa kutoa hoja tano, adha zinazomkumba msimulizi katika taarifa hii. **(alama 5)**

b) " Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi, " Thibitisha kauli hii ukirejelea kifungu hiki. **(alama 2)**

c) Taja methali moja inayodokezwa katika taarifa hii. **(alama 1)**

d) Kwa kutoa hoja tatu, eleza kinaya katika kauli "…baada ya Uingereza kuikabdhi nchi hii uhuru." **(alama 3)**

e) Thibitisha kuwa msimulizi ni mkakamavu. **(alama 2)**

f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika kifungu. **(alama 2)**

i) Nilipiga moyo konde

ii) kadhia

UFUPISHO. ALAMA 15

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:

Kenya inakumbwa na hali ya hatari kuwahi kutokea msimu wa mvua ambayo imefanya serikali kuchukua hatua madhubuti za kuzuia maafa zaidi. Baada ya tathmini ya kina kuhusu hali ya hewa inayotarajiwa, serikali imelazimika kutangaza hatua za kuepusha vifo na uharibifu huku mvua ikitabiriwa kuendelea kunyesha na kimbunga kutarajiwa kutua Kenya kwa mara ya kwanza katika historia. Kimbunga hicho kitasababisha mvua kubwa, upepo mkali na mawimbi yenye nguvu na hatari, ambayo yanaweza kutatiza shughuli katika Bahari ya Hindi na makazi yaliyo karibu na pwani ya Kenya. Hali hii imechangiwa pakubwa na mabadiliko ya tabianchi.

Matukio ya hivi majuzi yamepima ustahimilivu wa nchi yetu wakati wa changamoto ambazo hazijawahi kutokea. Mvua imeendelea kusababisha mafuriko ambayo yameharibu miundomsingi. Vilevile, shughuli za uchukuzi zimetatizika katika sehemu zote za nchi baada ya barabara kuharibiwa na madaraja kusombwa na mafuriko.

Viwango vya maji katika mabwawa makuu ya 'Seven Forks' vimefikia kimo cha kihistoria huku mabwawa hayo yakitishia wanaoishi karibu na maeneo hayo. Kuna mabwawa 178 na vidimbwi vya maji katika ardhi ya umma na ya kibinafsi katika kaunti 33 ambayo yamejaa na kuwa hatari kwa wakazi walio maeneo yaliyo karibu. Vifo vya watu, kufurushwa kwa watu kutoka makwao na uharibifu wa mali umeshuhudiwa nchini.

Hatari nyingine imetokana na maporomoko ya ardhi na matope katika baadhi ya kaunti na wakazi wanaoishi katika maeneo hayo watahamishwa huku wanaoishi katika maeneo yasiyoratibiwa kama ya makazi kwa mfano kando ya mito, wakipewa ilani kuhama kwa kutambua hatari iliyopo.

Kwa sababu ya janga la mafuriko, wizara ya Elimu imeagiza kuahirishwa kwa tarehe ya kufunguliwa kwa shule zote nchini kwa muhula wa pili kwa muda usiojulikana. Pia, madhara ya mvua katika baadhi ya shule ni mabaya zaidi kiasi kwamba maisha ya wanafunzi yamo hatarini. Hatua ya kuahirisha ufunguzi wa shule hadi tarehe isiyojulikana imeibua mgawanyiko wa kitabaka huku watoto kutoka familia maskini, wengi wao wanaosomea shule za umma, wakiendelea bila masomo wenzao kutoka familia tajiri wakisoma kidijitali. Isitoshe, bila tarehe mahususi za ufunguzi wa shule, ni vigumu kupanga masomo ya ziada wakiwa nyumbani. Hofu nyingine ni kuwa kukaa kwa

muda mrefu bila kufanya chochote kunaweza kuwapelekea wanafunzi katika matumizi ya mihadarati na mimba za mapema.

Serikali imetangaza kuwa tarehe mpya za muhula wa pili kwa shule za msingi na za sekondari zitarekebishwa ili kufidia muda ambao ungepotezwa kwa kucheleweshwa kufunguliwa kwa shule. Tena, kutokana na mafunzo yaliyopatikana kufuatia janga la korona, wazazi wengi wanahimizwa kununua vifaa vya kidijitali vya kisasa ili kutumika katika masomo ya kidijitali.

Jeshi la Ulinzi la Kenya na Huduma ya Polisi zimeagizwa kutumia rasilmali, maafisa na vifaa vyao kuhakikisha wakenya wako salama. Wangeshirikiana na shirika la Huduma ya Vijana kwa Taifa na maafisa wa Utawala kushughulikia dharura ikiwemo kuokoa wote walio kwenye hatari.

Baraza la mawaziri limeagiza Wizara ya Fedha kutoa pesa za kusaidia kukabiliana na janga hili. Hata hivyo, kumekuwa na ukosefu wa uwazi katika utoaji wa fedha na hata misaada ambayo inakusudiwa kuendea walioathirika na vilevile haifikii wenye ulemavu-udanyanyifu katika mchakato mzima kuanzia kuwasilisha majina ya waathiriwa hadi ngazi ya malipo.

Idara ya utabiri wa hali ya Hewa nchini imewatahadharisha wakenya dhidi ya kuishi kando ya mito iliyofurika. Wanafunzi ambao tayari walikuwa wamefika shuleni walitakiwa kubaki shuleni na usimamizi wa shule ungewahifadhi na kuhakikisha usalama wao.

Maswali:

a) Huku ukirejelea aya nne za kwanza, eleza athari hasi za mabadiliko ya tabianchi.
(Maneno80) **(alama 8)**
Matayarisho
Nakala safi

b) Fafanua masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya tano za mwisho**. (maneno 70)**
(alama 7)
Matayarisho
Nakala safi

MATUMIZI YA LUGHA. ALAMA 40

a.Andika muundo wa silabi katika neno Nyaraka. **(alama1)**
b. Bainisha dhamira katika sentensi zifuatazo. **(al 2)**
i).Mzazi wake aliwasili mapema.
ii).Meza tembe mbili mara moja kwa siku.
c.Tunga sentensi yenye kiwakilishi nafsi kiambata katika ngeli ya KI-VI **(al 2).**
d.Onyesha miundo miwili ya nomino katika ngeli ya A-WA. **(al 1)**
e.Tunga sentensi katika wakati ujao hali endelevu. **(al 2).**
f..Kwa kutoa mfano,eleza matumizi ya alama ya ritifaa. **(al 2)**
g.Ainisha neno lifuatalo; **(al 3)**
Niliyemtembelea
h.Onyesha yambwa tendwa na chagizo katika sentensi uliyopewa. **(al 3)**
David alimpelekea mama zawadi zilizokuwa nzuri ajabu.
i.Andika katika usemi wa taariifa. **(al 3)**

"Nitakuita kesho ili uwahutubie mahabusu". Beavon alimwambia Ochako.

j. Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mistari. **(al 4)**

Wembe alioutupa mama ulimkata mtoto vibaya sana.

k.Tunga sentensi katika hali kanushi inayoonysha kuwezekana kwa jambo. **(al 2).**

l.Eleza matumizi ya KU katika sentensi ifuatayo: **(al 2).**

Kucheza kwake vizuri hakukumzuia kuingia kulikokuwa maji mengi.

m.Eleza uamilifu wa vishazi tegemezi katika sentensi zifuatazo: **(al 2).**

i.Aliyeshinda amezawadiwa.

ii.Mtaka cha mvunguni,sharti ainame.

n.Kanusha sentesi ifuatayo; **(al 1).**

Nitaimba na kucheza kesho asubuhi.

o. Kando na kuonyesha nafsi,fafanua matumizi mengine ya kiambishi ni kwenye sentensi uliyopewa;

Niliwashangaa alipouliza kilichonipeleka nyumbani kwao **(al 2)**

p.Tunga sentensi ukitumia kihisishi cha kushukuru. **(al 1).**

q. Tambua virai kwenye sentensi hii; **(al 2)**

Wao wabaya walipigwa vibaya sana.

r. Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo. **(al 1)**

Jason alisafiri kuelekea ng'ambo.

Anza kwa;

Ng'ambo……

s.Thureya ni kwa nyota,…….…….ni kwa milima,……....ni kwa nyuki. **(ala 1)**

t.Tunga sentensi ukitumia kisawe cha maneno uliyopewa. **(al 2)**

i). Rafiki …….

ii).Bezo……

ISIMU JAMII. ALAMA 10

Yule wa 2A amekuwa akikohoa kama mwehu. Asije akaenda jongomeo hapa,mwite daktari aje amsaidie.

A. Kwa kutoa mfano,tambua sajili hii. **(al 2).**

B. Tambua mbinu za lugha katika sajili hii. **(al 2).**

C. Fafanua sifa mwafaka za sajili hii. **(al 6).**

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA KWANZA)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3 (FASIHI)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

c) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*

d) *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima.***

e) *Maswali hayo mengine* ***matatu*** *yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; Riwaya, Ushairi, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.*

f) ***Usijibu*** *maswali mawili kutoka sehemu moja.*

g) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
JUMLA	80	

SEHEMU A: RIWAYA
NGUU ZA JADI

1. LAZIMA

Jadili namna waketwa wanavyopambana dhidi ya uongozi dhalimu wa mtemi lesulia. **(al 20)**

SEHEMU B: TAMTHILIA
BEMBEA YA MAISHA

2. *"Wakati huo sikuona.sasa ninaona.Wanasema mwenye machi haambiwi tazama.kweli iliyoje!"*

a).Eleza muktadha wa dondoo hili. **(al 4).**

b). Tambua mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo hii.. **(al 4).**

c).Fafanua namna mwandishi amefanikisha mbinu rejeshi kwa kurejelea tamthilia ya bembea ya maisha. **(al 12).**

AU

3.*"Lakini watafanyaje?Wakae tu vijijini kwa sababu mji unaenda mbio? Labda bembea yao ya maisha ipo pale mjini!*

a).Eleza muktadha wa nukuu hii. **(al 4).**

b).Pambanua mtindo katika kifungu hiki. **(al 5).**

c). Eleza sifa za mnenaji**.** **(al 3).**

d).Tambua matatizo yanayokumba jamii ya bembea ya maisha**.** **(al 8)**

SEHEMU C: HADITHI FUPI
SABINA.

4 ***"Akili za masomo huna…zinzchangamkia barua na mambo ya wanaume tu.Mamako alikuwa vivyo hivyo na unajua kilichomfika.Kweli mtoto wa nyoka ni nyoka!"***

a).Eleza muktadha wa hili. **(al 4)**

b).Tambua mbinu za kimtindo katika dondoo hii. **(al 4)**

c).Onyesha udhaifu wa msemaji katika dondoo hili. **(al6).**

d).Eleza matatizo yanayokumba mtoto wa kike kwa mujibu wa hadithi**.** **(al 6).**

AU

5. NILITAMANI.

i. Fafanua namna uhitaji umesababisha athari hasi katika hadithi ya **"Nilitamani".** **(Al20)**

SEHEMU D: USHAIRI

6. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata

Nchi ni ile ambayo, imekita ardhini
Siyo ile iombayo, ghaidhbu na majirani
Taratibu siyo hiyo, wananchi twambizaneni
Daima hukaa chini, maganja ya mpewa ji

Chumo lote na mitaji, leo lirao maganjani
Bepari na wanyonaji, wasalie maguguni
Shirine utekelezaji, vingine havifanani
Daima hukaa chini, maganja ya mpewa ji

Twaishije tujihoji, wananchi humu nchini
Kila tunachohitaji, kupatakwe ugenini
Hiyo ni tete haviji, tongo tupangusaneni
Daima hukaa chini, maganja ya mpewa ji
Kuomba wataalamu, ni mwendo hauh'ngani
Tupate wa humu humu, wajuzi wa kila fani
Mbele washike hatamu, kwa mapimo na makini
Daima hukaa chini, maganja ya mpewa ji

Tuufuate wongozi, pamoja na nyingi imani
Tushiriki kila kazi, na mambo yalomkini
Mikopo ina kinyezi, si kitu cha tumaini
Daima hukaa chini, maganja ya mpewa ji

Vote hatuyatimizi, alotimiza ni nani
Lakini tuwe maizi, tusizurure mijini
Tkamshabihi kozi, kipanga au kunguni
Daima hukaa chini, maganja ya mpewa ji

Shujaa itakiwavyo, aonekane vitani
Nasisi vita tunavyo, roho kwa roho ugani
'Kutegenia' vilivyo, kondo tujiamueni
Daima hukaa chini, maganja ya mpewa ji

MASWALI

a).Lipe sahiri jina mwafaka. **(al 2)**
b)Shairi hili ni la aina gani? Eleza. **(al 2)**
c). Mshairi huyu ana dhamira ipi?. **(al 2)**
d). Tambua bahari tofauti katika shairi hili**.** **(al 6)**
e). Fafanua namna mshairi alivyotumia uhuru wake**.** **(al 4).**
e).Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari. **(al 4)**

AU

7. MWILI

Leo kitaka nifike, natamani, ila wauma mwili
Kwa kazi nihusike, samahani, unahiliki mwili
Napenda nihiasebike, makundini, ila huwezi mwili.

Vitisho pamwe kelele, ninavicha, kwa nafsi na mwili
Ila ugonjwa utimile, umechacha, na kuudhili mwili
Msikose simile, magalacha, si gurudumu mwili.

Vingekuwepo viraka, kuutia, ngeushuruti mwili
Kifundi kivipachika, kuingia, hata kuridhi mwili
Upya ukaungilika, kuvutia, roho na wake mwili.

Lakini mweme haiwi, kuvipata, vipande vyake mwili
Sihofu kupata mawi, sitajuta, kupigania mwili
Hata kufutwa sikawi, nitakite kidete nao mwili.

Kazi ninaiithamini, hakika, akilini na mwili
Ila kamwe siamini, kusagika, damu, jasho na mwili
Uwele hususani, kioneka, nguvu hitishi mwili.

MASWALI

a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili**.** **(alama 2)**
b) Fafanua mbinu nne za lugha zilizotumika katika shairi hili. **(alama 4)**
c) Eleza toni ya shairi h**ili.** **(alama 2)**
d) Ni nani anayezungumziwa na nafsi ya kwanza katika shairi hili? **(alama 2)**
e) Eleza bahari ya shairi hili kwa kurejelea vipande**.** **(alama 4)**
f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya nathari. **(alama 4)**
g).Fafanua namna mshairi alivyotumia uhuru wake

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yanayofuata.

Wanitambua kote pwani
Amu hadi lunga kwa wangu weledi
Kiingia baharini papa atetema
Ndimi! Ndimi! dume la madume
Jabali mtetemesha bahari
Mvuvi bora pwani sina wa kupigiwa mfano
Ndoana yangu ni shahidi kwa niyasemayo
Nani wakupinga?aje tumenyane.

A) .Tambua kipera hiki na utoe mfano. **(al 2)**
B) Eleza sifa za kipera ulichokitaja. **(al 5).**
C) Fafanua umuhimu wa kipera hiki. **(al 5)**
D) Ni changamoto zipi zinakumba kuendelea kwa kipera hiki? **(al 4)**
E) Tambua njia mwafaka za kutumia ili kuhifdhi na kuendeleza kipera hiki **(al 4).**

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA PILI)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1

INSHA

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… **SAHIHI**……

NAMBARI YA USAJILI…… **MKONDO**……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Andika insha* ***mbili****. Insha ya* ***kwanza*** *ni ya* ***lazima.***

c) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*

d) *Kila insha isipungue maneno* ***400***

e) *Kila insha ina alama* ***20***

f) *Kila insha* ***lazima*** *iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
Jumla	40	

MASWALI

LAZIMA

1. Wewe ni rais wa muungano wa viranja jimboni mwako, umehudhuria semina ya viranja wakuu ulioandaliwa shuleni mwenu kujadili chngamoto zinazowakabili viranja kutekeleza wajibu wenu shuleni. Andika hotuba ambayo ungetoa kwa walimu wakuu kuhusu changmaoto hizo na mapendekezo yenu wakati wa kikao cha walimu wakuu jimboni.

2. Kenya ni mmoja wa inchi zinazowania kuwa mbele katika ulimwengu wa kisasa. Wewe ukiwa mzalendo fafanua vipingamizi au vijanzo vya ongezeko la bei ya bidhaa Nchini huku ukionyesha athari za ongezeko hili.

3. Mzigo wa mwenzio kanda la usufi.

4. Tunga kisa kinachoanza kwa maneneo yafuatayo:

5. Baada ya matokeo ya mtihani wa mwaka uliotangulia kutangazwa na katibu mkuu katika wizara ya elimu, iliniwia vigumu kusadiki ukweli wa mambo lakini nilielewa fika kuwa kuanguka mtihani siyo mwisho wa maisha…..

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.

KILA LA HERI!

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA PILI)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

c) *Jibu maswali* ***yote****.*

d) *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

e) *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

1. UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Wakati wananchi katika kila pembe ya dunia waliadhimisha siku ya wapendanao maarufu kama Valentine Day, kwa mitindo mbalimbali, hali hiyo ilikuwa tofauti kwa baadhi ya wanaume nchini Kenya, baada ya kulalamika kuhusu kunyanyaswa na wake zao.

Kulingana na Mwenyekiti wa Chama cha Kutetea Haki za Wanaume nchini, idadi ya wanaume wanaopigwa na wake zao imeongezeka mno. Alisema juzi kuwa utafiti wa chama chake umeonyesha kuwa harakati za kumpa uwezo mwanamke zimeathiri maadili na kuwasababisha kuwadharau wanaume. Mwanaharakati huyo anadai kuwa tatizo hilo limechochewa zaidi na hali ya kuwa wanawake wengi sas wana kipato kikubwa kuliko waume zao.

Mwishoni mwa wiki Polisi walimtia mbaroni mwanamke mmoja mjini Nyeri mkoani kati, baada ya kumshambulia mumewe na kumjeruhi vibaya kwa panga. Mwanamume huyo bado anapata matibabu hospitalini. Yeye alirudi nyumbani kama amevaa miwani ndipo akakatwa katwa usoni na uchunguzi kuhusu tukio hilo bado unaendelea.

Inadaiwa kuwa zaidi ya wanaume 460,000 walinyanyaswa na wake zao mwaka jana na kwamba utafiti wa shirika la kuwatetea wanaume unaonyesha kesi nyingi za wanaume kuteswa na wake zao zinaripotiwa katika Mkoa wa kati.

Hata hivyo, baadhi ya wanaume katika eneo hilo wameunga mkono hatua ya wanawake kuwashambulia waume zao. Wanasema kuwa, wanapigwa kwa sababu wamekosa kuwajibika kwa familia zao. Wanadai kuwa *wanaume wengine hawajulikani nyumbani kwao.* Wake zao wanawajua makasisi ambao huja kuwaombea kuhusu matatizo ya nyumbani huku mbwana zao wakizama katika ulevi. Wanawake na wanaume wa Nyeri wametak serikali ikomeshe uuzaji na unywaji pombe haramu ambayo imechangia sana ugomvi wa kinyumbani.

<u>Maswali</u>

(a) Upe ufahamu huu anwani mwafaka. **(alama 1)**

(b) **Eleza** sababu za wanaume kupigwa katika ndoa. **(alama 4)**

(c) Mwandishi anamaanisha nini anaposema kuwa wanaume wengine hawajulikani nyumbani kwao. **(alama 2)**

(d) Fafanua majukumu ya makasisi katika jamii kwa mujibu wa kifungu hiki. **alama 2)**

(e) Eleza mabadiliko katika asasi ya ndoa kwa mujibu wa kifungu hiki. **(alama 3)**

(f) Eleza maana ya vifungu hivi kama vilivyotumika katika tungo. **(alama 3)**

(i) Mwanaharakati

(ii) Amevaa miwani

(iii) Waliadhimisha

2. MUHTASARI

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali.

Baada ya kuchunguza kwa makini nimeshagundua kuwa wasanii maarufu huishi maisha ya kifalme. Jambo hili linadhihirika kweli ninapopiga darubini maisha yao. Mathalan,wanapoenda jamaa hawa, mashabiki hujitokeza kwa maelfu kuwalaki kuwashangilia na hata kuwatazama tu. Si ajabu kusikia sauti za watu wakisema, "Tunataka, jitokeze tafadhali tunakupenda."

Ikiwa hushangazwi na jinsi watu wengi wanajitokeza kuwashangilia wasanii, labda utaduwaa nikikwambia kuwa baadhi ya wasanii husafiri kwa magari ya bei ghali kama vile benzi na mengio.

Usishangae pia nikikwambia kuwa baadhi yao huruka kwa ndege zao wenyewe toka mahali pamoja hadi pengine. Kila waendako jamaa hawa aghalabu huwa wamezingirwa na mameneja wanaoendesha shughuli zao, mawakala wa vyombo vya bahari pamoja na walinzi. Ama ukiona maisha ya wasanii hao, utadhani kuwa unawaona wafalme au malkia wa nchi mbalimbali.

Ikiwa hujachoshwa na hayo, pulika nikueleze mengine; kama walivyo jamaa wa aila za kifalme, picha za wasanii maarufu au "walioukata", kama tusemavyo mitaani, wana kipato kizuri kama walivyosema waliotutangulia "Mtaka cha mvunguni sharti ainame", Jamaa hawa kipato kizuri kama wameshainama kweli na sasa wanafurahia jasho lao. Jamiiya leo hulipa wasanii maarufu pesa mzo mzo. Lakini heby nikwambie kuwa fedha wanazopapta jamaa hawa si za bure: huwa wamezifanyia kazi kweli.

Usidhani kuwa pesa wanazolipwa wasanii maarufu ni zao peke yao. Pesa hizo hulipwa kodi kubwa serikalini na kodi hiyo kutumika kuendeleza huduma muhimu kwa jamii. Kwa sababu hiyo sidhani kuwa tunapaswa kuwaonea kijicho watu na vipawa vyao.

Chochote king'aacho si dhahabu. Ingawa baadhi ya wasanii wana mapesa mengi yanayowawezesha kuishi maisha ya utukufu na anasa, tusifikiri kuwa wanaishi katika pepo. Baadhi yao huzongwa na mazonge mbalimbali kama vile kutokuwa na familia imara, kupatwa na upweke wa mara kwa mara au hata wakati mwingine kufilisika. Isitoshe baadhi ya wasanii maarufu hawawezi kutoka nje ya nyumba zao au kutembea mitaani kama wewe na mimi tufanyavyo. Ama wanaweza kudhuriwa au kuhangaishwa na mashabiki wao kwa kila njia kwa sababu hiyo wasanii wengi maarufu hawafurahii maisha kama watu wa kawaida. Ingawa wanalipwa vizuri, lakini malipo hayo yana bei yake.

a) "Wasanii huishi maisha ya kifalme" Eleza jinsi kauli hii inavyodhibitishwa na taarifa.

maneno 60- 65).

Nakala Chafu

Nakala safi

b) "Chochote king'aacho si dhahabu" Msemo huu umefafanuliwa vipi katika taarifa ?**Maneno 40-45**

Nakala Chafu **(Alama 5)**

Nakala Safi

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) **Tumia msemo ufuatao katika sentensi.** **(alama 1)**

Fanya lele mama

b) Tunga sentensi kuonyesha tofauti ya vitate hivi. **(alama 2)**

i) Mjusi

ii) Mjuzi

c) Andika katika hali ya umoja . **(alama 2)**

i) Masaibu yaliyowapata yaliwafanya wapoteze matumaini maishani.

ii) Machaka ya waridi hayazai maua meusi.

d) Andika katika hali ya ukubwa. **(alama 2)**

Asiye na mwana aeleke jiwe

e) Tumia neno <u>mwitu</u> kama; **(alama 3)**

(i) Kivumishi

(ii) Kielezi

(iii) Nomino

f)**Changanua sentensi hii kwa kutumia jedwali.**

Wanafunzi wote wamewasili lakini wengi walichelewa sana. **(alama 4)**

g) **Kwa kutoa mifano eleza sauti zifuatazo** **(alama 2)**

(i) Kipasuo – kwamizo

(ii) Kitambaza

h)**Eleza matumizi ya <u>KU</u> katika sentensi ifuatayo:** **(alama 2)**

Kusoma sana hakukumzuia kujiingiza kulikokuwa na wajinga.

i) **Kanusha** **(alama 2)**

Ungeipoteza kalamu yake, ungelazimishwa kuinunua nyingine.

j) **Andika kwa usemi halisi .** **(alama 2)**

Asha alimwita Halima na kumsihi waandamane kwenda kuogelea siku iliyofuata

k) **Bainisha nyakati na hali zilizotumiwa katika sentensi ifuatayo**. **(alama 4)**

"Mgeni wangu akija nitampokea kwa mikono miwili, ningekuwa na jimbi ningemchimjia"

Mwanaidi alimwambia Mzee Juma.

l) **Andika sentensi hii tena bila kutumia 'amba'** **(alama 2)**

Ng'ombe ambaye hupewa chakula kizuri ndiye ambaye hukamuliwa maziwa mengi.

m) **Andika kinyume cha maneno yaliyopigwa mstari** **(alama 2)**

Maina <u>aliushindika</u> mlango ili <u>avue</u> sidiria.

n) **Tambua yambwa-kitondo na yambwa-kipozi** . **(alama 2)**

Juma aliwachemshia wageni wake chai na kisha akawapelekea mezani.

o) **Huu ni ungonjwa gani?** **(alama 2)**

Kifaduro;

p) Kwa kutoa mifano onyesha tofauti kati ya Shadda na kiimbo. **(alama 2)**

q) Eleza matumizi mawili ya:

Ritifaa **(alama 2)**

r) **Eleza maana mbili za sentensi hii:**

Mzee huyu anaogopa magonjwa zaidi ya vijana. **(alama 2)**

4. ISIMU JAMII

Eleza huku ukitoa mifano mwafaka sifa tano za sajili ya bungeni. ` **(alama 10)**

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO KUPIGWA CHAPA

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA PILI)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… **SAHIHI**……

NAMBARI YA USAJILI…… **MKONDO**……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

(a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(c) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
(d) *Swali la kwanza ni la* ***lazima.***
(e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki;yaani:Riwaya, Tamthilia,,Hadithi Fupi na Ushairi.*
(f) *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka sehemu moja.*

Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	

SEHEMU YA USHAIRI.

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Alikwambia wako mama, kajifanya hupuliki,
Kakuosa kila jema, ukawa ng'oo! Hutaki,
Sasa yamekusakama, popote hapashikiki,
Uliyataka mwenyewe!

Babayo lipokuonya, ukamwona ana chuki,
Mambo ukayaboronganya, kujifanya hushindiki,
Sasa yamekunganya, kwa yeyote hupendeki,
Uliyataka mwenyewe!

Mazuri uliodhania, yamekuletea dhiki,
Mishikeli mia mia, kwako ona haitoki
Mwanzo ungekumbuka, ngekuwa huaziriki,
Uliyataka mwenyewe!

Dunia nayo hadaa, kwa fukara na maliki,
Ulimwengu ni shujaa, hilo kama hukumbuki,
Ya nini kuyashangaa? Elewa hayafutiki,
Uliyataka mwenyewe!

Mwenyewe umelichimba, la kukuzika handaki,
Ulidhania simba, hutishiki na fataki,
Machungu yamekukumba, hata neno hutamki,
Uliyataka mwenyewe!

Kwa mno ulijivuna, kwa mambo ukadiriki,
Na tena ukajiona, kwambawe mstahiki,
Ndugu umepatikana, mikanganyo huepuki,
Uliyataka mwenyewe!

Majuto ni mjukuu, huja kinyume rafiki,
Ungejua mwisho huu, ungetenda yalo haki,
Uko na roho juu, popote hapatuweki,
Uliyaka mwenyewe!

a) **Eleza** ujumbe unaojitokeza katika shairi hili. **(alama 5)**
b) Bainisha vipengele vitatu vya kimtindo katika shairi hili. **(alama 3)**
c) Eleza bahari ya shairi hili. **(alama 2)**
d) Bainisha ana mbili za urudiaji katika ubeti wa tano **(alama 2)**
e) Fafanua umbo la shairi hili**.** **(alama 4)**
f) Eleza toni ya shairi hili. **(alama 2)**
g) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya natha**ri.** **(alama 2)**

SEHEMU B: RIWAYA

C. MOMANYI: NGUU ZA JADI

JIBU SWALI LA 2 AU 3

2. "Mama yetu!! Mama yetu"…. Alikisogelea kipaza sauti. Sauti yake ilikuwa hafifu lakini aliweza kusikika."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Bainisha sifa mbili za anayetoa sauti. **(alama 2)**

c) Fafanua mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili**.** **(alama 4)**

d) Jadili umuhimu wa mhusika anayetoa sauti katika kuijenga riwaya ya Nguu za Jadi.**(alama 10)**

3.a**) Changanua mtindo katika dondoo hili** **(alama 5)**

"Umejuaje? Una ithibiti au ni uzushi tu?" Mwanamume mwingine aliyekuwa na sauti nene kama radi aliuliza. "Hatuwezi kumwona bwana Chifu? Lazima anaelewa mambo haya" ajuza mmoja aliyekaa mbali na wao aliuliza "Wapi! Kwanza huyo ndiye mnafiki mkubwa.

b)"Nchi ya Matuo inahitaji ujenzi mpya. Thibitisha kwa kurejelea hotuba ya Lonare. **(alama 15)**

SEHEMU C: TAMTHILIA

T.M AREGE: BEMBEA YA MAISHA

JIBU SWALI LA 4 AU 5.

4.a) "Aliyesema mwanao ndiye mwokozi wako siku za shida hakukosea."

ii) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

iii) Bainisha sifa mbili za msemaji wa maneno haya **(alama 2)**

iv) Thibitisha ukweli wa dondoo hili kwa kurejelea tamthilia hii**.** **(alama 4)**

b) Fafanua jinsi maudhui ya uwajibikaji katika ndoa yalivyoshughulikiwa katika tamthlia hii. **(alama 10)**

5. Eleza namna mwandishi alivyofaulu kutumia mbinu zifuatazo katika tamthilia ya Bembea ya maisha,

i) Kinaya **(alama 10)**

ii) Mbinurejeshi **(alama 10)**

SEHEMU D: HADITHI FUPI

D.W. LUTOMIA NA MUTHAMA (Wah) Mapambazuko ya Machweo na Hadithi nyingine

Jibu swali la 6 au 7.

6. **Winnie N. Ongeche: Sabina**

Baradhuli mkubwa wee… utanitambua! Uvundo ulitoka mwanamke huyu. Alibaki pale amejishika kiuno.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili**.** **(alama 4)**

b) Bainisha toni katika dondoo hili. **(alama 2)**

c) Fafanua mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili. **(alama 4)**

d) Eleza matatizo yanayomkumba mtoto wa kike kwa kurejelea hadithi ya Sabina. **(alama 10)**

7. Mzamane Nhlapo: Nipe nafasi.

"Huyu mwanamke anasoma Bibilia kweli? Atajifunza lini kutuheshimu?"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Fafanua umuhimu wa anayerejelewa katika dondoo hili. **(alama 6)**

c) Eleza jinsi wanawake wanavyokabiliana na changamoto zinazowakumba katika hadithi hii. **(alama 10)**

8. SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI.

Soma ufungo ufuatao kisha ujibu maswali.

Ewe mpwa wangu,
Kwetu hakuna mwoga,usiwe kama msichana,
Uoga ukikufika, huenda ni wa akina mamayo.
Fahali tulichinja ili uwe mwanamume
Iwapo utatingiza kichwa
Uhamie kwa wasiokatwa
Waume wa mbari yetu
Si waoga wa kisu
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo.

Simama jicho liwe juu
Ngariba alilala jikoni
Visu ametia makali
Kabiliana na kisu
Wengi wasema ni kikali
Mbuzi utampata
Na hata shamba la mahindi
Usiende kwa wasiotahiri

a)i) Thibitsha kuwa huu ni wimbo wa tohara. **(alama 2)**

ii) Bainisha shughuli mbili za kiuchumi katika utungo huu **(alama 2)**

iii) Eleza vipengele vitatu vya kimtindo katika utungo huu. **(alama 3)**

b) Fafanua umuhimu wa aina hii ya wimbo katika jamii **(alama 8)**

c) Eleza jinsi jamii inavyoweza kudumisha utungo huu ili usififie **(alama 7)**

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA TATU)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1 (INSHA)

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

g) *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

h) *Andika insha* ***mbili****. Insha ya* ***kwanza*** *ni ya* ***lazima.***

i) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*

j) *Kila insha isipungue maneno* ***400***

k) *Kila insha ina alama* ***20***

l) *Kila insha* ***lazima*** *iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
Jumla	40	

MASWALI

LAZIMA

1. Wewe ni Mkurugenzi mkuu wa kampuni ya Tia Fora. Wateja wa kampuni yako wamekuwa wakilalamikia huduma duni kutoka kwa kampuni yako. Imebainika kuwa wafanyakazi katika kampuni yako wanahusika katika hulka hizi duni. Andika arifa/memo ukiwaonya dhidi ya jambo hili.

2. Jadili jinsi wanafunzi wanavyoweza kuimarisha matokeo katika masomo ya sayansi.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mchimba kisima huingia mwenyewe.

4. Andika kisa kitakachoanza kwa maneno haya: Niliyafuta machozi. Uchungu uliokuwa moyoni uliyeyuka ghafla,tabasamu ikanivaa,nikawa tayari kukabiliana na hali yangu mpya liwe liwalo…..

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.

KILA LA HERI!

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA TATU)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

(a)Andika jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

(b)Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani.

(c) Jibu maswali yote.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
	80	

1 *Soma dayolojia ifuatayyo kisha ujibu maswali yanayofuata.*

(Bw. Akot na Bi Khadija wamekaa katika sebule ya mkahawa wakiendesha dayolojia kuhusu uwajibikaji wa viongozi waliochaguliwa)

Bw. Akot: Bibiye, yasikitisha sana kuona kuwa viongozi tunaowachagua hawaonyeshi hata chembe moja ya kuwajibika.

Bi Khadija: Ah! Ndio sasa unayafahamu hayo? Wanapotuomba kura hudai kuwa ni watumishi wetu. Pindi wachaguliwapo, utumwa unawagura na wanajitwika joho la ubwana. Lakini usisahau kuwa hali hii si ya hapa nchini tu bali ni ya bara zima la Afrika.

Bw. Akot:Ingawa ni tatizo la bara zima, hapa kwetu limekithiri mizizi. Hawa viongozi wetu wamezidi. Kila baada ya miaka mitano sisi wananchi huenda kupiga kura. Huwa na matarajio makubwa kuwa tunaowachagua watayajali na kuyashughulikia maslahi yetu. Wanatufanya tuamini haya katika kipindi cha kampeni. Ukiwasikia katika majukwaa ya kuomba kura wanavyotongoa lugha na kutoa msururu wa ahadi, utafikiri maisha yetu, yahe, yataimarika mara tu tutakapowachagua. Ole wetu! Ukiamini haya, wajihadaa. Zote hizi ni ahadi za upepo zinazopeperushwa na hewa pindi wanapopata ushidi.

Bi Khadija: Kumbuka kuwa lawama zote haziwaendei viongozi hawa tu. Hata sisi raia twapaswa kulaumiwa. Baadhi yetu ni viongozi wazuri lakini tunaogopa kujitosa kwenye siasa.

Bw. Akot: Kwa nini tulaumiwe ilhali si sisi tunaoupata uhondo wa uongozi?

Bi. Khadija: Hapo ndipo lawama zinapojia. Sisi raia twapaswa kulaumiwa kwa sababu ya kuwaamini viongozi zaidi kupita mipaka. Sisi tunawaachia majukumu yote watuongoze mithili ya ng'ombe anayeongozwa na mchinjaji. Badala ya kutumia nafasi zilizoko za kuwaandama ili wawajibike, sisi raia hubaki tukilia tu. Hatujui kuwa tuna njia za kulazimisha viongozi wetu kuwajibika!

Bw. Akot: Tutawezaje kutekeleza hayo ilhali tunapowachugua wanatuambaa kama wagonjwa wa ukoma? Muda wa kuwapata ni baada ya miaka mitano wanapokuja kutuomba tuwapigie kura tena.

Bi. Khadija: Tusikate tama. Wakati huo ndio mwafaka kwetu kutumia kiboko tulichonacho kuwaadhibu wale ambao hawakutekeleza wajibu wao. Tunapaswa kutumia wakati huo kuwapiga kalamu walioshindwa kutekeleza majukumu yao. Kisha tusikomee hapo. Tunapaswa kuwachuja kwa makini viongozi tunaowachagua. Hatupaswi kukubali kuhadaiwa

kwa porojo na ahadi zisizotimia. Ili kutekeleza haya ni muhimu kujua wajibu wa kila kiongozi anayechaguliwa.

Hii ndiyo sababu wengi wetu raia huhadaika kwa urahisi wakati wanowania viti vya uwakilishi wanapotoa ahadi za kutujengea mbinu msingi kama shule, barabara na hospitali. Huu huwa uongo mtupu. Ujenzi wa mambo haya ni wetu raia kupitia kwa serikali. Ujenzi huu hutekelezwa kutoka kwa pesa tunazozitoa kama kodi. Jukumu la wabunge ni kuhakikisha wanapigania ujenzi huu utekelezwe katika maeneo wanayoyawakilisha. Ahadi hizi za uongo hazipaswi kuwa kigezo chetu cha kuwateua.

Bw. Akot: Lakini ukumbuke kuwa wanaotaka kuchaguliwa hutujia kwa hila nyingi.

Bw. Khadija: Hayo sipingi. Umma unapong'amua kuwa wanaotaka kuchaguliwa hutumia hila, unapaswa kukaa ange na kuzitambua hila hizo na kuzipiga vita. Tatizo letu kubwa sisi

tunaowachagua ni kutojua wajibu wetu.Pili, wengi wetu huwa wasakatonge na tunaporushiwa vihela kidogo kama chambo, tunakimbia kuziuza haki zetu na za watoto wetu. Kwa njia hii, tunawachagua viongozi wasiotujali na wanaotupotezea wakati pamoja na kuyahatarisha maisha yetu na ya watoto wetu.

Bw. Akot: Wengi wao hubadilika na kuanza kutubeza kuwa sisi ni wahuni, wavivu na watu wasiostaarabika. Wengine hujilimbikizia mashangingi yanayomeza mafuta kama sijui nini. Juu ya haya hutembea na misururu ya magari na makundi ya wapambe na walinzi. Baadhi yao wamehamia kwenye makasri makubwa yenye vyumba sita vya kulala na vidimbwi vya kuogelea. Yote haya kwa gharama ya yule mpigakura mlalahoi.

Bw. **Khadija**: Mwenzangu, usisahau kuwa mimi na wewe tuna wajibu wa kuwaelimisha wenzetu kuhusu wajibu wao katika uchaguzi wa viongozi.

Bw. **Akot**: Ninakubaliana nawe kabisa. Naomba tushikane bega kwa bega ili tutoke katika giza hili.

MASWALI

(a) Ni kwa namna gani viongozi waliochaguliwa hawaonyeshi chembe ya kuwajibika? **(ala 1)**

(b) Eleza mchango wa wapiga kura katika hali ya uongozi nchini mwao. **(alama 4)**

(c) Eleza maoni ya Bi. Khadija katika kufanikisha uongozi bora **(alama 4)**

(d) Bainisha mbinu wanazotumia viongozi ili kufanikisha ushindi wao kulingana na kifungu **(alama 3)**

(e) Andika maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa kwenye kifungu**. (alama 2)**

(i) Limekithiri mizizi

(ii) Wasakatonge

2 UFUPISHO (alama 15)

CHIMBUKO LA KISWAHILI

Kiswahili ni lugha ambayo huzungumzwa na takriban watu milioni mia moja kote ulimwenguni. Pia, ni lugha ya saba ulimwenguni na ya pili barani Afrika kwa kuwa na wazungumzaji wengi. Asili ya lugha hii imetafitiwa na wanaisimu na wanahistoria. Kuna maoni aina tatu kuhusu asili na chimbuko la Kiswahili. Baadhi ya watu kama F. Johnson, C. Meinhof, Akofu Steere, W.E. Taylor, G.W.Broomfield, W.H.Whitely na wengineo wameshikilia kuwa Kiswahili ni lugha mseto. Wasomi hawa wanadai kuwa Kiswahili kimetokana na maingiliano ya lugha za Kibantu na lugha za kigeni kama vile Kiajemi, Kiarabu na Kihindi. Wanaoshikilia wazo hili husema kuwa Kiswahili kilizuka ili kufanikisha mawasiliano katika shughuli za kibiashara. Wao wanasisitiza kuwa Kiswahili hakikuwepo kabla ya kuja kwa wageni.

Kuna madai pia kuwa Kiswahili ni lahaja ya Kiarabu. Dhana hii inapotosha kwa sababu inaonyesha kuwa kabla ya kuja kwa wageni kwenye upwa wa Afrika Mashariki hapkuwa na Kiswahili. Wazo hili si sahihi kwa sababu hakuna lahaja ya aina hii huko Uarabuni. Pili Waarabu pia walienda Afrika Magharibi kupitia Afrika Kaskazini, mbona lahaja ya namna hii haikuzuka huko?

Maoni ya mwisho ni kuwa, Kiswahili ni mojawapo ya lugha za Kiafrika yenye asili ya kibantu kama vile Kihaya, Kikuyu, Kiyao, Kimeru na Kigiriama. Lugha hii ya Kibantu iliweza kukopa maneno

ya kigeni kutoka kwa lugha za Kiarabu, Kiingereza, Kijerumani, Kihindi, miongoni mwa zingine. Ukopaji huu ulitokana na maingiliano ya jamii hizi kupitia kwa biashara na utawala.

Maoni yanayoshikiliwa sasa ni kuwa Kiswahili ni lugha ya Kiafrika yenye asili ya Kibantu. Ithibati ya kutosha imetolewa kupitia kwa utafiti wa Kiisimu, Fasihi Simulizi na Historia (mapisi).

Uchunguzi wa isimu historia na isimu linganishi uliofanywa na M Guthrie mwaka wa 1948 unaonyesha kuwa Kiswahili kina uhusiano na lugha zingine za Kibantu hasa tunapotazama mashina ya maneno mengi kutoka lugha mbalimbali za Kibantu. Maneno ya asili kama vile kichwa, mkono, maji, njia na majina ya wanyama katika lugha hizi yanahusiana, na hivyo kubainisha kuwa yalitoka kitovu kimoja.

Baada ya Wabantu kufanya makazi katika sehemu ya Mto Tana walishambuliwa na Wagalla. Baada ya mashambulizi haya Wabantu walitawanyika na kuanza makazi mapya kuanzia sehemu ya Modagishu upande wa kaskazini, hadi sehemu ya Mto Pangani, upande wa kusini. Baadhi yao walivuka Bahari ya Hindi na kwenda kufanya maskani yao katika visiwa vya Unguja. Pembe za Ngazija. Katika maeneo haya waliendelea kuzungumza lugha zao za Kibantu, lakini kutegemea wakati na umbali kati yao, tofauti za kimatamshi na msamiati zilizuka. Tofauti hizi zilisababisha kuwepo kwa lahaja mbalimbali za Kiswahili. Miongoni mwa lahaja hizi ni Kiamu, Kipate, Kingare, Kimvita,Kivumba, Kingazija, Kinzwani, Kipemba, Kiunguja, Kitumbatu, Kibajuni, Kisiu miomgoni mwa zingine.

Jambo lingine ni kuwa Kiswahili kina irabu tano kama zilivyo lugha nyingi za Kibantu. Irabu hizi ni a, e,i,o, na u. Hali kadhalika muundo wa msamiati wa Kiswahili kimsingi huchukua konsonanti – irabu - konsonanti –irabu. Kwa mfano; kigoda, maji, baba. Hata hivyo konsonanti mbili au tatu zinaweza kufuatana. Kwa mfano **nyw**ele, **pw**ani, **ngw**ena, **afy**a na mengine mengi.

Mpangilio wa nomino za Kiswahili huleta uwiano wa kisarufi na huitwa ngeli za nomino. Hujitokeza katika lugha zingine za Kibantu. Mfano wa mpangilio wa nomino hizi ni ngeli ya **KI-VI, U-I, A-WA, LI-YA**. Nomino hizi zinapotumiwa katika lugha ya Kiswahili huwa na uwiano na vitenzi. Jambo hili pia hujitokeza katika lugha zingine za Kibantu, na kudhihirisha kuwa Kiswahili ni mojawapo ya lugha za Kibantu.

Katika maoni ya fasihi simulizi, asili ya Kiswahili ni Kingozi. Mashairi ya Hamziya yaliyoandikwa katika karne ya 18 yaliandikwa kwa Kiongozi. Kiongozi kilikuwa kikizungumzwa sehemu iliyoitwa Ushwahili upande wa visiwa vya Magunyoni(Pate, Lamu, Faza) hadi bara kupakana na Mto Tana

Asili ya neno '*Kiswahili*' inasemekana ilitoka na kijana wa Kingozi aliyeulizwa na wageni (wasafiri wa Kiarabu) kuwa wao ni kina nani? Akajibu kuwa "*Sisi ni Wa-ziwa hili*." Yaani wenyeji wa ziwa hili. Kutegemea wakati na matamshi, jina hili lilibadilika na kuwa Waswahili

(a) Eleza ujumbe unajitokeza katika aya za kwanza tatu (Maneno 90, alama 9, 1 ya mtiririko)

Nakala chafu

Nakala safi

(b) Thibitisha kuwa Kiswahili ni lugha ya Kiafrika yenye asili ya kibantu. (Maneno 60. Alama 4,1 ya mtiririko)

Nakala chafu

Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Ni sauti gani haifai kuwa miongoni mwa hizi. Toa sababu **(alama 2)**

i. */ng'/ /g/ /t/ /k/*

ii. */s/ /v/ /ch/ /sh/*

(b) Andika neno lenye muundo ufuatao **(alama 1)**

Nazali ya ufizi, kipasuo ghuna cha kaakaa laini, irabu ya juu nyuma, irabu ya nyuma wastani.

(c) Ainisha mofimu katika neno walionana **(alama 3)**

(d) Eleza maana ya mzizi wa neno **(alama 2)**

(e) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano. **(alama 2)**

i. nywa (kutendwa) _____

ii. fa(kutendwa) _____

(f) Eleza matumizi ya maneno yaliyopigiwa mstari katika jozi ya sentensi hizi: **(alama 2)**

<u>Huyu</u> ni mkufunzi msomi.

Mkufunzi <u>huyu</u> ni msomi sana

(g) Ziandike upya sentensi zifuatazo kwa kufuata maagizo kwenye parandesi **(alama 6)**

(i) Niliwaeleza wazazi wetu kwa dhati.Walikuwa wamepigwa mafamba hadi hawakuamini niliyosema. (**Anza:** Wazazi…)

(ii)Watoto wanaovaa nguo fupi fupi siku hizi wamethiriwa na tabia za kigeni. (Anza kwa: Nguo fupi…)

(iii) Mtaalamu alituambia kwamba kusoma kwa mapana kungepalilia ubunifu wa wanafunzi wale wetu. (Andike kwa usemi halisi).

(h) Alama ya kiulizo hutumiwa katika sentensi ambayo ni swali. Eleza matumizi mengine ya alama hii. **(alama 1)**

(i) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi 'O' **(alama 2)**

(j) Ichanganue sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha visanduku **(alama 3)**

Marekebisho ambayo yamefanywa yanavutia sana.

(k) Geuza sentensi ifuatayo iwe kwa wingi **(alama 2)**

Mwanzi alioupanda karibu na mto umeshikana ukawa msitu mkubwa.

(l) Ashua ni mwanafunzi aliye na matatizo ya kibanafsi katika masomo yake. Licha ya yeye ni mwanafunzi bora shuleni. Hakuna anayeelewa changamoto zake kwa kuwa ameziweka siri. Huenda akasitisha masomo ikiwa hatapata msaada. Ni methali gani inayoweza kumfaa Ashua? **(alama 1)**

(m) Tunga sentensi moja itakayotofautisha maana ya *baa* na *paa*. **(alama 2)**

(n) Tambua aina za virai katika sentensi hii **(alama 2)**

Wanafunzi wote walizawidiwa na Rais.

(o) Kanusha sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Ukimwona Bakari umwambeia nitamtembelea kesho.

(p) Tunga sentensi itakayodhihirisha shamirisho kitondo na chagizo **(alama 2)**

(q) Iandike sentensi ifuatayo katika kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari. **(alama 2)**

Onyango <u>alihama</u> Kilifi baada ya <u>kuchimba</u> makaburi.

(r) Yakinisha sentensi ifuatayo katika nafsi ya pili umoja **(alama 1)**

Hataenda shuleni kesho

(s) Andika maana ya misemo ifuatayo **(alama 2)**

fanya inda_____

Changa bia_____

4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)

Umealikwa kama mshauri nasaha katika shule moja ya upili inayokumbwa na tatizo la mihadarati miongoni mwa wanafunzi. Andika sifa kumi za lugha utakazozingatia ili kufaulisha uwasilishaji wako.

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA TATU)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO:

a) *Jibu maswali manne pekee.*
b) *Swali la kwanza ni la lazima.*
c) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya,Ushairi, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.*
d) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
e) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	
Jumla	80	

SEHEMU A:

FASIHI SIMULIZI

LAZIMA

1. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali

Mimi ni Olichilamgwara
Olichilamgwara mwana mbee wa Ojilong
Ojilong wa Marukatipe
Wazee waliposhindwa
Nilivuka misitu milima na mito
Ni mimi jabali
Kipande cha jifya la mama
Nilipokuwa nalisha mifugo
Nilisikia baragumu inalia
Baragumu ya wito
Mifugo wa mtemi wamechukuliwa
Nikachukua mkuki wangu
Wenye kigumba cha mti
Nikachukua upanga wangu
Wenye makali kama mmweso wa radi
Upanga uliopasua pembe za nyati kwa dhoruba moja
Ndipo nilipofyatuka kasi kama umeme
Kufumba kufumbua nikawakaribia nduli
Kusikia vishindi vyangu wakaanza kubabaika
Kuona kifua changu cha manyoya ya kanga wakatetemeka
Macho yangu makali kama kaa la moto yalipowatazama wakakimbia
Mkuki wangu ulipaa kama umeme
Wote wakalala
Mifugo wakanifuata…
Mko wapi vijana
Mmekuwa kama majivu baada ya moto kuzimika?

Maswali

a) Tambua kipera ulichokisoma na udhibitishe jibu lako **(al. 2)**
b) Tambua sifa za jamii zinazosawiriwa katika utungo huu **(al. 2)**
c) Kwa kutoa mifano bainisha vipengele vine vya kimtindo vilivyotumiwa na nafsineni**al. 4)**
d) Fafanua sifa nne za kipera hiki **(al. 4)**
e) Eleza mambo manne ambayo mtendaji wa kipera hiki anaweza kufanya ili kufanikisha utendaji wake. **(al. 4)**
f) Fafanua mikakati ambayo jamii inaweza kutumia ili kuzuia tungo kama hizi kufifia**(al. 4)**

SEHEMU YA B: USHAIRI

Jibu swali la 2 au 3

2. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:**

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki,
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki
Ukweliwe haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo,
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakazifuata nyago,
Hadi kwenye wao ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Pindi kinunua kitu, hafurai Shaitani, bali tajawa chukizo,
Mtu kiwa mtukutu, tanunua mtimani, kwalo lako tekelezo,
Tamko lake 'Subutu', kuondoa tumaini, na kukuulia wazo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Aliye na taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai,
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,
Hana faida nyumbani, ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliejaa uchoyo,
Bahati ina hadaa, kukupa alo sadawi, aibatili rohoyo
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza vunja kaniyo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Ninacho change killo, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa matatizo kuambiwa,
Ama nitumie mbio, fuadi ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

MASWALI:

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. **(alama 1)**

b) Fafanua mambo **matatu** ambayo nafsineni analalamikia. **(alama 3)**

c) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. **(alama 3)**

(i) Idadi ya vipande katika kila mshororo

(ii) Mpangilio wa vina katika kila ubeti

(iii) Idadi ya mishororo katika kila ubeti

d) Andika ubeti **wa nne** katika lugha nathari. **(alama 4)**

e) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. **(alama 2)**

f) Huku ukitoa mifano, onyesha mbinu mbili alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. **(alama 2)**

g) Andika aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. **(alama 2)**

h) Fafanua muundo wa ubeti **wa tano**. **(alama 3)**

3. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Ee mpwa wangu,
Kwetu hakuna muoga,
Uoga ukikufikia, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tilichinja ili uwe mwanamume,
Eewe mpwa wangu, kisu kikali ajabu!
Iwapo utatingisa kichwa,
Uhamie kwa wasiotahiri.

Wanaume wa mbari yetu,
Si waoga wa kisu,
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo,
Wewe ndiye wa kwanza,
Iwapo utashindwa,
Wasichana wote,
Watakucheka,
Ubaki msununu,
Simama jiwe liwe juu
Ndege zote ziangamie.

Simu nimeipokea,
Ngariba alilala jikoni,
Visu ametia makali,
Wewe ndiye wangojewa,
Hadharani utasimama,
Macho yote yawe kwako,
Iwapo haustahimili kisu,
Jiuzulu sasa mpwa wangu,
Hakika sasa mpwa wangu,
Hakika tutakusamehe, mwaka kesho unakuja.

Asubuhi ndio hiii,
Mama mtoto aamushwe,
Upweke ni uvundo,

Iwapo utatikisa kichwa.
Iwapo wewe ni mme,
Kabiliana na kisu kikali,
Hakika ni kikali!

Kweli ni kikali!
Wengi wasema ni kikali!
Fika huko uone ukali!
Mbuzi utapata,
Na hata shamba la mahindi,
Simama imara,
Usiende kwa wasiotahiri.

Maswali

a) Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha **(al. 2)**
b) Tambua anayeimba na anayeimbiwa shairi hili **(al. 2)**
c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi za kiume **(al. 2)**
d) Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili **(al. 4)**
e) Taja shughuli zozote mbili za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili **(al. 2)**
f) Eleza mbinu alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiuarudhi **(al. 4)**
g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili? **(al. 4)**
   i) Mbari
   ii) Msununu
   iii) Ngariba
   iv) Uvundo

SEHEMU C: TAMTHILIA; BEMBEA YA MAISHA – TIMOTHY M. AREGE

Jibu Swali la 4 au 5.

4. "Huku ndiko kuvumilia hasa. Tazama faraja ilivyoalika sasa"

a) Weka dondoo hili katika muktadha. **(alama 4)**
b) Eleza sifa za msemaji katika dondoo. **(alama 6)**
c) Onyesha jinsi faraja ilivyoalika katika maisha ya msemewa kwa kurejelea tamthilia ya: Bembea ya Maisha. **(alama 10)**

AU

5.

(a) Changanua mtindo katika kifungu kifuatacho. (alama 10)

Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo. Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. (*Kimya*). Siku hazigandiwala jana hairudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika. (*Kimya*). Kwa bahati nzuri bado tupo. Ninaweza

kuiachia dunia tabasamu iwe silesi kwa vizazi vijavyo na kila mwenye nia njema. (*Kimya*). Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Lazima niache njia ya zamani na kuifuata mpya. Maisha mapya. Pombe! *(kama anayeisemea pombe).* Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu. Hapana! Siku zangu za uzeeni lazima nizitumie kumwangalia mke wangu mgonjwa. Lazima nimshukuru kwa vitendo kwa jinsi alivyojitolea kuijenga familia yetu. *(anapunga mkono.)* Kwaheri pombe. Buriani.

b) Bainisha toni ya dondoo hili. **(alama 2)**

c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kuijenga tamthilia nzima**.(alama 8)**

SEHEMU D: HADITHI FUPI

Jibu swali la 6 au 7

6. Harubu ya maisha *Paul Nganga Mutua*

"Naja. Nakamilisha shughuli ndogo hapa kisha nianze safari…"

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake **(al. 4)**

(b) Eleza sifa sita za msemaji wa kauli hii **(al. 6)**

(c) Jadili changamoto wanazokumbana nazo waajiriwa kwa kurejelea hadithi hii **(al. 10)**

7. D.W .LUTOMIA : *Msiba wa kujitakia*

Wetu ni wetu ,hata akiwa mbaya …ni wetu.hatuna budi kuchagua yeye .lisilobudi hubidi.

(a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (**alama 4)**

(b)Fafanua vipengele vya kimtindo katika dondoo hii. (**alama 4**)

(c)Hiari ya maamuzi ya wahusika mbalimbali yamewaletea madhila anuwai.jadili.(**alama 12**)

SEHEMU YA E: RIWAYA- NGUU ZA JADI

8. Hivyo,alitaka kubadili hali hata kama ilimaanisha kukitia kichwa chake kinywani mwa samba. Alitaka kuliokoa jahazi lililokuwa likielekea mwambani kwa kasi. Lakini angeliweza vipi kupambana na utandu wa mahasisi hao?.

(a) Eleza mbinu nne za mimtindozinazojitokeza katika dondoo **(al 4)**

(b) Eleza sababu za msemaji kutaka kufaulisha kauli iloyopigiwa mstari **(al 10)**

(c) Eleza umuhimu wa msemaji katika kujenga ploti ya riwaya hii **(al 6)**

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA NNE)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1

INSHA

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO KWA MTAHINIWA:

a) *Andika jina lako, nambari ya usajili na tarehe katika karatasi ya majibu.*
b) *Karatasi hii ina maswali manne.*
c) *Jibu maswali mawili pekee. Kila swali lina alama ishirini.*
d) *Swali la kwanza ni la lazima.*
e) *Chagua swali lingine lolote moja kutoka yale matatu yaliyosalia.*
f) *Majibu yote yaandikwe katika karatasi ya majibu uliyopewa.*

Sehemu hii imehifadhiwa kwa matumizi ya mtahini pekee.

SWALI	1	2	3	4
UPEO	20	20	20	20
ALAMA				

UPEO	40
ALAMA ZA MTAHINIWA	

MASWALI

1. Wanakijiji katika mtaa wa Nadhifu wanakumbwa na tatizo la taka zilizorundikana katika mazingira yao. Wanamazingira walikutana kuzungumzia swala hili. Andika kumbukumbu zilizotokana na mkutano huo**.** **(al 20)**

2. Ajali nyingi za barabarani husababishwa na makosa ya kibinadamu. Jadili. **(al 20)**

3. Andika kisa kitakachoafiki methali ifuatayo**:** **(al 20)**

Bura yangu sibadili kwa rehani.

4. Andika insha itakayokamilika kwa maneno yafuatayo; **(al 20)**

…Mungu mikononi mwako tunazikabidhi roho zetu.

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.

KILA LA HERI!

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA NNE)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2 (LUGHA)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

- *Andika **jina lako** na **namba yako** katika nafasi ulioachiwa hapo juu.*
- *Jibu maswali yote.*
- *Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

1. UFAHAMU – (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

Takwimu zinaonyesha kuwa punda hutumika kubeba mizigo mizito mashinani, hususan katika maeneo ambayo miundo misingi ya barabara ni duni. Aidha, wasimamizi wa vichinjio vya punda wamelaumiwa kwa kuhatarisha maisha ya wanyama hawa kupitia biashara ya viungo vyao, huku wezi wa punda wakivuna sehemu ambayo hawakupanda.

Hata hivyo, kwa mama Teresia Mumbi, mkulima kutoka kijiji cha Kwa Njaga, Kaunti ya Nyandarua, punda wamekuwa ni ofisi yake. Anasema ukulima na uchukuzi kwa Wakenya wengi unategemea miundo msingi bora ya usafiri, ndio maana wakulima wengi mashinani wamekuwa wakilalamika kuwa wanapata hasara mazao yao yanapochelewa kufika sokoni kwa wakati. Kulingana naye ni jambo ambalo limewafanya kuwekeza kwenye mradi wa kufanya biashara ya punda ambapo mara nyingi huuzwa kati ya Sh20,000-25,000. Ingawa wakulima wengi kutoka Kaunti ya Nyandarua wanakuza viazi, maharagwe, mihogo na mahindi, Mumbi anasema kuwa hajutii kujikita kwenye mradi huu, ambao umetengeneza nafasi nyingi za ajira na kurahisisha usafiri.

Kulingana naye, anaungama kuwa endapo wakulima watawapatia punda mafundisho mwafaka jinsi ya kuishi na mifugo, wanaweza kukaa na wanyama wengine kama vile kondoo, mbuzi au ng'ombe na hata kuwapatia ulinzi. Wakulima wamekuja na mbinu mwafaka ya kufanikisha ufugaji kwa kukata kwato, kuwapatia chanjo na kuwatengenezea mazingira mazuri.

Isitoshe punda ni wanyama ambao wanaweza kujitafutia malisho na kudumu katika mazingira magumu yenye joto au baridi kali. Kwa upande mwingine wakulima wengi kutoka Nyandarua ambao wanategemea punda, wamekuja na mbinu ya kuboresha ufugaji wa punda baada ya kupokea mafunzo kutoka kwa wataalam na wanaharakati wanaotetea haki za punda.

Kwanza punda wanafaa kubebeshwa mizigo kulingana na uwezo wao. Aidha wanahitaji wakati wa kutosha kupata mapumziko.

Mumbi amefaulu katika ufugaji wa punda kwa sababu yeye huhakikisha kuwa punda wake wanapata maji ya kutosha wakati wowote ambao huwa hawafanyi kazi. Vilevile, amewatengenezea punda wake watatu banda nzuri kuwakinga dhidi ya mvua, baridi kali au jua. Mumbi anasema kuwa kila siku akiamka huhakikisha kuwa punda wake wamelishwa vyema na kuwapangusa kwato kabla ya kurejelea shughuli za siku kusafirisha mazao kutoka shambani hadi sokoni. Baada ya kufanya vibarua sehemu mbalimbali miaka ya awali, Mumbi aliamua kutafuta mbinu mbadala ya kujiendeleza kimaisha ambapo alinunua mtoto wa punda na kumtunza hadi akakomaa.

Hapo alianza kutengeneza hela kwa kufanya vibarua kijijini kama vile kubeba mizigo, au kukodisha kwa wafanyabiashara wengine na hata kubebea maji kutoka mtoni. Ikumbukwe kuwa kijiji cha Kwa Njaga kina miundo msingi duni ambapo miinuko na mabonde hufanya nyingi ya sehemu zisiweze kupitika hasa wakati wa mvua nyingi. Alieleza kuwa imekuwa ni nafuu kwa vijana wengi na akina mama ambao walikuwa wamezoea kushinda mtaani, kwa sababu punda wametoa fursa ya kutengeneza nafasi nyingi za kazi.

Barabara nyingi katika Kaunti ya Nyandarua hazipitiki, jambo ambalo limekuwa likiwafanya wakulima kukadiria hasara kubwa mazao yao yanapochelewa kufika sokoni. Changamoto za wakulima wa matunda na mboga zilikuwa nyingi huku wengi wao wakikosa kujua namna ya

kuhifadhi mazao ya shambani mara tu baada ya kuvuna. Hapo awali watu wengi hawakuwa wakizingatia maslahi ya punda kama vile kuwaacha wajitafutie vyakula na kuishi kwenye mazingira duni.

Beth Kuria ambaye ni mwekahazina kutoka Shirika la Muungano wa Wamiliki wa Punda nchini (ADOK), anasema kuwa pana haja ya serikali kutilia mkazo suala la kuwahifadhi punda kwenye mazingira mazuri. Wafugaji wengi wameshindwa kuwapatia punda malazi mazuri na lishe bora, jambo ambalo amelitaja kama kuwakosesha haki zao za kimsingi.

Kama wanyama wengine punda wanahitaji kupatiwa lishe nzuri na chanjo kila mara, hii ikiwa ni pamoja na kuwafanyia huduma za kukata kwato na kuwawekea matandiko mazuri wakati wa kubebea mizigo ili ngozi zao zisije zikachujuka. Aliongezea kuwa akina mama wengi wanaokaa mashambani wanategemea punda kufanyia kila kitu kama vile kusafirisha viazi hadi sokoni na hata kuwabebea maji kutoka mtoni.

MASWALI

a) Ipe tarifa uliyoisoma anwani mwafaka **(alama 1)**

b) Eleza mambo ambayo yamekuwa yakiwahasisri wakulima katika Kaunti ya Nyandarua. **(alama 2)**

c) Eleza njia nne zinazoweza kutumiwa kufanikisha ufugaji wa punda **(alama 4)**

d) Eleza faida nne zinazotokana na ufugaji wa punda **(alama 4)**

e) Kwa nini ufugaji wa punda umekuwa rahisi ikilinganishwa na mifugo wengine **(alama 2)**

f) Eleza maana ya mafungu yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu **(alama 2)**

i.Punda wamekuwa ni ofisi yake…….....

ii. Kutengeneza hela…….…….....

SEHEMU B: UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

Lugha huundwa kwa sauti ambazo huunganishwa ili kuunda neno au sehemu ya neno, kisha maneno huungana kuunda miundo mikubwa zaidi yenye maana kama vile virai, vishazi, sentensi na aya. Kwa mfano: Mkulima (N) + Anavuna(T) = Mkulima anavuna. Hata hivyo, muungano huu wa maneno huwa haufanyiki shaghala baghala maadamu kuna kanuni na sheria zinazodhibiti mfuatano wa kila kipashio.Katika kila lugha, kuna kanuni maalum zinazodhibiti ama mfuatano wa sauti, mofimu, maneno au hata sentensi.

Kwa mintarafu hii, ndiposa tunahoji kuwa lugha ya binadamu ni mfumo wenye kanuni, sheria na taratibu mahsusi ambazo endapo zitakiukwa, hakutakuwa na utimilifu wa lugha husika. Wanajamii au ukipenda watumiaji wa lugha fulani huweza kuelewana kupitia kanuni hizo maalum zinazodhibiti mpangilio wa viunzi vya lugha husika.

Lugha ni mfumo wa sauti nasibu**8**. Kiambajengo hiki kina maana kwamba hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya neno na kitu chenyewe kinachotumika katika ujenzi na matumizi mengine (maana na kirejelewa). Inamaanisha vilevile kuwa ishara na maumbo ya kiisimu hayana uhusiano wowote au mfanano wowote na maana ambazo tunayapatia. Kwa mfano, neno 'jiwe' hakuna watu waliokaa na kusema kuanzia leo hili litaitwa jiwe. Aidha, hakuna uhusiano wowote kati ya neno "jiwe" na umbo linalorejelewa, ila uhusiano wake ni wa kinasibu tu na hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine.

Lugha huhusishwa na mwanadamu. Lugha ni chombo cha mawasiliano kinachotumika miongoni mwa binadamu pekee ambapo hakuna kiumbe mwingine ambaye si binadamu mwenye uwezo wa kutumia lugha wala kuzungumza. Kwa kuzingatia hoja hii, ni bayana kuwa kuna sifa maalum za lugha ya binadamu ambazo hazipatikani kwa kiumbe mwingine yeyote yule isipokuwa mwanadamu. Japo viumbe wasio binadamu mathalan wanyama na nyuni wanaweza kuwasiliana, mawasiliano yao huwa ni ya sauti au ishara ambazo kimsingi si lugha.

Aidha, mawasiliano haya hudhibitiwa na hisia kama vile uchungu, hofu, njaa,hamu au ishara za kutoa taarifa fulani. Isitoshe, binadamu ana uwezo wa kujifunza lugha mbalimbali na kuitumia katika mazingira yake jambo ambalo wanyama, nyuni na viumbe wengine hawawezi. Kwa mfano, ukimchukua mbwa wa Japan na kumleta Kenya atabweka kwa njia ile ile ya mbwa wa Kenya kueleza shida au ishara husika.

MASWALI

a) Kwa maneno yasiozidi 60 fupisha aya mbili za mwanzo (alama 7, moja ya utiririko)
Majaribio
Jibu

b) Kwa maneno 70 fafanua sifa za lugha zinavyojitokeza katika aya ya tatu hadi tano.
(alama 8, moja ya utiririko)
Majaribio
Jibu

3. SEHEMU C MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Andika neno lenye sauti sauti zifuatazo: sauti mwambatano ya ufizi, irabu ya chini, nazali ya ufizi, irabu ya mbele juu **(alama 2)**

b) Kuna tofauti gani kati ya kiimbo na shadda **(alama 2)**

c) Huku ukitoa mifano, eleza maana za maneno yafuatayo **(alama 3)**
viambishi
mofimu

d) Tunga sentensi moja inayodhihirisha kwamba neno panda ni kitawe. **(alama 2)**

e) Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi ya KU kama kikanushi cha wakati uliopita na

nafsi ya pili umoja **(alama 2)**

f) Tunga sentensi moja iliyo na shamirisho kipozi, kitondo na ala **(alama 3)**

g) Tunga sentensi kusisitiza katika wingi 'kiti' kikiwa mbali kidogo. **(alama 2)**

h) Changanua sentesi ifuatayo kwa kutumia jedwali **(alama 4)**

Mwanafunzi aliyeadhibiwa jana ameomba msamaha lakini mwalimu mkuu hajamsamehea

i) Eleza uamilifu wa vishazi tegemezi katika sentensi zifuatazo: **(alama 3)**

i. Aliyepotea amepatikana

ii. Mwanafunzi aliyepotea amepatikana

iii. Tulicheza alivyotufundisha

j) Andika kwa wingi **(alama 1)**

Mtanashati ameibuka mshindi

k. Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Huyu ndiye mwalimu anayejua kukimbia kwa kasi

l) Weka nomino hizi katika ngeli zake **(alama 2)**

i. vilembwe

ii. maghani

m) Yakinisha: Usingalitia bidii usingalipita mtihani. **(alama 2)**

n) Andika katika usemi wa taarifa: 'Nataka ufikirie sana juu ya maisha yako ya ndoa. Sitaki uishi maisha yasiyo na mweleko.' Babu alinishauri. **(alama 3)**

o) Baya ni kwa zuri kama vile …….. ni kwa tamu na bovu ni kwa ……... **(alama 2)**

p) Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya viakifishi vifuatavyo **(alama 3)**

i. ritifaa

ii. kinyota

iii. parandesi

q) Eleza maana ya **(alama 2)**

i. kuzamia lulu

ii. Dudu liumalo silipe kidole

4. SEHEMU D: ISIMU JAMII (ALAMA 10)

a) Huku ukitoa mifano mwafaka fafanua kaida nne katika jamii ambazo matumizi ya lugha hutegemea **(alama 4)**

b) Fafanua majukumu ya Kiswahili kama: **(alama 6)**

i) Lugha ya kitaifa

ii) Lugha ya kimataifa

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA NNE)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3 (FASIHI)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)

MAAGIZO:

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

c) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*

d) *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima.***

e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Hadithi Fupi.*

f) *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja****.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	
Jumla	80	

SEHEMU YA A: USHAIRI

MBELE YA SAFARI

1. Ilipoanza safari , ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

2. Njaa ikawa dhabiti ,na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti ,dhila na mingi mikiki
Tukajizatiti

3. Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari,utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari , juhudi iliyobaki
Tukajizatiti

4. Ile ilikuwa ndoto , mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto,sahala 'mekuwa dhiki
Wagombanio kipato,utashi haukatiki
Nakutabakari

5. Msafara ukasita , kwenye mlima wa haki
Kijasho kinatuita , mlima haupandiki
Basi sote 'kijipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina

6. Tukiwa migongo wazi ,tukainama kwa shaki
Tukawa'chia ukwezi , kialeni wadiriki
Wakapanda bila kazi ,Kuteremsha miliki
Wakaitapia

7. Wakafikia makazi,ya pumbao na ashiki
Huko wakajibirizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma ulomiliki
Mbele ya safari

8. Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema , kwa umati halaiki
Imezima nia yote ,kiza hakitakasiki
Mbele ya safari

(a) Eleza safari inayolejelewa katika shairi hili. **(al 2)**

(b) Onyesha kinaya cha safari inayozungumziwa. **(al 6)**

(c) Taja na ueleze bahari mbili za shairi ukizingatia **:** **(al 4)**

i. Mizani

ii. Vina

(d) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari. **(al 4)**

(e) Eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa sita **(al 4)**

(f) Eleza umbo/ muundo wa shairi hili. **(ala 2)**

SEHEMU YA B: TAMTHILIA

Timothy Arege;BEMBEA YA MAISHA

Jibu swali la 2 au la 3

2. (a.) Soma dondoo lifuatalo kasha ujibu maswali.

Sara : Mimi ninashukuru kwa hawa alionipa mungu. Nikitaka zaidi nitakuwa mchache wa shukrani.(kimya) Dina nimesemwa sanana kutukanwa kwa sababu ya hawa wasichana wangu. Wewe unajua yote yaliyosemwa, hadharani na faraghani. Si makanisani, si magengeni. Leo nikiviona vitoto hivi vilivyochekwa na kusimangwa jana, vikijiendeshea mambo yao, ninaridhika moyoni. Hata nikiitwa nitaondoka nikiwa nimeridhika. (Anatokwa na machozi)

Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha.

i.) Changanua maudhui katika dondoo hili **(ala 3)**

ii.) Bainisha toni katika dondoo hili **(ala 2)**

iii.) Tambua mbinu tatu za lugha ambazo zimetumiwa katika dondoo hili. **(ala 3)**

(b.) Jadili jinsi suala la utu linavyoshughulikiwa katika tamthilia ya Bembea Ya Maisha **(ala 12).**

AU.

3. Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(ala 20)**

SEHEMU YA C: RIWAYA;C. MOMANYI: **NGUU ZA JADI**

Jibu swali la 4 au la 5

4. "Lazima amejiunga na kundi la marafiki wenye pesa wanaojaribu kumpotosha."

(a) Eleza muktadha wa dondoo. **(alama 4)**

(b) Anayesema maneno haya ni jasiri. Thibitisha kwa hoja tano. **(alama 5)**

(c) Tathmini kwa hoja kumi na moja nafasi ya wenye pesa katika kuendeleza tamaa na ubinafsi katika nchi ya Matuo. **(alama 11)**

AU

5. "Mangwasha siku zote hizi ulikuwa unachezeshwa kayamba tu. Ati walisema Osama alikuwa hatari kwa usalama duniani; kuna Osama kuliko huyu?" alijiskia kusema. Alishusha pumzi kwa nguvu akajiuliza kimoyomoyo kwa nini Mungu aliruhusu moto kumtia kwenye shimo la maangamizi na wanawe. Hata hivyo, aliamini kuwa wakati mwingine Mungu huruhusu mabaya kutokea ili kuwafunza waja. Waaidha, alijua kuwa mashaka yanapomkumba mja, huwa ni funzo pia. Humtayarisha kuyahimili machungu zaidi ulimwenguni ama kumuasa dhidi ya kuabudu

maovu. Maovu yanapotendwa na wachache, hata wale wasio na hatia pia hujikuta wamo humo uovuni. Ni mtego wa waliomo na wasiokuwemo.

(a) Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 5)**

(b) Eleza umuhimu wa mandhari ya kanisani aliko Mangwasha katika kukuza Riwaya ya Nguu za Jadi **(alama 5)**

(c) Nchi ya matuo imeshinikizwa na Nguu Za Jadi zinazorudisha nyuma usawa katika jamii. Tathmini kauli hii kwa hoja kumi. **(alama 10)**

SEHEMU YA D :HADITHI FUPI

MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE

Jibu swali la 6 au 7

WINNIE NYARURI OGENCHE: ''SABINA''

1. ''Maneno ya ripota huyo yalimwiingia Ombati maskioni yakasalia huko.Hayakufika akilini.Mwalimu mkuu alipenya kwenye umati uliokuwa umeanza kuwa mkubwa na kumtaka Ombati awaelekeze alikokuwa Sabina .Kabla ya Ombati kuwajibu,Sabina alifika nyumbani amevaa rinda kuukuu huku harufu ya samadi inamvuka.Watu waliokuwa wakimngoja walimzoa juujuu na kuanza kuimba tena. Ombati aliwafurusha wageni waliokuja kumwoa Sabina pamoja na mifugo wao.Baada ya kufanya hivyo,alijiunga na Sabina kuhojiwa na kupigwa picha.Alijitanua jinsi alivyotunukiwa kumlea mwana mwepesi masomoni.''

a) Eleza umuhimu wa mhusika Sabina katika **kukuza hadithi husika**. **(alama 6)**

b) Kwa kutoa mifano mwafaka kutoka kifunguni,onyesha **aina nne za taswira** zilizojitokeza. **(alama 4)**

c) Fafanua **changamoto** zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi hii. **(alama 10)**

YUSSUF SHOKA HAMAD: ''*Mzimu wa Kipwerere*''

7."…Kabla mwanamke yule hajakiwasha kile kibatari,nilijitokeza mle mvunguni na maguo yangu meupe kama ya maiti nikaangua mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama."

(a)Yaweke maneno haya katika muktadha wake. **(Alama 4)**

(b)Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. **(Alama 4)**

(c)Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. **(Alama 2)**

(d)Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha *mlinda mzimu na wahenga waliotukuka* kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini mzimu wa Kipwerere kiasi cha kutofanya mzaha na maeneo yale ambayo mzimu uliotea.. **(alama 10)**

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

Swali la nane

8. a) Ulumbi ni nini**?** **(alama 2)**

ii) Ulumbi hutekeleza **majukumu** gani katika jamii?. **(alama 6)**

iii) Eleza **vipengele sita** vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. **(alama 6)**

b) Eleza namna ambavyo hadhira huhusishwa katika uwasilishaji wa fasihi simulizi.**(alama 6)**

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA TANO)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1 (INSHA)

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

m) *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

n) *Andika insha* ***mbili****. Insha ya* ***kwanza*** *ni ya* ***lazima.***

o) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*

p) *Kila insha isipungue maneno* ***400***

q) *Kila insha ina alama* ***20***

r) *Kila insha* ***lazima*** *iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. Rafiki yako anayesomea katika shule jirani amefukuzwa shule kwa sababu ya ukosefu wa nidhamu.Mwandikie barua ukimshauri kuhusu umuhimu wa kuwa na nidhamu shuleni.

2.Teknolojia ya kisasa ina faida na madhara kwa vijana wetu.Jadili.

3.Andika kisa kitakachoonyesha ukweli wa methali : **Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.**

4.Andika insha itakayoishia kwa:

…Ilinichukua muda mrefu kuyaamini niliyoyaona.

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA TANO)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
c) *Jibu maswali* ***yote****.*
d) *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
e) *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

UFAHAMU (ALAMA 15)

Shule Yangu Ya Upili

Majio yangu katika shule hii ya upili hayakutokea kwa bahati nasibu bali kwa mipango kabambe niliyoianza tangu nikiwa shule ya vichekechea.Nikiwa sitetereki hata kwa wazazi wangu waliponisihi nijiunge na shule nyingine za karibu nikawa sisikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini.Nikawa na ragba ya mkanja nikingoja siku ya kujiunga na shule yenyewe.Kweli majuto ni mjukuu na huja kinyume.

Nilizaliwa katika aila yenye nafasi iliyotopea na kubobea katika ukwasi uliodhihirika kutokana na mitaa tulikoselelea kwa muda kabla ya baba kuaamua kununua nyumba yake mwenyewe huko upande wa Karen hivyo tukagura kutoka Lunda.Wakatiwa likizo tukawa tunaruka hadi pwani ambako mama yangu alikuwa amemiliki jumba lililokuwa katika ufuo wa bahari lililojengwa katika kipande kisichopungua ekari tatu alilotunukiwa wakati wa nikahi yao na wakwe wa baba yangu.

Wavyele wangu wakawa wanaendesha magari meusi ya kifahari ingawa sikuwahi kumwona mama akichangamka kuendesha magari yake ya maana,kila macheo ya siku za kazi gari lililoendeshwa na dereva ambaye alimstahi mama hadi akawa anamfungulia mlango wa gari na kuufunga baada ya mama kujitoma katika tumbo la gari lilimjia na kumrejesha kwa wakati.Nikajiunga na shule ya msingi ya kibinafsi ambako nilishughulikiwa kama kikembe.Wengi wa wale tuliosoma nao walikuwa wa tabaka langu na walikuwa wametoka katika kila sehemu nchini Kenya.

Hayawi hayawi huwa na siku ya kuripoti ikafika.Alfajiri,dereva mmoja akatumwa kwenda hadi Kisumu ili atulaki na kutusafirisha kutoka uwanja wa ndege hadi shule ya upili ambayo ilikuwa yangu ya rohoni.Nasi tukaelekea hadi uwanja wa ndege ili turuke hadi Kisumu.Safari yetu kutoka kitongoji cha kifahari hadi Airport ilikuwa njema,safari yetu tulipoabiri ndege ilikuwa bila bughudha,safari yetu kutoka Kisumu mjini haikuwa na kasoro na tulienda kulingana na mpango.Safari yetu ilikuwa mufti hadi tulipofika katika langa la shule ya kitaifa!Tulipotia ozi tu!!....jamani.....jamani nikafa moyo.Labda mama aliweza kubaini mabadiliko ya hisia zangu,nilitamauka, nikawa mchege na kusema kweli niliyoyaona sikuamini.Mvua iliyokuwa imepasua hapo awali ilikuwa imeacha vitua vya maji kwenye vijia vya kutembea vilivyochakaa na kubomoka bila yeyote kuja kuvikarabati.Majengo yalikuwa makongwe yaliyojengwa miaka mia moja iliyopitana yalistahili kuitwa makavazi badala ya pahali pa kumkaribishia mwanafunzi aliyepita kwa alama mia nne na thelathini na tano.Asiye na wake ana Mungu,nikapiga moyo konde lazima nisajiliwe katika shule ya ndoto yangu.Ningewezaje kughairi wazo langu baada ya siku hizo zote za maandalizi tena mbele ya wanuna walioniona kama kielelezo chao tangu walipozaliwa.Nikasajiliwa!

Sikujua shule ya upili ya kitaifa yaweza kuwa hivi.Kweli mwanafunzi aweza kukosa viatu na hatakushindwa kununua rangi ya kupaka viatu hivyo iwapo amenunuliwa na wahisani?Nilimlaumu nina maana hakunieleza kuwa mtu anaweza kula chakula ambacho mbwa wetu hawezi hata kukiangalia.Nilipoingia katika ukumbi wa chakula nilihisi kitefutefu nusura nichafukwe na moyo. Makapi ya mboga na uchafu usioelezeka ulinikumba,kisha nikapewa kisahani cha plastiki na

kupakuliwa kipande cha ugali ambacho bado kilikuwa na unga na kuachiwa hiari ya kukila au kukitupa.Wenzangu wakawa wanakirambatia chakula kwa kasi huku mmoja wao alipoona jinsi nilivyokiangalia changu akanisihi nimpe chote na kukimaliza fyu.Wote walikuwa na furaha kemkem na kuajabia utukufu wa shule iliyotukuka ya kitaifa ila mimi. Baada ya mlo'rojorojo',tukaelekea darasani nilikopigwa na mghuma mkubwa. Tulikuwa wanafunzi hamsini na watano katika darasa moja tu! Mwalimu mmoja akaja na kutukaribisha shuleni kisha akatuarifu kuwa atakuwa mwalimu wa darasa letu.Nilipomsikia akinena nusura niishiwe na stahamala,kimombo chake kilinishangaza,hasa matamshi yake yalipungukiwa na kudhihirisha athari za lugha ya asili.Nilihisi kana kwamba ningemrekebisha lakini sikudhubutu.

Tukafululiza hadi bweni na nikajilaza kitandani chembamba huku mwingine nisiyemjua lakini asiyejua kuwa kuna nguo maalum za kulala akalala uchi katika ghorofa ya juu ya kitanda chetu.Mgeni njoo mwenyeji apone maana baada ya muda wadudu ambao sikuwahi kuwaona aushini mwangu wakaanza kunishambulia. Nikaamka baada ya kumnasa mmoja wa wadudu hawa na kuuliza mmoja wa wenzangu ni wapi wadudu hawa na kwa kutojali hata kidogo,akanieleza kuwa hawana neno bali ni kunguni tu,Sikujua na kwa kweli mama hakuniambia kuwa kuna wadudu wanaotafuna mtu na hunuka fye! Sikulala kwa hofu huku wenzangu wakiforota kwa njia ya kunighasi.Sikuwahi kudhani kuwa watu wengi wanaweza kulala chumba kimoja huku changu kikiwa na hamamu na vifaa vyote muhimu kikibaki bila mtu! Tulisomeshwa na walimu wasiojali kana kwamba tunaelewa au la.

Hawakushughulika iwapo tulifanya kazi za ziada aula,ndio,hakujali chochote. Kilichonishangaza ni kuwa wanafunzi waliojiunga nasi kutoka shule za umma wenye alama duni waliwapenda na kuelewa haraka walichosomeshwa na hawakujali matamshi yao,labda hawakuyatambua. Hatimaye tukafanya mtihani wa mwisho wa muhula wa kwanza.Nilishangaa ghaya iliponibainikia kuwa aliyetuongoza alikuwa ghulamu mmoja mshamba niliyempuuza tu mvulana kutoka kijijini ambacho singetambua katika ramani ya nchi ambaye hata vitu vya kimsingi vilimpiga chenga.Nikafanya uchunguzi nikatambua mwenzangu alikuwa na alama mia mbili hamsini na tatu akitoka katika darasa la nane. Nilifanikiwa kuwa nambari mia mbili hamsini na tatu kwa jumla ya wanafunzi mia tatu! Tulipofunga kwa likizo ya Pasaka nikaamua kuchukua hatua nyingine: Sitawahi kuhama kutoka shule hii ya upili wala kuwa zaidi ya nambari kumi!

Maswali

Thibitisha kauli kuwa msimulizi ana msimamo thabiti**.** **(alama2)**

Tofautisha jinsi mwandishi alivyofunzwa katika shule ya kibinafsi na shule ya upili**.** **(alama 2)**

Taja mambo matatu yanayotuonyesha kuwa msimulizi alilelewa katika aila ya kikabaila kulingana na aya ya pili. **(alama3)**

Andika masuala matatu yaliyomshangaza katika shule ya upili**.** **(alama3)**

Andika tamathali mbili zilizotumika katika kifungu**.** **(alama2)**

Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika kifungu**.** **(alama3)**

Alimstahi……

Kughairi…….

Kunighasi…….....

SEHEMU B:UFUPISHO (ALAMA15) ; ***Soma kifungu kisha ujibu maswali.***

Ripoti za kila mara kuhusu uharibifu wa pesa za umma katika serikali za kaunti ni za kusikitisha.Kuna mabilioni ya pesa za kulipa ushuru ambazo hufujwa katika serikali kuu,na hivyo basi wananchi wanakosewa sana wanapoona mtindo huu ukiendelea pia katika serikali za kaunti.Wakati katiba ilipopitishwa mwaka wa 2010,Wakenya wengi walikuwa na matumaini mno kwamba ugatuzi ungewatatulia matatizo ambayo walikuwa wakipitia katika tawala zilizotangulia,hasa katika maeneo yaliyotengwa kimaendeleo.

Miaka tisa baadaye,kuna mafanikio ambayo yamepatikana ila hatua kubwa zaidi inaweza kupigwa katika kuboresha maisha ya kila raia kama mianya inayotumiwa kufuja pesa za umma itazibwa.Wizi huu unaojumuisha pia jinsi magavana wanavyobuni nafasi za kazi zisizo na maana ambazo wakati mwingi hupeanwa kwa jamaa na marafiki wao,ni sharti ukomeshwe mara moja.

Kuna wananchi wengi ambao tayari wameanza kufa moyo kuhusu umuhimu wa ugatuzi ilhali ukweli ni kwamba hatungependa kurejelea utawala ulio chini ya serikali kuu pekee.Changamoto za ugatuzi zinazosababishwa na ulafi wa viongozi wachache zinatoa nafasi kwa wakosoaji wa mfumo huu wa uongozi kushawishi wananchi na hata wahisani wasishughulike kuchangia katika maendeleo ya kaunti zao.

Juhudi zozote zile za maendeleo haziwezi kufanikishwa bila ushirikiano kutoka kwa wananchi na wahisani na hivyo basi ni jukumu la viongozi kuonyesha nia ya kutumia mamlaka waliyopewa kwa manufaa ya raia.Tume ya maadili na kupambana na ufisadi (EACC) kufikia sasa imeonekana kufanya kazi nzuri kwa kuwasaka na kuwashtaki magavana walio mamlakani na wengine walioondoka,kwa kushukiwa kufuja mali za umma.Tungependa asasi zote zinazohusika na masuala ya kupambana na uhalifu, pamoja na wadau wengine katika jamii wenye nia njema kwa wananchi wasifumbie macho maovu yanayotendwa katika kaunti zetu.

Nchi hii inatawaliwa kwa misingi ya kisheria na hivyo basi hakuna sababu kumhurumia kiongozi yeyote anayekiuka sharia anapokuwa mamlakani kwa msingi wa mamlaka aliyoshikilia.Ni kupitia adhabu kali za kisheria pekee ambapo tutafanikiwa kukomesha uongozi mbaya kwani kama wananchi watakuwa wakisubiri kuwaadhibu wahusika kwa kuwaondoa mamlakani pekee,watakuwa wametoa nafasi ya ufujaji kwa viongozi wapya kila miaka mitano.

(Kutoka gazeti la Taifa Leo)

(a)Fupisha ujumbe wa aya tatu za kwanza kwa maneno 80. (alama8,1 yamtiririko)

Matayarisho

Jibu

(b)Fupisha aya mbili za mwisho kwa maneno70. (alama7, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

Jibu

SEHEMU C: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

Andika neno lenye muundo ufuatao; **(alama 2)**

Kikwamizo sighuna cha mdomo meno,irabu ya mbele juu,nazali ya midomo,kipasuo ghuna cha midomo na irabu ya nyuma wastani.

Tunga sentensi kwa kutumia kiwakilishi huru cha nafsi ya tatu umoja**.** **(alama 2)**

Tambulisha vipashio vitatu vya lugha ya kiswahili**.** **(alama 3)**

Tumia neno 'vibaya' kama; **(alama 2)**
Kivumishi
Kielezi
Tunga sentensi moja katika wakati ujao hali endelevu**.** **(alama 2)**
Eleza matumizi ya 'ni' katika sentensi hii. **(alama 2)**
Ingieni darasani mara moja ili niwape zoezi ambalo ni rahisi.
Ainisha vielezi vya namna katika sentensi hii. **(alama 2)**
Mzee huyu mkongwe alicheka kijinga huku akila haraka haraka.
Tambua miundo mitatu ya ngeli ya LI-YA. **(alama 3)**
Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo. **(alama 3)**
Kimani aliukata mti kwa kisu jana asubuhi.
Andika kwa usemi wa taarifa**:** **(alama 2)**
Karani: Njoo nikutume kwa baba yangu.
Kamau: Sitaki kupita njia ya kwa babu.
Nimenunua dawa ili iwamalize wadudu wanaotusumbua hapa kwetu nyumbani**.** **(alama 2)**
Anza: Wadudu
Andika kwa ukubwa hali timilifu**.** **(alama 2)**
Mtego ulimnasa ndovu huyo.
Bainisha vishazi katika sentensi fuatayo. **(alama 2)**
Ingawa alitia bidii masomoni,alifeli mtihani.
Tambua aina mbili za sentensi ukizingatia uamilifu na utoe mfano mmoja kwa kila moja.**(ala 2)**
Taja na utolee matumizi mawili ya mkwaju. **(alama 2)**
Changanua sentensi hii kwa kutumia kielelezo cha visanduku. **(alama 4)**
Waswahili husema chema chajiuza kibaya chajitembeza.
Andika sentensi moja ukitumia kitenzi ulichopewa katika kauli ya kutendewa**.** **(alama 1)**
Ja
Bunda ni kwa noti ,na bumba ni la nyuki ilhali _____ ni kwa karatasi**.** **(alama 1)**
Kamilisha methali hii**.** **(alama 1)**
Mfa maji

SEHEMU D: ISIMU JAMII (ALAMA 10)

Kibiko: Hujambo dada Cheupe?
Cheupe: (akikohoa) Sijambo ndugu Kibiko.
Kibiko: Unaendelea namna gani?
Cheupe: Niko poa isipokuwa maumivu kidogo ya chest.
Kibiko: Usijali nitakupa pain relievers utakuwa sawa.
Cheupe: Asante sana,nashukuru.

Maswali.

Eleza muktadha wa mazungumzo haya**.** **(alama 2)**
Taja na ueleze sifa za lugha iliyotumika katika mazungumzo haya. **(alama 8)**

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA TANO)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3 (FASIHI)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

(a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

(b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

(c) *Jibu maswali **manne** pekee.*

(d) *Swali la kwanza ni la **lazima.***

(e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani:Riwaya, Tamthilia,,Hadithi Fupi na Ushairi.*

(f) *Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja.*

Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	

SEHEMU A: HADITHI FUPI (LAZIMA)

D.W. Lutomia na Phibbian Muthama : Mapambazuko Ya Machweo Na Hadithi Nyingin Lazima

Athari ya mawazo yake ilijiandika dhahiri shahiri usoni mwake. Alianza kwa kuachia tabasamu pana mithili ya msafiri aliyefika salama. Baada ya dakika chache, machozi yalianza kumtoka njia mbilimbili huku kajishika tama. Alifikiria kuhusu mtihani uliodhamiriwa kuanza siku ya Jumanne. Mtihani ambao ungemwezesha kupata ufadhili katika shule ya upili ya bweni ikiwa angepita vyema. Hili ndilo wazo lililozua tabasamu. Lakini, angefeli je? Hatima yake ingekuwa ipi? Maswali haya yalimliza yakamwacha akisinasina kama mgonjwa wa mafua. Akiwa katika hali hii, aliyakumbuka maneno ya mwalimu mkuu, "Mizizi ya elimu ni michungu ila matunda yake ni matamu. Ikiwa mnataka kuyaonja matunda ya elimu, lazima mtie bidii kwani mtaka cha mvunguni sharti ainame."

Akiwa amezama kwenye lindi la mawazo, alizinduliwa na sauti ya Yunuke ikimwita, "Sabina! Sabina! Sabinaa!"

Changanua mtindo kwenye kifungu. **(alama 8)**

Suala la kazi na bidi limeangaziwa kwa kina kwenye diwani ya mapambazuko ya machweo. Tetea ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi zifuatazo:

Fadhila za punda

Mapambazuko ya machweo

Sabina **(alama 12)**

SEHEMU B: RIWAYA

Clara Momanyi: Nguu za Jadi.

Jibu swali la 2 au la 3

2. **"***atawatoa wananchi wa Matuo kutoka katika mchanga wa moto unaowaunguza."*

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake_ **(aL4)**

b) Tambua mbinu ya uandishi katika dondoo hili. **(aL2)**

c) Kwa kurejelea riwaya nzima, Fafanua jinsi wahusika mbalimbali wanaunguzwa naserikali **(aL14)**

3. Eleza jinsi Mtemi Lesulia amejenga usaliti katika riwaya ya Nguu za Jadi. **(aL20)**

SEHEMU C: TAMTHILIA

Timothy Arege: Bembea Ya Maisha

Jibu swali la 4 au la 5

4. "Hata nikiitwa nitaondoka nikiwa nimeridhika."

a)Eleza muktadha wa dondoo hili . **(alama 4)**

b)Kwa hoja **tano**, eleza sifa za msemaji wa maneno haya . **(alama 5)**

c)Tambua mbinu **moja** ya lugha iliyotumika katika dondoo hili. **(alama 1)**

d) Wahusika mbalimbali kwenye tamthilia wamekubwa **na majonzi na furaha**. Thibitisha. **(alama 10)**

5. "...Tayari unakuwa umeonja seli.Hata wahudumu wenyewe hawana mlahaka mwema .amri na vitisho kama askari.Unashindwa kama uuguze moyo ama ugonjwa.Katika wodi hewa iliyojaaa harufu ya dawa imezagaa,vitanda vimesalimu amri mpaka shiti zikagura.Yaani hali nzima haikupi matumaini ya kutoka ukiwa bora.matumaini yanadidimia .Tumaini lako unaliweka katika sala. "

(a) Tambua toni mbili katika kifungu **hiki** **(alama 2)**

(b) Tambua aina mbili za taswira katika dondoo hili **(alama 2)**

(c) Kando na taswira chambua vipengele vingine vya kimtindo **(alama 6)**

(d) Fafanua namna mandhari ya dondoo hili yalivyochangia kujenga tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(alama 10)**

SEHEMU D: USHAIRI.

Jibu swali la 6 au la 7

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Taifa ni Ushuru

Lau kama ingakuwa, madhali tuna uhuru
Watu kodi kutotowa, na kuifanya kufuru
Vipi nchi ingakuwa, taifa bila ndururu
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Hivi taifa kumea , nakuendelea mbele
Kwamba lajitegemea, haliwategei wale
Yataka kujitolea, ushuru bila kelele
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Wafanyikazi wa umma, mfano mwema walimu
Wauguzi mahashuma, daktari wahadimu
Bila hizi darahima, vipi wangalihudumu?
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Si vyema kuombaomba, kwa wageni kila mara
Huwa twajifunga Kamba, na kujitia izara
Adha zinapotukumba, kujitegemea bora
Taifa halingakuwa,bilashi bila ushuru

Miradi ya maendeleo, yahitaji darahima
Ndo tufikie upeo, ulio dunia nzima
Wadogo na wenye vyeo, bila kodi tutakwama
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Ushuru si kwa wanyonge, wasokuwa na uwezo
Watozwe hata wabunge, na wengine wenye nazo
Yeyote asijitenge, kodi akalipa bezo
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Kwetu kutoa ushuru,ndiko kujitegemea
Pasiwepo na udhuru, usio wa kuelea
Huwa ni kama kiguru, asenao kutembea
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Maswali

(a) Tambua hadhira inayolengwa katika shairi hili. **(alama 1)**

b)Huku ukitoa mfano,onyesha mbinu **tatu** ambazo mshairi ametumia kutosheleza uhuru wake. **(alama 3)**

c)Bainisha aina **tatu** za urudiaji zinazojitokeza katika utungo huu. **(alama 3)**

d)Eleza muundo wa ubeti wa sita. **(alama 4)**

e)Andika ubeti wa **nne** katika lugha ya nathari/tutumbi **(alama 4)**

f)Kwa kutolea mfano,taja mbinu **tatu** za kimtindo zilizotumika katika shairi hili. **(alama 3)**

g)Weka shairi hili katika bahari yake ukirejelea : **(alama 2)**

i)Vipande

ii)Vina

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Sikilizeni wimbo huu:
Niliokuwa mtoto nilitwa chacha Kwa matamshi yangu ya sasa
Nilipokuwa mtu mzima niliitwa Manywele Nilipokuwa mwalimu nikaitwa Bure.

Huu utakuwa wimbo wako Utakapostaafu urudipo nyumbani Umelewa kangara na nyayo zako
Zikishindwa kulenga njia nyembamba vijijini. Utakuwa kichekesho cha watoto Watakaoukuita,
Ticha! Popote upitapo.

Kumbuka mwalimu utakapostaafu, Mijusi watataga mayai ndani ya viatu Vyako vilivyokwisha
visiginino.
Na ndani ya sidiria chakavu Zilizoshikizwa Kamba kwa pini
Mende watazaliana ndani ya chupa tupu Za marashi na za bia.

Na manyigu yatajenga ndani ya kofia Zilizosahaulika kutani
Utakapokufa nge watazaliana Chini ya jiwe juu ya kaburi lako, Na mlevi fulani akipita atapenga

Na kupangusa vidole kwenye jiwe pweke
Mwanzo na mwisho wako ndio huo.

Lakini wakati ungali hai
Unaweza kubadilisha mkondo wa maji Lakini kwanza mzungumze. Wewe na mimi. Acha mioyo yote izungumzwe
Baada ya kunyanyaswa Na kisha nusu mshahara.

Utafundisha tena nyimbo kuwasifu viongozi? Utafundisha tena ngonjera?
Utapeleka tena wanafunzi asubuhi Wakajipange barabarani kusubiri Mgeni afikaye saa kumi na apitapo
Apunga tu mkono kuwatia kichaa cha shangwe
Na huku nyuma mwasambaa na njaa?
Tazama hilo runda madaftari mezani Utalimaliza kwa mshahara mkia wa mbuzi? Tuzungumze. Ninyi na mimi.
Acha mioyo yetu izungumze
Mkiwa waoga na kujikunja kama jongoo Mtawekwa kwenye vijiti na kutupwa Nje ya ua, ndani mtawaacha
Wacheza ngoma wakitunga nyimbo mpya

Sikilizeni walimu,
Anzeni kufundisha hesabu mpya
Mjinga mmoja kujumlisha na wezi ishirini Ni sawa na sifuri. Hapana utawala Fundisheni historia historia mpya
Hapo zamani za sasa Hapakuwa na serikali.

Sikilizeni kwa makini Umoja hatuna
Twasambaratika kama nyumba Tulicho nacho ni woga,
Na kinachotuangusha ni unafiki. Lakini tusikate tamaa kama mbuni. Tukiupata umoja bado tunayo silaha. Kura.

Maswali

Fafanua sifa za shairi huru zinazojitokeza katika shairi hili. **(al. 5)**
Eleza jinsi maudhui ya utamaushi yanavyojitokeza ukimrejelea nafsi-nenewa**.** **(al. 4)**
Nafsi-nenewa anapaswa kujilaumu kwa masaibu yake. Thibitisha**.** **(al. 2)**
(i) Bainisha nafsi-neni katika shairi hil**i.** **(al. 1)**
Taja toni ya shairi hili. Toa mfano. **(al. 2)**
Eleza matumizi mawili mawili ya usambamba na jazanda katika shiri hili. **(al. 4)**
Eleza maana ya kufungu kifuatacho:
Mjinga mmoja kujumlisha na wezi ishirini ni sawa na sufuri. **(al. 2)**

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. **Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali**

1. Angole angole mwanangu
Mwanangu nakuchombeza
Nakuchombeza ulale
Ulale ukiamka
Nikupikie ubwabwa
Na mchuzi wa papa
Ukilia waniliza, wanikumbusha
Ukiwa wa baba na mama

2. Baba na mama watende
Ilimu kunikatizia
Ng'ombe, mbuzi kupokea
Kunioza dumu kongwe
Haliuki na halende
Kazi kupiga matonge

3. Likingia mvunguni
Lavunjavunja vikombe
Likilala kitandani
Languruma kama gombe

MASWALI

a) Bainisha kipera cha utungo huu. Thibitisha. **(alama 2)**
b) Eleza ujumbe unaofumbwa katika wimbo huu. **(alama 5)**
c) Tambua mbinu za kifani ambazo zimetumiwa kuwasilisha utungo huu. **(alama 3)**
d) Bainisha shughuli mojamoja ya kijamii na ya kiuchumi ambazo huendelezwa katika jamii ya utungo huu. **(alama 2)**
e) Unakusudia kukusanya data kuhusu kipera hiki. Eleza manufaa manne ya kutumia mahojiano. **(alama 4)**
f) Kipera hiki kinazidi kufifia katika jamii yako. Fafanua njia nne ambazo jamii ya kisasa inaweza kutumia kukuza na kuendeleza kipera hiki. **(alama 4)**

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA SITA)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1 (INSHA)

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

(a) *Andika jina lako na nambari ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(c) *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima.***
(d) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
(e) *Kila insha isipungue maneno **400**.*
(f) *Kila insha ina alama 20.*
(g) *Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
(h) *Insha zote **sharti** ziandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
	20	
JUMLA	40	

MASWALI

1. Wewe ni kiranja anayehusika na masomo katika Shule ya Angaza. Mwalimu mkuu amekuchagua wewe kuwa katibu wa jopo la watu watano. Mmetakiwa kuchunguza visababishi vya matokeo mabaya katika mitihani ya kitaifa kisha kutoa mapendekezo. Andaa ripoti yenu.

2. Jadili umuhimu wa sheria za shule kwa mwanafunzi.

3. Tunga kisa kitakachoafiki maana ya methali ifuatayo: Kidole kimoja hakivunji chawa.

4. Tunga kisa kitakachomalizikia kwa maneno yafuatayo: Hapo ndipo nilipotambua kuwa kama masuala yao hayatashughulikiwa kwa dhati, vijana ni bomu ambalo liko tayari kulipuka wakati wowote.

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA SITA)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2 (LUGHA)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

i. *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

ii. *Weka sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

iii. *Jibu maswali yote*

iv. *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*

v. *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

Kwa Matumizi Ya Mtahini Pekee:

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

1. UFAHAMU (Alama 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Ufisadi ni uhalifu unaohusu kuzitumia njia za ulaghai kujipatia pesa, mali au vitu hasa vya umma. Nchini Kenya ufisadi hujitokeza kwa njia mbalimbali na kila mojawapo ina athari zake. Kwa mfano, kuna maafisa wa serikali wajipatiao pesa kwa kuuza stakabadhi za serikali kama vile pasi, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kumiliki mashamba, vitambulisho na nyinginezo kwa raia. Kuna hatari kubwa kwa sababu watu wasio raia wa Kenya wameweza kusajiliwa kama Wakenya na kuendeleza uhalifu kama ugaidi, wizi na ulanguzi wa dawa za kulevya.

Wengine hujipatia vibali vya kufanya kazi na kuajiriwa kazi ambazo zingefanywa na Wakenya. Hii imechangia ongezeko la uhaba wa kazi nchini. Watumishi wengine wa umma huuza mali ya serikali kama vile magari, nyumba na ardhi na kufutika pesa za mauzo mifukoni mwao. Wengine wao hujinyakulia na kufanya vitu hivyo kuwa mali yao. Ufisadi wa aina hii umegharimu serikali kiasi kikubwa cha fedha. Serikali imelazimika kununulia maafisa wake magari baada ya muda mfupi, kulipia wafanyikazi wake kodi za nyumba na kukosa viwanja vya upanuzi na ujenzi wa shule, hospitali, vituo vya polisi na taasisi zingine maalumu.

Baadhi ya wataalamu kama madaktari huiba dawa kutoka hospitali za umma na kupeleka vituo vyao vya afya. Pia hutumia wakati wao mwingi katika kazi zao za kibinafsi na kuwaacha wagonjwa katika hospitali za umma wakihangaika. Sio madaktari tu, kuna masoroveya, wahandisi, mawakili, walimu na mahasibu ambao hukwepa majukumu yao serikalini na kufanya kazi za kibinafsi. Wengine wasio wataalamu huendesha biashara za aina tofauti, huku wanaendelea kupokea mishahara.

Wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo na shule bora za umma na hawakuhitimu wakati mwingine hulazimika kusalimu amri na kutoa hongo hili wapate nafasi za kusoma. Kiasi cha pesa kinachohitajika huwa kikubwa hivi kwamba ni wachache humudu hizo rushwa. Wale wasiojimudu kifedha hubaki wakilia ngoa. Kuna wazazi ambao hutumia vyeo vyao na 'undugu' kupata nafasi zilizotajwa, jambo ambalo huwanyima wanafunzi werevu kutoka jamii maskini nafasi ya kupata elimu. Matokeo huwa ni kuelimisha watu wasiostahili na ambao mwishowe hawaziwezi kazi wanazosomea wakihitimu na kuanza kuhudumia jamii.

Ufisadi umekita mizizi na kushamiri katika sekta za umma na za kibinafsi kwa upande wa kuajiri wafanyakazi. Ni vigumu kupata kazi ikiwa hujui mtu mkubwa katika shirika linalohusika au uzunguke mbuyu. Matokeo ni kuajiri wafanyakazi wasiohitimu na wasiowajibika kazini.

Vyeo na madaraka katika baadhi ya mashirika hutolewa kwa njia ya mapendeleo na ufisadi. Kwa hivyo, wafanyakazi wenye bidii hufa moyo kwa sababu hawasaidiwi ipasavyo. Badala yake wale wasio na bidii hupandishwa vyeo na kuwaacha palepale.

Hata hivyo, mbio za sakafuni huishia ukingoni. Serikali imetangaza vita dhidi ya ufisadi. Tayari tume kadhaa zimebuniwa kuchunguza visa vya ufisadi uliotekelezwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni Tume ya kuchunguza Kashfa ya "Goldenberg" ambapo pesa za umma ziliporwa na mashirika ya watu binafsi. Watakaopatikana na hatia ya kushiriki ufisadi huo watahitajika kurudisha pesa hizo. Serikali pia imeunda kamati ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi waliohasiriwa na mawakili walaghai ambao hupokea ridhaa kwa niaba ya wateja wao na kukosa kuwalipa au kuwatetea mahakamani ilhali wamekwishalipwa. Ni matumaini yetu kuwa ulaghai huu utaangamizwa kabisa kwani hakuna refu lisilokuwa na ncha.

Maswali

a) Eleza aina nne za ufisadi zilizotajwa katika kifungu ulichosoma. **(alama 4)**

b) Kulingana na kifungu ulichosoma,ufisadi umeathiri nchi yetu kwa njia gani ? (**alama 2)**

c) Serikali inafanya jitihada gani ili kukomesha ufisadi ? **(alama 3)**

d) Kwa maoni yako, unafikiri ufisadi husababishwa na nini **?** **(alama 3)**

e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kifunguni: **(alama 3)**

i) shamiri……..……

ii) waliohasiriwa……..……

iii) wakilia ngoa……..……

2. UFUPISHO (alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Katika siku za hivi karibuni, kumekuwa na malalamiko magazetini kuhusu tatizo Ia ajali za barabarani ambalo ni dhahiri kuwa sasa limekuwa donda sugu. Janga hili kubwa ni tishio sio tu kwa maisha na mali ya Wakenya bali pia kwa maendeleo ya uchumi wa taifa, hivyo linahitaji kutafutiwa ufumbuzi wa haraka. Ninaomba nitoe mapendekezo yangu kuhusu mikakati inayoweza kuchukuliwa ili kuepuka ama kukomesha matukio ya mara kwa mara ya ajali za barabarani.

Ongezeko Ia matukio ya ajali za barabarani zinazosababisha kuteketea kwa maisha, kwanza kabisa linatokana na uvunjaji wa sheria za usalama barabarani na ukosefu wa uangalifu miongoni mwa baadhi ya madereva. Hata hivyo, abiria nao wanachangia kusababisha ajali hizo. Inasikitisha kuona kuwa baadhi ya abiria wanakubali kupakizwa kupita kiasi kwenye magari mithili ya mapakacha ya machungwa kama kwamba wanalazimishwa kuyapanda kwa mtutu wa bunduki. Si ajabu vilevile kuona kuwa magari yanapopelekwa kwa mwendo wa kasi wa kupindukia, abiria wanakaa kimya kama kondoo wa kafara ama wanashangilia madereva hao. Ni ukweli usiopingika kuwa iwapo gari lililo katika kasi kubwa Iitakumbwa na hitilafu ni vigumu kwa dereva kulimudu na kulidhibiti gari hilo. Litakuwa ni jambo la busara iwapo magari yote ya abiria yatafungiwa vifaa vya kudhibiti kasi. Abiria na wananchi kwa jumla wana jukumu Ia kukemea na kuwakataza madereva wasiojali maisha ama kuwashitaki kwa vyombo vya dola. Aidha, ninapendekeza kuwa madereva wanaotiwa hatiani kwa makosa ya kuvunja sheria za usalama barabarani bila simile waadhibiwe vikali na ikibidi wapokonywe leseni zao.

Licha ya hayo, inapasa halmashauri inayohusika na utoaji wa leseni nchini, ihakikishe kuwa madereva wote wana leseni halali kwa mujibu wa sheria na kwamba siku zote utaratibu wa kusitoa leseni unazingatiwa kwa dhati. Mathalani, kabla ya kutolewa kwa leseni ihakikishwe kuwa kuna uthibitisho wa chuo cha udereva na hali kadhalika wa askari wa usalama barabarani kuhusu umahiri wa dereva anapoomba leseni. Kwa utaratibu kama huu hapana shaka kuwa vitendo vya kughushi leseni za bandia vitapungua na ajali zinazosababishwa na madereva wasio na ujuzi hazitakuwepo kabisa. Mkakati mwingine ni kutoa mafunzo ya uhakika kwa madereva. Aidha vyuo hivyo vinavyotoa mafunzo ya udereva viwe vinakaguliwa mara kwa mara na maofisa wa Baraza Ia Kitaifa Ia Usalama barabarani kwa lengo Ia kuhakikisha kuwa mtaala rasmi wa mafunzo unatumiwa.

Serikali kwa upande wake haina budi kutupia macho ukarabati wa barabara. Kwa hivi sasa,

barabara ziko katika hali ya kusikitisha. Ubovu wa barabara, udhaifu wa kingo za madaraja na ukosefu wa taa za kuongozea magari kwenye makutano ya barabara ni chanzo kinginecho cha ajali barabarani. Ni jukumu la Wizara ya Ujenzi kujenga utamaduni wa kukarabati miundo mbinu kwa kufanya matengenezo ya mara kwa mara ya barabara. Chambilecho wahenga, usipoziba ufa utajenga ukuta.

Hata ingawa hatua hizi ni njia madhubuti za kukabiliana na tatizo Ia ajali za barabarani, itakuwa ndoto kuzikomesha iwapo utekelezaji wa sheria za usalama barabarani utakuwa wa kutetereka. Sharti pawepo askari wa usalama barabarani iii kusaidia katika matumizi mazuri ya barabara, kuyakagua magari na leseni za madereva na vilevile kuwaffingulia mashtaka mahakamani wale wanaobainika kuzivunja sheria za usalama barabarani.

Tatizo la ajali za barabarani si jambo la kufumbia macho. Kinga ni bora kuliko tiba. Ninayo imani kuwa iwapo wananchi wataungana na serikali katika kuchukua hatua thabiti ili kupunguza ajali barabarani, maisha hayataendelea kuteketea ila yataokolewa.

Maswali

a) Ajali barabarani ni mwiba wa kujidunga. Thibitisha kwa kurejelea taarifa.
(maneno 40) **(Alama 6,1)**
Nakala Chafu
Majibu

b) Kwa maneno yako mwenyewe, bainisha mambo muhimu yanayozungumziwa kwenye aya ya **3, 4 na 5** **(maneno 90)** **(alama 7,1)** **Nakala chafu**
Majibu

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Tunga neno moja lenye konsonanti mbili ambazo hujulikana kama nusu irabu. **(al. 1)**

……

(b) Tunga sentensi ukitumia neno "kijana" kama ; **(al. 2)**

(i) Nomino ..……

(ii) Kivumishi ……

(c) Tunga neno lenye irabu zenye sifa zifuatazo**.** **(al. 2)**

(i) chini, kati, tandazwa……

(ii) nyuma, kati, viringwa……

(d) Andika sentensi yakinishi kutokana na hii. **(al. 1)**

Chakula hakipikiki vizuri

(e) Tumia vitenzi vifuatavyo vya silabi moja kutunga sentensi katika kauli ya kutendewa. **(al.2)**

(i)-ja……

(ii)-la ……

(f) Andika katika kinyume; Msichana yule mfupi ameingia darasani. **(alama 1)**

(g) Andika ukubwa wa sentensi hii katika wingi. **(al. 1)**

Kitabu kiliibwa na mwizi.

(h) Tunga sentensi kubainisha; **(al. 1)**

Chagizo cha mahali

(i) Andika kwa msemo halisi. **(al. 2)**

Mwanahamisi alisema kuwa angeenda Mombasa siku ambayo ingefuata.

(j) Akifisha sentensi hii ilete maana mbili tofauti. **(al. 2)**

Baba Maria anakuja.

(k) Changanua sentensi ifuatayo kwa jedwali. **(al. 4)**

Mtoto mjeuri ambaye alituzwa leo asubuhi amesafiri.

(l) Ainisha virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Watoto wa Juma wamegongwa na gari.

(m) Tunga sentensi moja kubainisha matumizi ya 'po' ya wakati maalum**.** **(al 1)**

(n) Eleza matumizi ya NI katika sentensi hii. **(al 1)**

Nitakulimia shamba lako ila hutanilipa.

(o) Unda nomino kutokana na kiarifa vifuatacho. **(al.1)**

Fa ..……

(p) Tunga sentensi inayodhihirisha wakati uliopita hali timilifu. **(al 1)**

(q). Ainisha mofimu katika neno **lililong'oleka** **(al.3)**

(r) Tunga sentensi ukitumia kisawe cha neno **tabibu**. **(al.1)**

(s) Tia shadda kwenye maneno haya; i. minyoo……ii. Mbuyu…**…….** **(al 1)**

(t) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao : **(al. 2)**

KN(W+V)+KT(t+N+H+N)

(u) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? **(al. 2)**

(i) uwele..……

(ii) petroli..……

(v) Mwanadamu yeyote anafaa kufanya juhudi wakati anapopewa msaada wa awali ili msaada huo ukifika mwisho ajiweze.Andika methali inayoafiki maelezo haya. **(al.1)**

..…… (w)

Tumia kishazi kitegemezi katika sentensi kama kiima**.** **(al.1)**

..…… (x)

Kwa kuzingatia dhamira, ainisha sentensi zifuatazo. **(al. 2)**

i. Meza tembe mbili mara tatu! ..…….

ii. Wanafunzi watasafiri leo jioni. ..……

(y) Ainisha silabi katika neno **Machweo.** **(al 2)**

4. ISIMUJAMII **(alama 10)**

a. Jadili jinsi mambo yafuatayo yanavyodhibiti mitindo ya lugha. **(al. 5)**

cheo cha mtu:…

Umri;…

Idadi ya lugha azijuazo mtu:…

Mada ….

Njia za mawasiliano: …

(b) Fafanua wajibu wa Kiswahili **kimataifa** **(al. 5)**

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA SITA)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3 (FASIHI)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(c) Jibu maswali manne pekee.
*(d) Swali la **kwanza** ni la lazima.*
(e) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki: yaani; Riwaya, Ushairi na Fasihi simulizi
(f) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
(g) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

Kwa matumizi ya mtahini pekee

SWALI	1	2	3	4	5	6	7	8	JUMLA
ALAMA									
UPEO	20	20	20	20	20	20	20	20	80

SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

1. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Mfalme ana watoto wawili wa kiume na anataka mmoja wao amrithi. Kwa sababu hataki kupendelea yeyote, anawapa changamoto ya kukimbia hadi mji wa mbali kwa farasi wao. Yule ambaye farasi wake atafika mwisho ndiye atakayemrithi. Ndugu hawa wanazembea jangwani kwa siku kadha kwa sababu kila mmoja anataka kufika wa mwisho. Hatimaye wanakutana na mzee mwenye busara ambaye anawapa wosia. Wanapanda farasi upesi na kutoka mbio ili wafike kwenye mji wa mbali walioagizwa na baba yao. Je, Mzee mwenye busara aliwaambia nini?

a) i) Tambua kijipera (**alama 1)**

ii) Taja sifa za kijipera hiki **(alama 4)**

iii) Wewe ni mmoja wanaowasilishiwa kipera hiki. Taja mambo Matano utakayoyafanya ufanikishe uwasilishaji huu**.** **(alama 5)**

b) Soma utungo ufuatao kisha hujibu maswali yanayofuata

Mtoto ni kito mzigo mzito

i) Tambua kijitanzu **(alama 1)**

ii) Eleza manufaa ya kukirithisha kijitanzu hiki kwa vizazi vijavyo **(alama 4)**

iii) Kipera hiki kinaendelea kudidimia katika jamii yako eleza mbinu tano utakazotumia kukidmisha katika jamii yako**.** **(alama 5)**

SEHEMU B :Tamthilia – BEMBEA YA MAISHA - *Timothy* Arege

Jibu swali la 2 au 3.

2. Maisha ya sasa hayana fundi. Yanamwendesha kila mtu kama tawi lililosukumwa hadi likang'oka kutoka taagani na kupeperushwa na upepo….Ulimwengu wa sasa haubagui. Wadogo kwa wakubwa…..

a) Eleza mkutadha wa nukuu **(alama 4)**

b) Changanua vipengele vitano vya kimtindo katika nukuu **(alama 5)**

c) Fafanua mbinu nne za kutambua hulka za **mneneji** **(alama 4)**

d) 'Maisha ya sasa hayana fundi.' Fafanua mbinu ishi wanazotumia wahusika tamthiliani kukabiliana na hali zao. **(alama 7)**

3. (a) Changanua mtindo katika kifungu kifuatacho. **(alama 4)**

Naam, bembea! Hata bembea ikiwa ya kamba au chuma hatimaye hulika. Wanasema papo kwa papo kamba hukata jiwe. Bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa mchezo. Huungwa na mchezo kuanza tena.

(b) Eleza toni katika dondoo hili. **(alama 2)**

(c)Jadili umuhimu wa mandhari katika tamthilia hii **(alama 6)**

(d) (i) Fafanua kinaya katika kauli iliyopigiwa mstari (**alama 1)**

(ii) Dhihirisha kinaya katika kauli iliyopigiwa mstari kwa kurejelea tamthilia (**alama 7)**

SEHEMU YA C: RIWAYA – Clara Momanyi *Nguu za Jadi*.

Jibu swali la 4 au 5.

4. Fafanua jinsi Mbwashu anajenga maudhui ya ufisadi. **(aL20)**

5. *"Daima mtu yule hunichukiza."*

a. Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(al.4)**

b. Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kujenga maudhuiriwayani. **(al.12)**

c. Eleza sifa nne za mtu anayerejelewa **(al.4)**

SEHEMU D : USHAIRI

Jibu swali la 6 au la 7

6. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yafuatayo;

Wangu niliyekupenda, leo nitakufukuza
Kuishi umenishinda, waniletea mayaza
Ola vile nimekonda, jasadi nimepooza
Uwache kuniumiza,ni heri mwana kunenda

Ulikuwa wangu nyonda, huba nikaikoleza
Kukupenda kama tunda, embe lenye uliwaza
Ukajigeuza punda, teke umenicharaza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Nimekonda kama ngonda, mwandani wanilemaza
Sautiyo ya kinanda, sitaki kusikiliza
Sikutaki bora kwenda, muhibu wanishangaza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Mengi ulionitenda, si madogo yakupuza
Nalikupa kila gwanda, uvae na kupendeza
Ulikula na kuwanda, kadiri ulivyoweza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda.

Kinyume ulipokwenda, nilidhani kuteleza
Na wewe hukujilinda, nyendo mbaya kupunguza
Cha kuvunda kisha vunda, hata ukikifukiza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Mja wewe wanishinda, kwa tama wachukiza
Kila kitu unadanda, kingawa cha kuumiza
Huwi ndani ya kibanda, huishi kujitembeza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

MASWALI

a) Tambua na uthibitishe nafsi neni katika shairi **(alama 2)**
b) Fafanua umuhimu wa kipokeo cha shairi hili **(alama 1)**
c) Eleza sifa za kiarudhi katika ubeti wa **tatu** **(alama 4)**
d) Taja methali inayodokezwa katika ubeti wa **tano** wa shairi hili **(alama 1)**
e) Eleza maudhui ya ubeti wa **sita** wa shairi hili. **(alama 2)**
f) Ni jambo lipi zuri ambalo mshairi atalikosa? **(alama 1)**
g) Andika ubeti wa **pili** wa shairi hili katika lugha nathari **(alama 4)**
h) Fafanua mbinu alizotumia mshairi kutimiza mahitaji ya kiarudhi **(alama 2)**
i) Tambua aina tatu za urudiaji katika shairi **(alama 3)**

7. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Pana haja ya kupima, neno tuzowele -angu
Tusizowee kusema, hili ni teuo langu
Huenda huji mapema, -angu huja kuwa tungu
Ikaja kukusakama, na kukuposha kwa Mungu
Pana haja ya kupima.

Neno huwa ni la kwako, likiwa ndani moyoni
Lakini katu si lako, likishavuka menoni
Kwa hivyo likutokako, liweke kwenye mizani
Linaweza kuwa cheko, ama tusi kwa wendani
Pana haja ya kupima.

Vivyo hivyo kwa lebasi, huwa yako kisutuni
Hivyo nina wasiwasi, wambe yako sebuleni
Itavutiya matusi, ya wenzio insani
Wakakuchoma nafusi, kwa mishale ya lisani
Pana haja ya kupima.

Mwana ujuwe ni wako, punje ukiimezele
Lakini katu si wako, nde ukimletele
Akiwa yu ndani yako, ni wa duniya vivile
Ukishishila ni wako, muavye tukakuole
Pana haja ya kupima.

Maisha nayo si yako, utabaradi milele
Ungayaishi ja yako, ni tunu ya maumbile
Mgawa si kufu yako, mshindane hili lile
Akupapo akupako, utaishi pale pale
Pana haja ya kupima.

Ni chetu, chako si chako, ulimwengu huwa vile
Juhudi zingawa zako, wa kufaidi ni wale
Ikifika siku yako, nyono zikukae mbele
Ulichosema ni chako, huwabakiya wawale
Pana haja ya kupima.

Kaseme na moyo wako, ubaini haya yale
Ukuambacho ni chako, kisikupe mageule
Kitu utajacho chako, huenda kiwe cha wale
Na usemacho si chako, kiwe chako ndicho kile
Pana haja ya kupima.

(Maanga ya Ushairi na Diwani ya Mjileo* - Henry Indindi*)

Maswali

(a) Pendekeza anwani inayoafiki shairi hili. **(al 1)**
(b) Eleza dhamira ya shairi. **(al 2)**
(c) Fafanua maudhui yoyote matatu yanayojitokeza katika shairi. **(al 3)**
(d) Ainisha mkondo wa shairi hili. **(al 4)**
(e) Tambua nafsi nenewa katika shairi. **(al 1)**
(f) Toa toni ya shairi. **(al 1)**
(g) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya kiriwaya. **(al 4)**
(h) Dhihirisha mtunzi huyu alivyofanikiwa kutumia uhuru wake. **(al 2)**
(i) Toa maana za maneno haya yalivyotumiwa katika shairi. **(al 2)**
(i) lebasi
(ii) punje ukiimezele

SEHEMU E : Hadithi Fupi – Mapambazuko ya Machweo

8. ***(a) Mzimu wa kipwerere-Yussuf Shoka***

"Siku iliyofuata, majira ya magharibi pevu, nilifika pale mzimuni. Kama ilivyo ada yangu, nilivaa guo jeupe lililonifunika gubigubi kama maiti. nikaangalia huku na huko, sikuona mtu. Hapo nikasogea karibu zaidi na ule mzimu. Nilipofika nikauimba ule wimbo wote. Nilipomaliza tu nikajitoma kichakani mle bila hofu wala kimeme…nilichokiona humo, sikuamini macho yangu! Mle ndani ya mzimu mlikuwa na makanda na makasha ya tumbaku, unga wa kilevi na bangi kwenye marobota. Kulikuwa na mapipa ya chang'aa na tembo ya mnazi. Humo pia, mlikuwa na kitanda cha besera kilichotandikwa vizuri. Juu ya kitanda hicho, palitupiwatupiwa asumini na maua ya mlangilangi.."

a)Eleza aina nne za taswira katika kifungu hiki**.** **(al 4)**

b)Ukirejelea hadithi ya*" **Mzimu wa Kipwerere**,"* Fafanua jinsi imani katika mambo ya kichawi yamejikita katika jamii**.** **(al 6)**

(b)**Mapambazuko ya Machweo** – Clara Momanyi

Onyesha vile **Jua la Macheo** linawabishia wahusika mbalimbali katika **Machweo** yao **(al 10)**

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA SABA)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1 (INSHA)

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Andika insha **mbili**. Insha ya **kwanza** ni ya **lazima.***

b) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*

c) *Kila insha isipungue maneno **400.***

d) *Kila insha ina alama **20.***

e) *Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. Mauaji katika ndoa yamekita mizizi katika taifa letu. Umeteuliwa na rais wa jamuhuri kuwa katibu wa Tume ya Uwiano wa Kijamii kuchunguza sababu za mauaji haya na hatua za kukabiliana na janga hili. Andika Ripoti. **Alama 20**

2. Kama mwanafunzi bora katika shule yako umepata nafasi ya kuzuru kwenye mbuga la wanyama la Masai Mara kwa siku tano ambapo umejifundisha mengi kuhusu umuhimu wa kuhifadhi misitu katika mfumo ikolojia. Andika shajara. **Alama 20**

3. Tunga kisa kitakachodhihirisah ukweli wa methali:
Asiyemjua simba atazame mtegowe. **alama 20**

4. Nilipoipokea simu nilisikia: "Njoo upesi kwenye kituo cha afya cha Kamaliza kuna dharura…" Endeleza. **Alama 20**

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA SABA)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2 (LUGHA)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

c) *Jibu maswali **yote**.*

d) *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

e) *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

UFAHAMU

Somo kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Muhula wa kwanza wa kidato cha tatu ulipoanza, kama ilivyokuwa desturi katika shule ya Askofu Timotheo, wanafunzi walichunguzwa hali na Sista. Sista akaandika nakala ya matokeo ya uchunguzi wake na kumkabidhi mwalimu mkuu wa shule Bi. Margaret. Mwalimu mkuu akafanya lililomjuzu**.** Akaandikia waraka wazazi kwa wasichana waliuokuwa katika nakala ya matokeo ya Sista.

Jumatatu ya juma la tatu ilianza kama siku nyinginezo. Wanafunzi walijumuika gwarideni. .Maombi ya asubuhi yalifanywa. Mwalimu wa zamu akawakumbusha wanafunzi majukumu yao na bendera ikapandishwa. Zamu ya mkuu wa shule ilitimia. Aliwakumbusha wanafunzi umuhimu wakuwajibikia vitendo vyao. Baada ya hilo, aliita majina ya wanafunzi watatu na akatangaza kwamba baada yakufumukana wafike ofisini mwake. Vicheko vya chini kwa chini vilianguliwa. Sababu ya kuitwa kwa wanafunzi wale ilikuwa dhahiri.

Sela na wenzake walipofika ofisini walielekezwa wasubiri katika chumba cha mapokezi. Ingawa walifahamu sababu ya kuitwa pale, mpango uliokuwapo ulikuwa usiku wa giza. Hakuna aliyezungumza na mwenziwe kutokana na muemeo wa mawazo. Wote waliinamisha nyuso zao.

Baada ya nusu saa hivi, ofisini mliigia wazazi wawili; wa kike na kiume. Walikuwa wazazi wa Sela ; Mzee Butali na mkewe. Wao walionekana kuemewa na fikira. Kutokana na urasmi wa muktadha ule, hapakuwa na mazungumzo baada ya salamu. Mara kwa mara, Mzee Butali alitupia bintiye jicho la uhasama kabla ya mhazili kumfahamisha mwalimu mkuu kuhusu mjo wa wazazi wale.

Ofisini, Bi. Margaret ***alitia udibaji*** , " Asanteni kwa kuja. Sisi kama walimu na wazazi hukabiliana na mengi. Tukio lililowaleta hapa ni la kawaida kwetu. Ingawa sisi hufanya tuwezavyo kuwalinda wanetu, mara nyingi tabia zao hutupiga chenga…"

Wakati huu wote wazazi wa Sela walikuwa wamenyamaza. Mamake Sela alikuwa akimtazama Bi. Margaret huku Mzee Butali akiwa ameinama. Bi. Margaret alipohitimisha usemi wake, Mzee Butali aliinua uso wake na kumtazama mwalimu mkuu.

"Mwalimu nina swali moja ambalo ningetaka unijibu. Je, ni kwa nini sisi huwaleta watoto shuleni?" mzee Butali aliuliza kwa sauti iliyojaa uchungu.

Baada ya mazungumzo kati ya mwalimu mkuu na wazazi wa Sela, uamuzi ulitolewa. Sela na wenzake wawili hawangeweza kusoma pamoja na wengine baada ya hali yao kubainika. Bi. Margaret alipendekeza watafutiwe shule za kutwa karibu na watokako ili waendelee kusoma huku wazazi wakiwatunza. Alikuwa amewaandikia barua za mapendekezo ili wapokelewe katika shule ambazo wangechagua. Sela aliondoka shuleni na wazazi wake.

Boma la Mzee Butali liligeuka jahanamu baada ya kutoka shuleni. Mzee Butali aliwazulia ***majojo*** Sela na mama yake. Majirani nao walishuhudia bughudha hizo kwa mbali.

" Leo ndio mtanitambua. Mama gani anayemtaza mwana akigeuka afriti? Sikutumia hela zangu mimi katika elimu yake hadi nikaitwa pangu pakavu? Mtwae kilicho chenu mniondokee!" mzee Butali aliwafokea Sela na mama yake.

"Baba Sela, nani kasema huu ni msiba wangu? Tutautwaa pamoja. Huyu ni mtoto wetu, sio maradhi. Tutaondoka ndio; lakini elewa uchungu wa mwana ajuaye ni mzazi." Mama yake Sela alitoa kauli yake.

Maswali

(a) Shule ya Askofu Timotheo imejengwa katika msingi wa kidini. Fafanua. **(alama 2)**

(b) ".. sisi hufanya tuwezavyo kuwalinda wanetu,.." Kulingana na kifungu eleza jinsi wazazi na walimu wanavyolinda wana wao**.** **(alama 4)**

(c) Mwalimu mkuu alisisitiza kuhusu umuhimu wa kuwajibikia kwa wanafunzi katika vitendo vyao. Taja matokeo tatu ya kutowajibika kwa Sela. **(alama 3)**

(d) Kwa kutolea sifa mbili, eleza hulka ya Mzee Batili. **(alama 2)**

(e) Taja mtindo uliotumika katika kauli hii: Boma la Mzee Butali liligeuka jahanamu… **(alama 1)**

(f) Eleza maana ya: **(alama 2)**

(i) alitia udibaji

(ii) majojo

(g) Kipe kifungu hiki anwani mwafaka**.** **(alama 1)**

UFUPISHO

Hapana shaka yeyote kuwa, ujio wa teknolojia nchini ulibadilisha ufumo wa kimaisha uliokuwepo hapo awali. Binafsi, ni miongoni mwa kizazi kilichozaliwa na kulelewa wakati hakukuwa na teknolojia yoyote katika jamii. Pengine teknolojia kubwa iliyokuwepo nyakati hizo ni redio na saa. Njia kuu ya mawasiliano ilikuwa uandishi wa barua.

Shirika la Posta Kenya lilikuwa na umuhimu mkubwa sana, kwani idadi kubwa ya wananchi ambao hawangemudu gharama ya kupiga simu za serikali walikuwa wakilazimika kuandika barua kuwatumia wapendwa wao. Si wengi walimudu kutumia simu hizo, kwani nyingi zilikuwa katika maeneo ya mijini. Kwa hivyo ili kutumia ingemlazimu mtu aliye katika maeneo ya mashambani kutenga siku fulani kusafiri hadi mjini ili kuitumia simu fulani.

Hata hivyo, mwanzoni wa 2000, hali ya mawasiliano ilianza kubadilika nchini kutokana na ujio wa simu za rununu. Wale walimudu kununua simu hizo walionekana kama matajiri . Lilikuwa jambo la kipekee kumwona mtu akiwasiliana kwa kutumia kisanduku kidogo kilicho bonyezwabonyezwa vidude kwa vidole . Miaka ilivyosonga, mawasiliano yaliendelea kurahisika .Bei za simu zikashuka pakubwa . Miundo ya simu pia iliimarika, kiasi kwamba kwa sasa,ni vigumu kumwona mtu yoyote bila simu hata watoto. Kwa sasa ,mtu yeyote anayemiliki simu isiyo na intaneti huonekana kama"aliyebaki nyuma".

Si intaneti tu, simu za sasa ni kama ofisi ndogo. Kando na intaneti,zina huduma nyingi ambazo hupatikana katika saibakefu,kwani ndiko kuna tarakilishi zilizounganishwa na intaneti. Sababu ya urejeleo ni kuonyesha jinsi teknolojia na mawasiliano yalivyo badili katika jamii. Kilicho wazi ni kuwa ,ujio wa simu za kisasa umerahisisha sana mawasiliano na jinsi tunavyopata habari kuhusu matukio tofauti duniani kwa muda mfupi. Licha ya manufaa hayo yote,kuna tatizo kubwa kuhusu simu hizo: uwepo wa baadhi ya apu na mitandao ya kijamii.

Ukweli ni kuwa baadhi ya apu zilizo katika simu hizo zinatishia kuvuruga maadili katika jamii. Kwa mfano, muundo wa apu ya Tiktok humruhushu mtu kurekodi video na kuiweka mtandaoni. Hilo

huwapa nafasi maelfu ya watu kutazama video husika na kuifurahia. Wengine hueleza hisia zao kuhusu video husika.

Hata hivyo kile kinachohitajika ni kuhakikisha kuwa sawa na mitandao mingine ya kijamii kama vile Facebook , Instagram, Twitter au Whatsapp, kanuni na masharti ya kuutumia yanafuatiliwa kuhakikisha uzingatiaji ili usivuruge mustakabali wa kimaadili kwa kizazi cha sasa na vile vijavyo.

(a) Kwa **maneno 80** fupisha aya tatu za kwanza. **(alama 8)**

matayarisho

jibu

(b) Fupisha ujumbe wa aya tatu za mwisho kwa **maneno 70.** **(alama 7)**

Matayarisho

jibu

MATUMIZI YA LUGHA **(ALAMA 40)**

(a) Andika neno lenye sauti zifuatazo **(alama 1)**

(i)Kipasuo-kwamizo sighuna cha kaakaa gumu,irabu ya juu,nyuma,irabu ya juu,nyuma ,kikwaruzo ghuna cha masine,irabu ya chini,kati tandaze

(ii)Dondoa sauti mwambatano katika maneno yafuatayo na uainishe mahali pa kutamkia. **(alama 1)**

Tamba

Afya **(iii)**Linganua irabu katika neno;**mavue.** **(alama 1)**

(b)(i) Onyesha muundo wa silabi kwenye kiima katika sentensi ifuatayo. **(alama 1)**

Mwalimu aliwasili kwa gari ili awasilishe ripoti ya wanahabari.

(ii) Eleza tofauti kati ya sauti mwambatano na silabi mwambatano.Thibitisha kwa mfano. (**alama 2)**

(c)Weka shadda panapofaa katika maneno yafuatayo. **(alama 1)**

(i)katakata (kugawa vipande.)……

(ii)katakata (kabisa kabisa)…….

(d)Bainisha dhamira inayoibuliwa na sentensi ifuatayo. **(alama 1)**

(i)Ombeni bila kusita.

(e)Andika maneno yenye miundo ifuatayo. **(alama 1)**

(i)Mofimu ya nafsi ya tatu wingi,hali timilifu ,mzizi,kauli ya kutendwa,kauli ya kutenda(kiishio).

(f)Kwa kutunga sentensi,tumia 'a'unganifu kuonyesha dhana zifuatazo; **(alama 2)**

(i)uhusiano wa cheo/kazi

(ii)uhusiano wa wakati

(g)Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo.

(i)Wachezaji huenda wanaweza kushinda mchezo wa leo. **(alama 2)**

(Bila kutumia vitenzi visaidizi)

(ii) Mwalimu huwaadhibu wanafunzi wapotovu.Mwalimu huwarekebisha wengi. **(alama 2)**

(unganisha kuwa sentensi changamano;Anza kwa kiunganishi)

(iii) Maandalizi yalifanywa kwa wakati ufaao.Wanajeshi walishinda vita hivyo. **(alama 2)**

(Tumia 'ki' ya masharti kuunda sentensi moja)

(iv) Michuano itaanza juma lijalo.Wakufunzi wanaendelea kuwatia makali wachezaji. **(alama 2)**

(Unganisha kuwa sentensi moja inayoanza kwa: Wakufunzi…)

(h) Tunga sententensi ukitumia aina zifuatazo za maneno. **(alama 2)**

(i)nomino ambatano

(ii)nomino ya kitenzijina

(i)Tunga sentensi ukitumia kivumishi cha pekee cha nyongeza **(alama 1)**

(j) Tunga sentensi ukitumia shina -w-kama ; **(alama 2)**

(i)kitenzi kisaidizi

(ii)kitenzi kishirikishi

(k)(i)Eleza dhana ngeli. **(alama 1)**

(l)Tunga sentensi kwa kutumia nomino zifuatazo na ubainishe upatanisho wa kisarufi. **(alama 1)**

(i)simanzi

(ii)wino

(m)Andika sentensi ifuatayayo katika hali ya ukubwa wingi; **(alama 2)**

Mama huyo aliicheza tarumbeta kwa vidole na midomo .

(n)Kwa kutolea mifano bainisha miundo miwili ya ngeli ya KI-VI. **(alama 2)**

(o) Pambanua sentensi ifuatayo kwa mishale, **(alama 3)**

Bwalo ambalo lilisakafiwa litafunguliwa mwakani.

(p)Iandike upya sentensi ifuatayo ukianza kwa shamirisho kipozi. **(alama 1)**

Alila aliwakatakatia mifugo wale nyasi kwa upanga.

(q)Eleza dhana chagizo. **(alama 1)**

(r)Tunga sentensi yenye muundo ufuatao; **(alama 1)**

KN(Ø)+KT(T)

(s)Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Hawa ni watoto wa marehemu Bwana Nzovu na Bi.Makambo.

(t)Tunga sentensi moja kutofautisha sahibu na shaibu. **(alama 1)**

(u) Taja visawe viwili vya ,kata kamba , **(alama 1)**

ISIMU JAMII

Wewe ni chifu wa kata la Mawindoni. Umealikwa kuhutubia wanakijiji kuhusu swala la usalama.

Fafanua mtindo wa lugha utakayotumia**.** **(alama 10)**

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA SABA)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
c) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
d) *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima*****.**
e) *Maswali hayo mengine* ***matatu*** *yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; Riwaya, Ushairi, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.*
f) ***Usijibu*** *maswali mawili kutoka sehemu moja.*
g) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
JUMLA	80	

SEHEMU YA A: *Mapambazuko Ya Machweo Na Hadithi Nyingine- Clara Momanyi*

SWALI LA LAZIMA

1. "Mike! Mike! Mike! Njoo! Nilijua utafanya vyema mwanangu…"

(a) Tambua na ueleze **toni** ya dondoo hili. **(alama 2)**

(b) Changanua mtindo katika dondoo hili**.** **(alama 2)**

(c) Eleza sifa **nne** za msemaji wa dondoo hili. **(alama 4)**

(d) Eleza mbinu **mbili** ulizozitumia kutambua sifa za msemaji wa dondoo hili. **(alama 4)**

(e) Tambua na ufafanue madhila yanayomsakama mhusika mkuu katika hadithi hii ya *"Sabina".* **(alama 8)**

SEHEMU YA B: RIWAYA

Nguu za Jadi-Clara Momanyi

Jibu swali la 2 au 3

2. Fafanua nafasi ya mhusika Sihaba katika kujenga maudhui riwayani. **(aL20)**

3. *"Nawe ulimkataa na kuolewa na mtu aliyemfahamu na kumdharau sana"*

d. Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(aL4)**

e. Tambua sifa za msemewa wa maneno haya kwa kurejelea dondoo hili **(aL4)**

f. Kwa kurejelea riwaya nzima, jadili jinsi msemewa amepigana kuikomboa jamiiyake **(aL12)**

SEHEMU YA C: TAMTHILIA

Bembea ya Maisha- Timothy Arege

Jibu swali la 4 au 5

4."…anachukua vidonge vyake na kuvimeza kabla ya kuketi kwenye kochi mpya."

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama 4)**

(b) Tambua aina za taswira katika dondoo hili. **(alama 2)**

(c) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. **(alama 4)**

(d) Eleza nafasi ya mwanamke ukijikita katika utamaduni wa jamii ya *"Bembea ya Maisha".* **(alama 10)**

AU

5. " Wakati mwingine maisha haya hukufanya kijisikia kama abiria kwenye gari liendalo kwa kasi. Unatamani dereva apunguze mwendo lakini unakumbuka kuwa safari bado ni ndefu na hutaki kufika ukiwa umechelewa. Basi unatulia japo ndani una wasiwasi, hutulii. Lakini huwezi kushuka maana safari itaganda. Kwa hivyo, unajitahidi tena, japo wakati mwingine unajikuta umetambaliwa na uchovu, shaka na tuhuma."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

(b) Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama4)**

(c) Dhihirisha umuhimu wa mzungumziwa wa maneno haya katika kuijenga tamthilia ya *"Bembea ya Maisha*". **(alama 6)**

(d) Eleza namna maisha yanamfanya mzungumzaji "kujisikia kama abiria kwenye gari liendalo kwa kasi". **(alama 6)**

SEHEMU YA D: USHAIRI

Jibu swali la 6 au 7

6. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Jama, Jama, Jamani
Mbona twabebeshwa mateso hivi
Mizigo mikubwa ya dhiki kama
Kwamba hatuna haki ya kusema
Kukataa ndoa za lazima
Kukataa kuozwa wazee
Kukataa kukatishwa masomo
Kukataa tohara ya lazima

Jama, Jama Jamani
Iweje tuteswe mateso haya
Na watu wasio kuwa hata na haya kama
Kwamba hatuna haki ya kulalamika
Kulalamikia kutumikishwa kama mayaya
Kulalamikia kudhalilishwa kiunyama
Kulalamikia kutolindwa na sheria

Jama, Jama, Jamani
Sasa hii ni awamu nyingine
Na macho tumeyafungua kabisa
Tumekataa kudhalilishwa kabisa
Tumekataa kuteswa kama watumwa
Tumekataa tohara ya lazima
Tumekataa kuozwa..... Tumekataa! Tumekataa
Hii awamu ya 'Haki ya mtoto wa kike'

<u>Maswali</u>

(a) Taja mambo **matatu** muhimu yaliyozungumziwa na mshairi kisha ueleze kila moja . **(alama 6)**

(b) Eleza muundo wa shairi hili **(alama 4)**

(c) Taja mbinu **mbili** za lugha alizotumia mshairi kisha ueleze kila moja **(alama 4)**

(d) Kwa nini mshairi huyu anasema hii ni 'awamu' nyingine? **(alama 3)**

(e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa na mshairi **(alama 3)**

(i) awamu

(ii) kudhalilishwa

(iii) Dhiki

AU

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo

1. Mkata ni mkatika, harithi hatoridhiwa
Sina ninalolishika, wala ninalochukuwa
Mlimwengu kanipoka, hata tone la muruwa!
Mrithi nini wanangu?

2. Sina ngo'mbe sina mbuzi, sina konde sina buwa
Sina hata makaazi, mupasayo kuyajuwa
Sina mazuri makuzi, jinsi nilivyoachwa
Mrithi nini wanangu?

3. Sina kazi sina bazi, ila wingi wa shakawa
Sina chembe ya majazi, mno nikukamuliwa
Nakwa'cheni upagazi, ngumu kwenu ku'tuwa
Mrithi nini wanangu?

4. Sina sikuachi jina, mkata hatasifiwa
Hata nifanye la mana, mno mi kulaumiwa
Poleni wangu sana, sana kwenu cha kutowa
Mrithi nini wanangu?

5. Sina leo sina jana, sina kesho kutwaliwa
Sina zizi sina shina, wala tawi kuchipuwa
Sina wanangu mi sina , sana la kuacha kuraduwa
Mrithi nini wanangu?

6. Sina utu sina haki, mila yangu meuliwa
Nyuma yangu ili dhiki, na mbele imekaliwa
N'nawana na miliki, hadi nitakapofukiwa
Mrithi nini wanangu?

7. Sina ila kesho kwenu, wenyewe kuiongowa
Muwane kwa nyinyi mbinu, mwende pasi kupumuwa
Leo siyo kesho yenu, kama mutajikamuwa
Mrithi nini wananngu?

(a) Taja mambo yoyote **mawili** ambayo mtunzi angewarithisha wanawe. **(alama 2)**
(b) Eleza sababu ya mtunzi kutoweza kuwarithisha wanawe. **(alama 3)**
(c) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. **(alama 4)**
(d) Dondoa mifano **miwili miwili** ya : **(alama 2)**
(i) Inkisari
(ii) Tabdila
(e) Chambua shairi hili kwa upande wa :

(i) Dhamira **(alama2)**

(ii) Muundo **(alama 4)**

(f) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumiwa katika shairi. **(alama 3)**

(i) Mlimwengu kanipoka

(ii) Sina konde sina buwa.

(iii) Wingi wa shakawa.

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.

Malaika
Nakupenda malaika x2
Ningekuoa malaika...
Ningekuoa dada...
Nashindwa na mali sina wee...

Ningekuoa malaika x2

Pesa, zasumbua roho yangu x2
Nami niafanyeje, kijana mwenzio
Nashindwa na mali sina wee...

Ningekuoa malaika x2

MASWALI

(a) Ainisha wimbo huu kwa kuzingatia kipengele cha maudhui**.** **(alama 2)**

(b) Andika sifa **mbili** za jamii inayosawiriwa na wimbo huu. **(alama 2)**

(c) Eleza mikakati **sita** ambayo mwimbaji angetumia kufanikisha uwasilishaji wa wimbo huu. **(alama 6)**

(d) Unanuia kutumia mahojiano kukusanya habari kuhusu nyimbo za aina hii.

(i) Eleza manufaa **matano** ya kutumia mbinu hii. **(alama 5)**

(ii) Eleza changamoto **tano** za kutumia mbinu hii**.** **(alama 5)**

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA NANE)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1

INSHA

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Andika insha **mbili**. Insha ya **kwanza** ni ya **lazima.***

c) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*

d) *Kila insha isipungue maneno **400***

e) *Kila insha ina alama **20***

f) *Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. Lazima

Wewe ni mwenyekiti wa vuguvugu la Tazama Afrika. Andika mazungumzo yako na mawaziri wawili kutoka mataifa yaliyoendelea barani kujadili matatizo yanayokumba bara la Afrika.

2. Uhuru unaopewa vijana leo katika nchi yetu una madhara zaidi kuliko faida.Jadili.

3. Maji ukiyavulia nguo, yaoge.

4. … Nilijitoa kafara na msaada wangu ukazaa natija kwa wengi.

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA NANE)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

a) *Jibu maswali* ***yote.***

b) *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kitabu hiki cha maswali.*

c) *Majibu yote* ***lazima*** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

d) *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa na kuwa* ***maswali yote yamo.***

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

1. UFAHAMU (Alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Mengi yamesemwa kuhusu utiifu. Ukweli ni kuwa,watu wengi hudhani kuwa maisha yangekuwa mazuri zaidi ikiwa kila mtu angeruhusiwa kufanya atakavyo. Kulingana na mimi, ni makosa kufikiria hivyo madhali mienendo isiyodhibitiwa na sheria ni kiini cha vurugu na ukiukaji wa sheria nchini. Hebu fikiria hali ingekuwa vipi ikiwa mwendeshaji pikipiki angeiendesha kulia na kushoto katikati ya barabara na kupuuza sheria za trafiki. Hali kama hii huweza kusababisha msongamano mkubwa wa magari mjini, hivyo kuwafanya watu wachukue muda mrefu kabla ya kufika waelekeapo. Kutengenea au shwari kwa mambo hutokana na kila mtu kufuata kanuni zote zilizowekwa.

Kila mtu hana budi kuelewa kuwa utiifu si udhaifu au woga. Ni hali ya kutambua kuwa kutii utawala wa kisheria huhakikisha kuwa kuna muumano na utangamano wa kijamii. Utiifu una maana ya kufanya yanayotarajiwa. Vilevile utiifu una maana ya kutambua na kukubali kuwa kufanya matendo mema ni bora zaidi kuliko kutekeleza jambo au matendo ya kibinafsi tu. Kwa hakika, ni vyema kutafakari kuhusu tunayoambiwa tufanye na wenzetu au hata watu wengine. Hatufai kufuata kila maagizo tunayopewa bila kuyatathmini vizuri. Mathalan; ikiwa mtu atakuambia ujihusishe na ujambazi, unafaa kuwajibika kwa kukataa kufuata amri ya aina hiyo hata kama mtu huyo ana mamlaka makubwa namna gani. Maagizo au kanuni tunazofaa kufuata au kutii ni zile zenye maana;yaani, maagizo au kanuni zenye manufaa.

Je, kwa nini watu wengi huona vigumu kuwatii walimu, wazazi au watu wenye mamlaka? Sababu kuu ni kuwa wao ni wabinafsi. Wao huchochewa na kufanya kutotii kutokana na lengo la kutenda mambo yatakayowafaidi; yale mambo yatakayowasaidia kutimiza matakwa yao ya kibinafsi. Kiini cha mioyo ya watu kama hawa kukaidi maagizo na kanuni maishani, hutokana na ukweli kuwa utiifu humlazimu mtu kupuuzilia mbali matakwa ya kibinafsi na mara nyingi hujumuisha kutekeleza anayoambiwa afanye na wengine.Hata hivyo,ikiwa watu kama hawa watazingatia manufaa ya utiifu, watatamani kupalilia utiifu kama mojawapo wa maadili maishani mwa binadamu.

Ukweli ni kuwa katika maisha ya kila siku, tunatii kanuni nyingi bila kufahamu au kujua. Hakuna mtu,kwa mfano, anayetulazimisha kuzingatia lishe bora au kufuata maagizo ya daktari. Wengi wetu huhudhuria shule au kwenda kazini kwa wakati unaofaa bila kushurutishwa. Ikiwa kwa mfano una gari unalomiliki, hakuna anayekuarifu kulipeleka kwenye gereji likatengenezwe au likarabatiwe. Hebu jiulize hapo ulipo; je, kwa nini watu hufanya mambo kama haya bila kuagizwa au kukahiriwa?Ukweli ni kuwa,tendo lolote lile la kutotii au kutotekeleza yanayohitajika litakuwa na matokeo mabaya au hata ya kuhatarisha maisha ya watu. Kwa hivyo, utiifu huleta utangamano na humfanya mtu kuishi bila mfadhaiko wowote.

Kiini cha vijana kukosa kukubali na kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa hutokana na ukweli kuwa, wao huziona kama zilizopitwa na wakati. Ni ukweli kuwa si mambo yote wanayotuhimiza wenzetu kufanya yana mantiki. Hata hivyo, ni muhimu kuzingatia **matilaba** ya kuyatenda badala ya kuyapuuza. Zaidi ya hayo, tunaosema kuwa wana mawazo yaliyopitwa na wakati wanaweza kuwa

na **tajriba pevu** na umaizi au utambuzi mkubwa wa mambo kutuzidi. Vijana wengi wanaokaidi maagizo ya wazazi wao huteseka maishani. Inafaa ieleweke kuwa hata kama wazazi na walimu wanaweza kuonekana wakali na wasiozingatia kila tutakalo, daima wao hututakia mazuri na huwa na malengo mema kuhusu maisha yetu.

Baadhi ya matatizo ya kijamii, kiuchumi na hata kisiasa tunayopitia au kukumbana nayo hutokana na kutotii sheria. Hali ya kutotii sheria au hata kanuni zilizowekwa huwafanya baadhi ya watu hukataa kulipa ushuru, wengine kubadhiri au kuhariji mali ya umma au kujihusisha na vitendo vya kifisadi; hali ambayo huinyima nchi yetu mapato au maduhuli. Vitendo kama hivi huifanya nchi kurudi nyuma kimaendeleo. Kutotii sheria husababisha madhara mengi kwa mtu binafsi; watu wengi huharibu maisha yao kwa kupiga mtindi kupindukia, kuvuta sigara au hata kasumba na kujihusisha na mapenzi kiholela. Ukweli ni kuwa wao hujua hatari itokanayo na mienendo kama hiyo. Kabla ya kuvunja sheria au kupuuza kanuni zozote zile ni muhimu kufikiria kuhusu matokeo yake kwanza. Aidha ni vyema kugundua kuwa hakuna mtu yeyote yule anayeweza kuepuka athari za uasi.

Maswali

a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. **(alama 1)**

b) Je, ni kwa nini watu hawawezi kuruhusiwa kufanya watakavyo? **(alama 2)**

c) Eleza maana ya utiifu kwa mujibu wa taarifa hii. **(alama 2)**

d) Eleza sababu inayowafanya watu kuasi. **(alama 1)**

e) Kwa nini tunafaa kusikiliza wanayotuambia wazazi na walimu wetu hata kama hatukubaliani nayo **(alama 2)**

f) Eleza manufaa matatu ya utiifu. **(alama 3)**

g) Fafanua matokeo mawili ya uasi kulingana na taarifa hii. **(alama 2)**

h) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika taarifa**:** **(alama 2)**

(i) matilaba

(ii) Tajriba pevu

2. UFUPISHO (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali uliyoulizwa.

Suala la uzito wa mwili ni mojawapo wa masuala ambayo yamewashughulisha wataalamu katika miaka ya karibuni.Tatizo hasa sio uzito wa mwili wenyewe bali ni uto ambao aghalabu unaenda sambamba na uzito huo. Uzito wa mwili ni kipimo cha mwili mzima ukihusishwa na misuli ya mwili. Zipo njia mbali mbali zinazoweza kuchangia uzito wa mwili.Kimsingi, hutokana na kalori za ziada ambazo mwili huo huwa nazo. Kalori hizi hutokana na hamirojo , mafuta au hata proteini.Kalori hizi huhifadhiwa na mwili katika seli maalum (tishu za mafuta). Asilimia 50 ya

jumla ya mafuta au uto wa mwili huhifadhiwa chini ya ngozi ya mwili. Ile nyingine huzunguka viungo mbalimbali vya mwili kama vile moyo.

Uto una faida kadha mwilini.Kwanza,ni msingi muhimu na mkuu wa nishati za mwili. Uto unapochomwa na mwili huvyaza oksijeni ya ziada ambayo husambazwa kwenye seli za mwilini.Oksijeni hii inapoungana na atomu za kaboni na haidrojeni huwa chanzo cha joto mwilini.Uto pia hukinga mifupa na viungo vya mwili,huhifadhi au kuukinga mwili hasa dhidi ya baridi na huwa nyenzo muhimu hasa kwa mwenye matendo ambayo yanahitaji matumizi ya nguvu.Licha ya faida zake hizi,uto huwa na matatizo.Kimsingi, uto mwingi unaweza kuwa chanzo cha unene au utipwatipwa wa mwili ambao unaweza kuwa chanzo cha fedheha kutokana na unene.Uto pia unahusishwa na hali kadha za kimatibabu kama kufupisha uwezekano wa maisha kuwa marefu.Yapo maradhi ambayo yanahusishwa kwa kiasi kikubwa
na unene wa mwili,unaotokana na uto ,kama maradhi ya moyo,bolisukari,ugonjwa wa ini na matatizo ya figo.

Vyanzo vya tatizo la uto hutofautiana.Wataalamu wanaamini zipo chembechembe zinazorithiwa ambazo huweza kuwa chanzo cha ulaji unaopiku ambao unaweza kusababisha unene. Hata hivyo, ingawa msimbojeni unaweza kuwa chanzo hiki,ulaji usiozingatia hatari kama hizi huchangia pakubwa. Vipo baadhi ya vyakula ambavyo vina mchango mkubwa katika kulivyaza tatizo la unene.Vyakula hivi ni vile vinavyojulikana kama vyakula chapwa vikiwemo kaukau na viazi vya kutafuna.Aidha, vinywaji huweza kuwa vyanzo vya kalori ambazo huishia kuwa chanzo cha uto mwingi mwilini.Ili kupambana na tatizo la unene, pana haja ya kuhakikisha kuwa tunapunguza ulaji wa baadhi ya vyakula.Hivi ni vyakula vyenye mafuta mengi.Kwa mfano,mtu wa wastani anaweza kukung'uta kalori 300 kwa saa afanyapo mazoezi.Mazoezi haya husaidia viungo vingine vya mwili kama vile moyo kwa kiasi kikubwa.

Hizi ni njia nyepesi ambazo zinaweza kutumika kupunguzia uzito kuliko matumizi ya madawa au njia nyingine za kihazigi ambazo huweza kuwa na matokeo hasi kwa mwili.

Maswali

a) Fupisha ujumbe wa aya ya kwanza kwa maneno 50 (Alama 5;1 ya mtiririko)

Matayarisho

Jibu

b) Eleza masuala ambayo mwandishi ameibua katika aya ya pili kwa maneno 50.

(Alama 7;1 ya mtiririko)

Matayarisho

Jibu

c) Fupisha ujumbe wa aya ya tatu kwa maneno **40** **(Alama 3)**

Matayarisho

Jibu

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Andika sauti zenye sifa zifuatazo: **(alama2)**

(i) kipasuo **sighuna/hafifu** cha ufizi

(ii) irabu ya mbele juu

(b) Neno 'kwapa ' liko katika **ngel**i gani? **(alama 1)**

(c) Tofauitisha sentensi zifuatazo **kimaana** **(alama 2)**

(i) yote yameliwa .

(ii) yoyote yameliwa.

(d) Andika neno moja lenye **mofimu** zifuatazo: **(alama 3)**

Nafsi ya pili wingi , hali timilifu ,yambwa,mzizi, kauli tendea, kiishio

e) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya **ukubwa wingi** **(alama 2)**

Ng'ombe huyo alinunuliwa mbali na mji ule mkuu.

(f) **Ka** imetumika kuleta maana gani katika sentensi zifuatazo : **(alama 2)**

(i) Rais kazuru mbuga za wanyama

(ii) Mgeni kaingia humu ndani kupumzika.

i) **Kirai** ni nini? **(alama 1)**

(ii) Bainisha **aina** za virai vilivyopigiwa mstari**.** **(alama2)**

Yule mzembe alipigwa na mwanawe.

(h) Tofautisha maana ya **jozi** ifuatayo ya maneno. **(alama 2)**

i. ridhi ……

ii. rithi…….....

(i) Eleza matumizi yoyote mawili ya alama ya **kistari kirefu** katika sarufi ya Kiswahili**.(Alama 2**

(j) Ainisha **vihusishi** katika sentensi: **(Alama 2)**

i) Hawa watatumia pesa nyingi kushinda wale.

ii) Darasa nzima litatuzwa na mwalimu wao.

(k) **Sahihisha** sentensi zifuatazo . (**alama 2)**

i) Kile kitabu kilipasuka ni changu .

ii) Mtu mwenye ameanguka ni ndugu yangu.

(l) Nyambua vitenzi hivi katika kauli ya **kutendesha**, kisha uvitungie sentensi . **(alama 2)**

i) oa…….

ii) la……

(m) Mkunga ni mtu mwenye maarifa ya kushugulikia wanawake wajawazito wakati wa kujifungua . Tunga sentensi mbili zitakazodhihirisha maana nyingine mbili za neno hili. **(alama 2)**

(n) Kwa kutungia sentensi, dhihirisha matumizi ya '**kwa**' ili kuonyesha : **(alama 2)**

i) sababu / nia

ii) Jinsi ya kutenda/kitendo kilivyofanywa

o) Changanua sentensi hii kwa kielelezo cha **matawi.** **(alama 4)**

Muumini atakayeshtaki ni msaliti mkubwa sana.

(p) Bainisha shamirisho kitondo katika sentensi :

Lola alimpasulia nyanya kuni**.** **(alama 1)**

(q) Tumia viashiria vya **kutilia mkazo** katika sentensi zifuatazo: **(alama 2)**

c) Wema----------ulisababisha atuzwe.

ii) Polisi waliwafuata ---------- walikoenda.

(r) Andika **kitenzi** kinachotokana na neno : **(alama 1)**

mfuasi

(s) Eleza **tofauti** baina ya sentensi hizi: **(alama 2)**

i) Ningekuwa na pesa ningenunua pikipiki.

ii) Ningelikuwa na pesa ningelinunua pikipiki.

(t)Andika **methali** inayoafiki maelezo yafuatayo: **(alama 1)**

Mwanadamu hakosi ila. Aliyekamilika ni Mungu pekee.

4 ISIMUJAMII **(Alama 10)**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Jumamosi ,Disemba 26,2020

Ananyoa kwa shoka

Na Wangu kanuvi

Julius Mwangi, 24, ni kinyozi ambaye amevuma kwa kunyoa wateja wake. Kinyozi huyu aliamua kuanza kutumia shoka miezi mitatu iliyopita baada ya kutambua kuwa ipo haja ya kuwa na njia ya pekee ya kuwanyoa watu.

"Nimebobea katika kutumia mashine lakini nilitaka njia mbadala na ya kipekee ya kuwanyoa watu…"

Wateja wake hujaa kibao katika kibanda chake kilicho katika mtaa wa Tayari, kaunti ya kiambu…

a) Bainisha sajili ya makala haya. **(Alama 2)**

(b) Eleza sifa zozote **sita** za sajili hii kwa kurejelea makala haya. **(alama 6)**

(c) Fafanua sifa nyingine **mbili** za sajili hii ambazo zingejitokeza katika makala haya. **(alama2)**

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA NANE)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3 (FASIHI)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… **SAHIHI**……

NAMBARI YA USAJILI…… **MKONDO**……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Jibu maswali manne pekee.*
b) *Swali la kwanza ni la lazima.*
c) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; tamthilia, riwaya, hadithi fupi na fasihi simulizi.*
d) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
e) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
f) *Andika nambari ya maswali uliyoyajibu.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
	20	
	20	
	20	
	20	
JUMLA	80	

SEHEMU YA A: USHAIRI

MBELE YA SAFARI

1. Ilipoanza safari , ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

2. Njaa ikawa dhabiti ,na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti ,dhila na mingi mikiki
Tukajizatiti

3. Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari,utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari , juhudi iliyobaki
Tukajizatiti

4. Ile ilikuwa ndoto , mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto,sahala 'mekuwa dhiki
Wagombanio kipato,utashi haukatiki
Nakutabakari

5. Msafara ukasita , kwenye mlima wa haki
Kijasho kinatuita , mlima haupandiki
Basi sote 'kijipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina

6. Tukiwa migongo wazi ,tukainama kwa shaki
Tukawa'chia ukwezi , kialeni wadiriki
Wakapanda bila kazi ,Kuteremsha miliki
Wakaitapia

7. Wakafikia makazi,ya pumbao na ashiki
Huko wakajibirizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma ulomiliki
Mbele ya safari

8. Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema , kwa umati halaiki
Imezima nia yote ,kiza hakitakasiki
Mbele ya safari

a) Eleza safari inayolejelewa katika shairi hili. **(al 2)**
b) Onyesha kinaya cha safari inayozungumziwa. **(al 6)**
c) Taja na ueleze bahari mbili za shairi ukizingatia : **(al 4)**
i. Mizani ;
ii. Vina
d) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari**.** **(al 4)**
e) Eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa sita. **(al 4)**
f) Eleza umbo/ muundo wa shairi hili. **(ala 2)**

SEHEMU YA B: TAMTHILIA

Timothy Arege

BEMBEA YA MAISHA

2. Hiyo ndio ajabu! Kizazi hili hakitaki kufanya kazi. Kinataka kuja kazini kwa sababu ya mshahara tu. Wachapa kazi hodari ni njozi iliyopotea.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(ala 4)**

b) Eleza sifa za msemaji wa dondoo hili. **(ala 4)**

c) Fafanua imuhimu wa msemewa katika kazi ya Bembea ya Maisha. **(ala 4)**

d) Taja na uonyeshe mbinu za uandishi zilizotumika katika dondoo. **(ala 4)**

e) Eleza maudhui yanayokuzwa katika muktadha wa dondoo. **(ala 4)**

3. Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(ala 20)**

SEHEMU YA C: Riwaya
Clara Momanyi;Riwaya ya Nguu za Jadi
Jibu swali la 4 au 5

4. Fafanua jinsi Mrima amechangla kuibomoa jamii yake **(al.20)**

5.*"Hamwoni kwamba mila hainiruhusu mie nikatunzwe na mke kama mgonjwa? Aummesahau mikatale ya utamaduni kwa sababu mnaishi mjini"*

a. Fafanua muktadha ya dondoo hili **(al 4)**
b. Tambua mbinu mbili za lugha katflca dondoo hili_ **(al.4)**
c. Tambua maudhui katika dondoo hili_ **(al.8)**
d. Fafanua umuhimu wa mandhari ya dondoo hill **(al.4)**

HADITHI FUPI

D.W Lutomia na Phibbian Muthama: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

Jibu swali la 6 au la 7

6. "Isije ikawa mwenye nyumba kuja na yeye mpangaji akachelewa kumfungulia mlango; itakuwa balaa bin beluwa"

i. Eleza muktadha wa dondoo **hili** **(ala 4)**

ii. Jadili umuhimu wa mwenye nyumba anayerejelea **(ala 6)**

iii. Maisha yalikuwa balaa bin beluwa kwa mpangaji. Thibitisha **(ala 10)**

7.

(a) Machoka alikumbuka kauli ya jirani yake, Zuhura, aliyeishi kumkumbusha, "wetu ni wetu, hata akiwa mbaya … wetu. Hatuna budi ila kumchagua yeye. Lisilobudi hubidi. Awe amesoma ama hajasoma, angali wetu."leo hii hata Zuhura mwenyewe alikuwa anajutia kumchagua huyo wetu.

Kwa muda mrefu, Machoka na Zuhura walikuwa kama fahali wawili hawakai katika zizi moja. Kisa na maana, ni wafuasi wa watu wawili tofauti. Leo hii kinachowaleta pamoja Machoka na Zuhura ni udhikinifu, hali ngumu ya maisha, mfumuko wa bei za bidhaa muhimu na kutozwa ushuru wa kiwango cha juu na serikali hiyo hiyo ya 'watu wao'. Zuhura alisuta nafsi yake. Alikuwa akiitazamia nchi nzuri na maisha bora baada ya uchaguzi. Alitazamia 'watu wake' wangezitimiza ahadi walizozitoa wakati wa kampeni zao. Leo hii imebakia kujuta. Kujuta ghya ya kujuta! Tayari alikuwa amekwishafanya kosa. Kosa ambalo alifahamu lilikuwa la kujitakia. Ulikuwa mwiba wa kujidunga usiokuwa na kilio wala kuambiwa pole. Maji yalikuwa yashamwagika, katu hayangeweza kuzoleka…"

Chambua maudhui katika dondoo hili**.** **(ala 12)**

(b) Eleza sababu nne zinazochangia jimbo la Matopeni kutoshuhudia maendeleo ya kisiasa tangu nchi kupata uhuru . **(ala 8)**

SEHEMU YA E

FASIHI SIMULIZI

8. i)Eleza maana ya misimu. **(al 2)**

ii)Taja mambo manne ya kimsingi yanayochangia kuchipuka kwa msimu. **(al 4)**

iii)Eleza umuhimu wa misimu katika jamii. **(al 10**

iv)Taja sifa nne za misimu. **(al 4)**

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA TISA)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1 (INSHA)

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) Andika insha mbili
*b) Swali la kwanza ni la **LAZIMA***
c) Kila insha isipungue maneno 400
d) Chagua insha nyingine moja kutoka kwa hizo tatu zilizosalia
e) Kila insha iandikwe kwa lugha ya Kiswahili
h) Majibu yote yawe katika kijitabu hiki

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	ALAMA
1	
JUMLA	

MASWALI

1. LAZIMA

Wewe ni katibu wa jopokazi lililoteuliwa kuchunguza vyanzo vya ongezeko la umaskini nchini.

Andika ripoti ya uchunguzi huo huku ukitoa mapedekezo **(alama20)**

2. Unywaji wa pombe haramu umekithiri miongoni mwa vijana shuleni. Wewe kama kiranja wa ushauri nasaha, waandikie ilani kuhusu madhara ya pombe haramu **(alama20)**

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali; Achanikaye kwenye mpini hafi njaa

(alama20)

4. Tunga kisa kitakachoanza kwa maneno yafuatayo;

Majeruhi walifikishwa hospitalini mmoja baada ya mwingine wakiwa katika hali mahututi. Sauti nzito ya daktari mkuu ilihanikiza hewani baada ya **……** **(alama20)**

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO KUPIGWA CHAPA!

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA TISA)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2 (LUGHA)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Andika jina lako na nambari ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*

b) Tia sahihi yako na kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu

c) Jibu maswali yote

d) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali

e) Majibu yote ni lazima yaandikwe kwa lugha ya kiswahili

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
Ufahamu	15	
Ufupisho	15	
Matumizi ya lugha	40	
Isimu jamii	10	
Jumla	80	

UFAHAMU

Soma makala haya ujibu maswali yafuatayo

Utotoni niliamini kwamba kusoma ndiko ufunguo wa kila kitu ulimwenguni kwa jinsi kunavyoonekana kuwatoa watu katika uzuzu, ukata na ugonjwa: na kuweka kwenye maisha bora ya mwangaza wa kujua kusoma na kuandika, utajiri wa kuweza kuvaa hata suti ya vipande vitatu, na kuwa na afya ya kuonekana kwa kitambi. Hizo ni zamani zile ambapo shule ya vidudu haikuwa sharti la mtoto kukubaliwa katika darasa la kwanza. Mtoto angelisha ama kusaidia kwa kazi za nyumbani mpaka kufika umri wa miaka kumi kisha, kufumba na kufumbua, afisa wa serikali angeonekana akishauriana na wazazi wa mtoto. Matokeo yangekua mtoto huyo kuanza safari ndefu ya kila siku, apate asipate chakula.

Mimi kwa upande wangu sikujali maisha pata-nenda shule, kosa-bado-neda-shule. Sikujali kero za baridi kali wala karaha za vua la asubuhi. Kuanzia utotoni *niliwahusudu* wenzangu waliokuwa wakirauka kiasi cha kufikiriwa walilala kwa shati na kaptula zao, au kwa blauzi na skati na kaptula zao. Nilipendezwa na unifomu zao nikatamani na hata kuapa kwamba siku moja nitavaa kama wao na kutembea kwa maringo kama wao. Zaidi nilitamani kufika walikokuwa wakienda na kufanya walivyokuwa wakifanya huko.

Penye nia hapakosi njia. Nia yangu ilidhihirika nilipojiunga na darasa la kwanza. Darasa la kwanza lilinisoma kisogo baada ya siku mbili tu. Nalo la pili likanipungia mkono baada ya juma moja. Miaka mitano baadae nilikutana na kiunzi cha kwanza kwenye mtihani wa kitaifa wa chumba cha saba uliokuwa kifungua mlango wa kuingia kidato cha kwanza.

Baada ya miaka minne nilikutana na mlango funge mwingine nilibisha na ukanifungukia kwa *kutia fora* katika mtihani wa kiwango cha elimu ya pili. Katika miaka miwili iliyofuatia nilijiunga na shule maarufu ya kitaifa siku hizo.

Masomo hayakuendelea kuwa mteremko kwangu kwani uchechefu wa karo na masurufu ulimaanisha kuwa siku nyingi nilikuwa nje ya kuta za darasa letu. Hata hivyo *nilijifunga masombo*. Hatimaye nilifunguliwa mlango wa kuingia ndaki.

Baada ya kuhitimu kwa shahada ya kimsingi ya uzamili, kisha uzamifu au daktari falsafa hatimaye, nilifanywa meneja kufikia leo. Hata nikiwa ukubwani bado nazidi kusoma na kutafiti ili nisiote ukurutu wa akili.

Cheo na madaraka haya ya umeneja yamaanisha kila siku nivae suti kamili na shati nyeupe pe, amabayo shingoni imeambatanishwa na kipande maalumu cha kitambaa kinacholewalewa kifuani. Nijiangaliapo kiooni hujifananisha na mtu ambaye amejitia jitanzi shingoni.

Nina kitambi ambacho labda ni *taashira* ya utajiri. Hata hivyo ingawa mimi si mwenye sauti kubwa kiuchumi, ninaweza kujivunia elimu yangu ilivyoniwezwsha kujimudu kidogo maishani. Sasa nina shamba langu mwenyewe, nyumba yangu mwenyewe ambayo imejaa mali yangu mwenyewe. Nina redio yangu mwenyewe, rununu yangu mwenyewe na wanyama wangu mwenyewe.

Lakini mwenzangu ambaye zilimwishia ukingoni katika shule za nasari, hana elimu, pesa wala mahali pa kuzikiwa wakati mpira utakapomwia mwingi.

MASWALI

a) Eleza imani ya mwandishi kuhusu elimu **(alama3)**

b) Taja dhiki zilizomkabili mwandishi alipokuwa shuleni **(alama2)**

c) Onyesha uhusiano uliopo kati ya elimu, kazi na ukwasi kwa mujibu wa habari hii **(alama3)**

d) **Ukirejelea** makala haya, fafanua msemo,'elimu ni bahari haina kikomo' **(alama3)**

e) Hatima ya wale ambao hawakupata elimu ni ipi? **(alama2)**

f) Badala ya maneno yafuatayo mwandishi angetumia msamiati gani? **(alama3)**

i) Nilijifunga masombo

ii) Ndaki

iii) Taashira

UFUPISHO (Alama 15)

Dhuluma kwa wanawake sio matokeo ya sasa baada ya uhuru, bali ni matokeo ya hali iliyokuepo tangu enzi za mababu zetu; kabla ya ukoloni. Kubaguliwa na kudhulumiwa kwa wanawake kiasi kunaoana na kunyonywa kwake kijamii kunakoshuhudiwa siku nenda miaka rudi.

Elimu ya jadi ilimwandaa mwanamke kuwa chombo kitiifu cha mwanamume. Mwanamke aliandaliwa katika unyago na katika mfumo mzima wa malezi kuwa chombo cha kutumikia mwanamume-kumstarehesha, kumfariji, kumlisha na kumzalia watoto. Mwanamke tangu jadi hakuruhusiwa kushiriki katika shughuli za kisiasa na utawala wala hakuna mtu aliyeamini kwamba mwanamke angeweza kushikilia wadhifa wowote wa uongozi.

Demokrasia ya jadi naihusudu sana; ambapo wazee walikaa chini ya mbuyu na kuamua mambo ya jumuiya. Mahakama ya kijiji ilikuwa aghalabu ni ya wazee na wanaume peke yao. Hakukuwa na mwaname aliyeshirikishwa, hata kama alikua ajuza. Sifa waliokua nayo wanawake ni ile ya usihiri na uganga. Mwanamke yeyote aliyezeeka alidhaniwa kuwa bingwa wa uchawi, ulozi na ushirikina. Kwa hivyo, wanawake ndio waliokuwa washirikina wakubwa, maana fursa ya kupata elimu pana zaidi hawakuwa nayo. Si ajabu kuwa mwanamke alipojitokeza na kusema jambo la busara, aliuupza na pengine kutukanwa hadharani.

Kwa bahati nzuri, kumezuka mwamko uliotuingiza katika enzi mpya. Vita vya wanawake vya kujihami na kujiendeleza katika ulimwengu unaotawaliwa na wanaume vimetapakaa kote katika kila sehemu ya dunia. Wanawake wengi wamekiuka misingi na mizizi ya utamduni na kung'oa asasi za kijamii na itikadi ambazo daima zimeendelea kumnyanyasa na kumuumbua utu mwanamke tangu jadi. Watetezi wa haki za wanawake zamani walilaumu suala la serikali za mataifa mwaka hadi mwaka. Huku maswala ya wanawake ya kijamii, uut na utamaduni yakishangiliwa kupitishwa, watetezi wameeleza wasiwasi wao ikiwa kupitishwa kwa maazimio kutasaidia kuleta maendeleo ya haraka kwa wanawake kimataifa au katika nchi moja. Fauka ya hayo, baadhi ya wachunguzi wanaonelea kuwa maazimio mengi hayadokezi hatua za kufikiwa haki za wanawake.

Maazimio mengine yanazungumzia juu ya kuondolewa kwa ubaguzi dhidi ya wanawake, kushiriki kwao katika uendelezaji wa amani ya kimataifa, na ushirikiano wa kimataifa, majukumu yao katika jamii, mfuko wa umoja wa Mataifa wa wanaweka (Unifem) na kuimarisha hadhi ya

wanawake katika sekretariati ya Umoja wa Mataifa miongoni mwa shughuli nyingine katika mkabala huu.

Wanawake wameonyesha vipaji vyao katika nyanja mbalimbali za maisha; siasa, uchumi, utawala na kadhalika. Wanawake wamejikakamua na kudhihirisha kuwa wao pia wana jukumu muhimu la kutekeleza ili kuyaongoza maisha yao na ya watu wengi. Wadumishaji wa dhuluma za kijinsia hawana budi kusalimu amri na kuukubali ukweli huu, wapende wasipende. Mtazamo juu ya haki sawa unatokana na kukubaliwa na kuondolewa kwa aina zote za ubaya dhidi ya wanawake wanaojitolea mhanga kutetea hadhi yao pamoja na ya wanyonge wengine. Wao huonekana kama waasi, wapinga mila na watovu wa utii.

MASWALI

a) Bila kubadilisha maana asilia, fupisha aya tatu za kwanza.(Maneno 45-55) **(alama6)**

Matayarisho

Jibu

b) Kwa kurejelea aya tatu za mwisho, pambanua hoja muhimu zinazoguziwa na mwandishi (Maneno 60-65) **(alama9)**

Matayarisho

Jibu

MATUMIZI YA LUGHA

a) Andika maneno yenye vitamkwa vya sifa zifuatazo **(alama2)**

Kikwamizo sighuna cha kaakaa gumu, irabu ya nyuma juu, kikwamizo ghuna cha kaakaa laini, irabu ya nyuma juu, kitambaza na irabu ya mbele juu.

ii) Taja sifa zinazonyesha usawa baina ya jozi hizi

/gh/ na /ng'/

/f/ na /v/

b) Andika neno lenye muundo ufuatao wa tamko kamili katika neno **(alama2)**

K,KI,KKI

KiK

c) Ainisha mofimu katika neno hili **(alama2)**

Kifurahieni

d) Tunga sentensi ukitumia nomino uga (wingi) pamoja na kivumishi cha pekee cha kusisitiza na kielezi cha kiasi **(alama2)**

e) Andika katika hali ya ukubwa **(alama2)**

Wanawake wale wana midomo mikubwa inayotisha

f) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo **(alama4)**

Mwanafunzi aliadhibiwa kwa kuwa alikosea mwalimu (badilisha maneno yaliyopigwa msitari kuwa nomino)

ii) Mapambano baina ya mwanadamu na mazingira yalizaa fasihi (anza kwa fasihi)

iii) Margret ni mkakamavu. Onyi ni mkakamavu pia. (unganisha iwe sentensi moja yenye kihusushi cha kulinganisha)

iv) Maji ambayo wanakunywa ni hatari (tumia hali ya mazoea bila 'amba')

g) Tunga sentensi ukitumia kishazi tegemezi kinachofanya kazi ya kiwakilishi **(alama2)**

h) Andika wingi hali katavu **(alama2)**

Nyanya na babu : Sisi ndisi wakulima

i) Andika sentensi moja kwa wakati uliopita hali endelevu ukitumia kitenzi – P - katika kauli ya kutendana **(alama2)**

j) Tumia kijalizo katika sentensi kama: **(alama2)**

i) kiwakilishi

ii) kielezi

k) Tunga sentensi moja kutofautisha maneno haya: taka na daka **(alama2)**

l) Andika kinyume **(alama2)**

Mjomba hakumtwika nyanyake mzigo hivyo akapata laana

m)Onyesha kiima, chagizo na aina za shamirisho **(alama2)**

Mpodozi ambaye alikuja juzi alipaka kucha rangi jana jioni mara kadha wa kadha

n) Eleza matumizi ya 'KU' katika sentensi hii **(alama2)**

Alikusaidia kwenda kule wakati hukuwa na uwezo wa kusoma

o) Changanua sentensi hii ukitumia kielelezo cha msitari **(alama2)**

Hasikii la mwadhini wala mtekaji msikitini

p) Bainisha maana mbili zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Mwakuona angefuata somo angefaulu

q) Eleza matumizi mawili ya alama ya kibainshi **(alama1)**

r) Tunga mfano mmoja wa sentensi kuzingatia muundo ufuatao **(alama2)**

S - (RH + RH + t + N + V)

s) Neema amekuwa kiduchu toka utotoni lakini mwenye akili nyingi akitazama unaona kama anayezisoma a akili zako (tumia methali mwafaka kuafiki maelezo hayo) **(alama1)**

t) **Jaza** pengo **(alama2)**

i) Mtu ni kwa mja, ukongo ni kwa ..... na kiate ni kwa .....

ii) Tunapotaka kuomba radhi kabla ya kutamka jambo ambalo linaweza kumuudhi mtu tunasema ..... ilhali tunapotamka kuonyesha mshtuko au jambo la hatari tunasema .....

ISIMU JAMII(alama10)

Jambo Kenya! Nachukua fursa hii kumkaribisha mheshimiwa Profesa Chan kutoka jamhuri ya watu wa Uchina. Kufikia hapo kila kitu ki barabara tunapoendelea kujadiliana kuhusu swala hili la mabadiliko ya hali ya anga ulimwenguni. Suala hili linaendelea kupunguza idadi ya watu duniani. Nawaomba tusimame kuwaheshimu walioondoka.

(anawaashiria wasimame)

Asanteni sana!

a(i) Tambua sajili hii **(alama1)**

ii) Eleza sifa za sajili uliotaja hapo juu ukizingatia kifungu **(alama4)**

b) Order! Lazima kutii mpangilio! Katili hauruhusiwi kuongea bila ruhusa. Polisi, mpelekeni nje.

i) Tambua sajili hii **(alama1)**

ii) Fafanua sifa zozote nne ambazo zingejitokeza iwapo mazungumzo yangeendelea**(alama4)**

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA TISA)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3 (FASIHI)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
b) Jibu maswali manne pekee
c) Swali la kwanza ni la lazima
d) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobakia yaani : Riwaya, hadithi fupi,ushairi na fasihi simulizi
e) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
f) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
g) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
USHAIRI	20	
TAMTHILIA	20	
RIWAYA	20	
HADITHI FUPI	20	
FASIHI SIMULIZI	20	
JUMLA		

SEHEMU A: TAMTHILIA

Timothy M.Arege :Bembea ya Maisha

1. **LAZIMA**

La! Kila mbegu ipandwayo haina budi kuzaa na izaapo mazao yake huvunwa. Mtu hutakasa sahani akijua itamfaa tena. Kinacholelewa hakina budi kulea.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**

b) Changanua mtindo katika dondoo hili **(alama3)**

c) Kauli iliyopigiwa mstari inaonyesha majukumu ya watoto kwa wazazi. Thibitisha kwa kuonyesha wazi alivyowajibika anayerejelewa na msemaji **(alama4)**

d) Fafanua umuhimu wa msemaji katika kujenga tamthilia ya Bembea ya Maisha **(alama4)**

e) Eleza sifa tano za msemewa **(alama5)**

SEHEMU B: RIWAYA

Clara Momanyi: Nguu za Jadi

Jibu swali la 2 au 3

2. "Tangu lini mke amuulize mumewe kule aendako au atokako?.....Ama kweli, wanawake wa kisasa wanavunja kila mwiko uliowekwa na wazee."

i) Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. **(alama4)**

ii) Kwa kutoa mfano,**taja mbinu ya lugha** iliyotumika**.** **(alama2)**

iii) Eleza **umuhimu wa msemaji** **(alama4)**

(iv) Kwa kutoa mifano **kumi** kutoka riwayani, fafanua jinsi **mwanamke amesawiriwa** katika jamii ya Matuo. **(alama 10)**

3. Jamii ya Matuo katika riwaya ya 'Nguu za Jadi' imekumbwa na **usaliti** si haba. Kwa kutoa mifano mwafaka riwayani, onyesha ukweli wa kauli hii. **(alama20**)

SEHEMU C:HADITHI FUPI

MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE

Jibu swali la 4 au la 5

Racheal Wangare:Fadhili za Punda

"Rudi, nyumbani mwanamke wewe! Nitakuja jioni tuyamalize haya."

a)(i)Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**

(ii) Fafanua hulka ya msemaji wa kauli hii **(alama4)**

iii) Huku ukizingatia hadithi hii, jadili maudhui ya mabadiliko yanavyojitokeza katika hadithi **(alama7)**

b) Changanua mtindo katika dondoo hili **(alama 5)**

Alasiri ile, baada ya ibada mbili, mhubiri akawa hoi kwa mavune. Akatamani kufika nyumbani apumzike, kazi ya kuwalisha kondoo wa Mungu si kazi rahisi. Wamefika nusu safari, bintiye katulia kama maji ya mtungi. Akimtazama kipembe anamkumbusha marehemu mkewe. Miaka mitatu sasa na dhiki ya kuondokewa haijamwisha. Alihisi ukiwa, akatamani mwenziye. Sasa kazi kukilea kitoto chao, kibinti hiiki kilicho mlanda mamake kama shilingi kwa ya pili. Nyuma ilijaa kicheko alipokua hai mamake. Kama si bintiye ambaye ulimi wake hautulii, kiroho kingemvamia labda hata kumvuta kuelekea kaburini .

AU

5. Winnie Nyaruri Ogenche; Sabina

"Ninaomba wazazi wenzangu muwape watoto wa kike elimu badala ya kuwaoza mapema. Hongera, mwanangu kwa kupata alama mia nne arubaini na saba"

a) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kukuza hadithi husika **(alama5)**

b) Tambua mbinu ya kimtindo iliyotumika katika dondoo hili **(alama1)**

c) Fafanua jinsi mbinu yenyewe ilivyotumika ili kufanikisha utunzi wa hadithi **(alama6)**

d) Fafanua changamoto zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi **(alama8)**

SEHEMU D :USHAIRI

Jibu swali la 6 au la 7

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Nazuka mtunga mambo, na watunzi watungao
Wafungatao masombo, kushika msu na ngao
Naipiga ya ngambo, sauti ifike kwao
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

Ni siku nyingi kitambo, **ninyemele** naja leo
Kama kweli wana nyimbo, nawaje niimbe nao
Na sababu ni vigambo, vya wale wajitwazao
Wawapi wajigambao,tugambiyane vigambo?

Iwapo mu wana nyimbo, na ungoi upasao
Musingewaonya mambo, waoga mwatishao
Mungefungata masombo, kuteta na wawezao
Wawapi wajigamboa, tugambiayane vigambo?

Wawapi fundi wa nyimbo, malengo wajitwazao
Wasemao kula jambo, kuwa walijua wao
Kuna kipambua pambo, chatafuta wapambao
Wawapi wajigambao,tugambiyane vigambo?

Musidhani ni msimbo, hayano nambano leo
Nawaeleza ni mambo, yamtaka atakao
Ajifungate msombo,mdudoateze nayo
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

Imani wenya utambo, mutambao kwa matao
Muelewao mafumbo, na mbinu za wafumbao
Kuna 'tomvu za ulimbo, tengani muruke nao
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

Sasa tafunuwa wimbo, takasani masikio
Siimbi la mtu jambo, alojiweka kituo
Hili' metunga no fumbo, n' nao niwatakao
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

Tamati enyi warembo, nasubiri matokeo
Hivi sasa sina jambo, ela naaga nendao
Ni mimi simba wa wimbo,marara ningurumao
Wawapi wajingambao, tugambiyane vigambo?

Maswali

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka **(alama1)**
b) Eleza muundo wa shairi hili **(alama4)**
c) Taja na utoe mifano ya mbinu nne za kimtindo zilizotumika katika shairi hili **(alama4)**
d) Fafanua uhuru wa kishairi katika ubeti wa nne **(alama3)**
e) Andika ubeti wa pili katika lugha ya nathari **(alama4)**
f) Tambua nafsi nenewa katika shairi hili (alama1)
g) Taja toni la shairi hili **(alama1)**
h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika ushairi **(alama2)**
   i) Wafungatao masombo
   ii) Ninyemele

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki,
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki
Ukweliwe haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo,
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakazifuata nyago,
Hadi kwenye wako ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Pindi kinunua kitu, hafurahi Shaitani, bali tajawa chukizo,
Mtu kiwa mtukutu, tanuna mtimani, kwalo lako tekelezo,
Tamko lake 'Subutu' Kuondoa tumaini, na kukuulia wazo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Aliye na taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai,
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,
Hana faida nyumbani,ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliyejaa uchoyo,
Bahati ina hadaa, kukupa alo sadawi, aibatili rohoyo,
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza kuvunja kaninyo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Ninacho changu kilio, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa matatizo kuambiwa,
Ama nitumie mbio, fuadini ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

MASWALI:

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka **(alama1)**
b) Fafanua mambo **manne** mabayo nafsineni analalamikia **(alama4)**
c) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: **(alama3)**
   (i) Idadi ya vipande katika kila mshororo
   (ii) Mpangilio wa vina katika kila ubeti
(iii) Idadi ya mishororo katika kila ubeti

d) Andika ubeti wa **nne** katika lugha nathari **(alama3)**
e) Bainisha tamathali **mbili** za usemi zilizotumiwa katika shairi hili **(alama2)**
f) Huku ukitoa mifano, onyesha mbinu **mbili** alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi **(alama2)**
g) Andika aina **mbili** za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili **(alama2)**
h) Fafanua muundo wa ubeti wa **tano** na **sita** **(alama3)**

SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI

8 .Niaje wazungu wanaweza kutunza vitu vikajaa kwenye friji. Yani nimeweka soda mbili tu kweye friji lakini akili haitulii hadi nizinywe. Niko sebuleni nazunguka tu. Najaribu kuwaza vitu vingine lakini wapi akili inaniambia 'My friend, kunywa soda.'

a) Bainisha kipera cha utungo huu **(alama1)**
b) Fafanua aina tatu za taswira zilizotumika katika kifungu hiki **(alama3)**
c) Utanzu wa kipera hiki huweza kuchukua nafasi muhimu katika fasihi simulizi. Thibitisha kwa hoja zozote sita **(alama6)**
d) Ufanisi wa uwasilishaji wa utanzu huu unategemea fanani. Teteta kauli hii. **(alama5)**
e) Ni changamoto zipi zinaweza kumkabili mwanafasihi mtafiti nyanjani? **(alama5)**

HII NDIO UKURASA WA MWISHO KUPIGWA CHAPA!

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA KUMI)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1(INSHA)

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

a) *Andika insha* ***mbili****. Insha ya* ***kwanza*** *ni ya* ***lazima***
b) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia*
c) *Kila insha isipungue maneno* ***400***
d) *Kila insha ina alama* ***20***
e) *Kila insha* ***lazima*** *iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
f) *Karatasi hii ina kurasa mbili zilizopigwa chapa.*
g) *Watahiniwa wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	ALAMA
1	
JUMLA	

1. Lazima

Umepata tangazo la nafasi ya kazi ya ualimu katika shule moja maarufu nchini kwenye gazeti la Pambazuko. Andika barua ya kuomba nafasi hii na uiambatanishe na wasifukazi wako.

2. Wanafunzi wa shule za kutwa wanakabiliwa na changamato nyingi katika juhudi zao za kupata elimu wakilinganishwa na wa shule za bweni. Jadili.

3. Tunga kisa chenye kudhihirisha ukweli wa methali; Mchumia juani hulia kivulini.

4. Andika kisa kitakachokamilika kwa maneno haya;

… tulifumukana huku nyuso zetu zikiwa na tabasamu la matumaini ya kuneemeka kwa maisha yetu ya baadaye.

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA KUMI)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2 (LUGHA)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

*a) Jibu maswali **yote** .*
*b) Majibu yote yaandikwe katika **nafasi** ulizoachiwa katika kitabu hiki cha maswali.*
*c) Majibu yote ni **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
*d) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii **zimepigwa chapa** sawasawa na kuwa **maswali yote yamo.***

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

1. UFAHAMU (alama 15)

Swali la usawa wa kijinsia katika jamii ni jambo ambalo limeleta kero kwa wengi katika jamii kwani waja wengi huchukulia kuwa jinsia ya kiume ina uzito sana kuliko ya kike. Wanaume wengi bado wana mawazo yaliyopitwa na wakati. Wao hufikiri kuwa hata wakati Mungu alipomuumba mwanadamu, aliyeumbwa kwanza alikuwa mwanamme kabla ya mwanamke kuumbwa. Kwa sababu hii isiyokuwa na mashiko, wao hujipendelea na kumdharau mwanamke. Wanawake wengine pia wametingwa katika minyororo ya utamaduni kiasi cha kujiona wanyonge na watumwa wa wanaume.

Katika jamii nyingi za kiafrika,mtoto mvulana alichukuliwa kuwa mrithi wa mali ya babake na pia mtu ambaye angesaidia kuendeleza jina la familia au ukoo aliotoka. Kwa sababu hii, ilikuwa ni lazima kwa mke kumpata mtoto mvulana. Wengi waliokuwa hawana bahati ya kuwazaa wavulana walitalikiwa au mume kumwoa mke wa pili. Inaaminika kuwa ni kwa sababu hii ndipo suala la ndoa ya wake wengi liliibuka. Mtoto wa kike alileta huzuni katika jamii kwani hakuchukuliwa kama mojawapo wa wanaukoo wowote na wakati wa kuolewa ukifika, basi aondoka.

Kizazi kipya kinayapa mawazo haya ya kijadi kisogo. Ni yakini kwamba mtoto wa kike ameanza kuonekana kama kiumbe mwenye manufaa mengi. Siku hizi tunawaona wanawake wakiwa na nyadhifa muhimu sana katika jamii, kiasi cha kuwapiku wanaume. Katika shule nyingi na taasisi za juu nchini na ulimwenguni kote, wasichana wamebobea katika masomo na huibuka na alama za kuridhisha katika mitihani. Usawa wa kijinsia kwa hivyo yafaa uonekane katika sekta nyeti ulimwenguni kote.

Hapo jadi, kazi ambayo mwanamke angefanya na iridhishe ilikuwa tu kazi ya ulezi, usafi wa kijamii pamoja na kumfurahisha mwanamume. Hata hivyo, wazo hili limebadilika kwani wanawake wengi wanafanya kazi tofauti tofauti ambazo hata zingine zilizodhaniwa za kiume. Katika mashirika mengi nchini, huwa tunakumbana na wake wakiwa wakurugenzi. Katika nyadhifa nyingi zinazochukuliwa na wanawake, huwa kuna uwajibikaji wa hali ya juu. Si vyema kutenga kazi kwani kujaribu ni kutenda, na kazi yoyote ile yaweza kufanywa na mtu yeyote.

Elimu ndiyo uti wa mgongo wa fanaka maishani na ndio ufunguo wa maisha mema. Majukumu mengi wanayopewa watoto wa kike huwafanya wasihudhurie masomo. Jamii nyingi humpendekeza mtoto wa kiume asomeshwe kuliko wa kike.Wazazi wengi wamejipata wakiangamia kutokana na ugonjwa wa ukimwi, na majukumu ya kuchunga familia huachiwa mwana wa kike. Jambo hili huwafanya kutohudhuria masomo na kupata elimu. Inafaa ifanywe jambo la dharura kuwaelimisha wasichana na wavulana, kwani wote ni sawa na yafaa wajitegemee **aushini**. Ni jambo la kuridhisha kuwaona watoto wa kike pia wakifanikiwa kwa wingi katika masomo. Siku hizi, si nadra kumwona mtoto wa kike amewashinda wengine wa kiume katika masomo, na jambo hili linaonyesha kuwa jamii imezinduka.

Katika taifa letu, imekuwa ikipiganiwa kuwa katika bunge, idadi ya wanaume itoshane na wanawake. Hii inaonyesha kuwa hata wanawake wana uwezo kisiasa, hata ingawa siasa **inasawiriwa** kuwa mchezo mchafu. Katika bunge la sasa kuna wanawake kadhaa, na hata wengine wamefanikiwa kupata nyadhifa za uwaziri. Hii inaonyesha kuwa tofauti na miaka ya nyuma,wanawake pia wamezinduka kisiasa. Hata katika nchi ya Liberia, kwa mara ya kwanza kihistoria, kiongozi mwanamke alipigiwa kura na kuwa rais wa nchi hiyo. Mwanamke huyo aliingia katika vitabu vya

kihistoria kwa kuwa rais wa kwanza kabisa wa kike barani Afrika. Kwa hivyo ni bayana kuwa kisiasa wanawake wana uwezo katika uongozi.

Sheria za kitamaduni za kitambo zilikuwa zinamlinda mtoto wa kiume hadi ukubwani. Waliounda sheria zenyewe walikuwa makundi ya wazee waliowapendelea waume kuliko wake. Hata hivyo sheria hizo zimeonyeshwa kisogo hivi sasa kwani sheria zilizoko sasa ni zinazowalinda waja wote pasi na kuzingatia jinsia. Sheria hizo huwa za kumkabili mkosa wala siye mume au mke. Katika katiba ya nchi ya Kenya, mwanamke amepewa nafasi kubwa na wajibu unaomfaa. Jambo hili linampa motisha sana na kumfanya mwanamke ahisi akiwa mmoja miongoni mwa wanajamii.

Katika kiwango cha kifamilia, yafaa mume na mke washirikiane katika kila jambo. Katika majadiliano yafaa mwanamume amjumuishe mke ili kuwe na usawa katika maafikiano. Hali hii itaepusha migongano na kutoelewana nyumbani. Jamii nzuri yafaa iendeshwe na wazazi wote, na siyo mwanamume au mwanamke pekee.

Kwa kuhitimisha basi, ni vyema kwa jamii kumchukulia mtoto wa kike kama kiumbe anayefaa heshima, elimu, uongozi, na kufanya maamuzi nyeti yanayoweza kuirekebisha jamii. Kasumba na mielekeo ya jadi imepitwa na wakati. Sheria yafaa ifuatwe ili kumlinda mtoto wa kike au mwanamke.

MASWALI.

(a) Ni nini maana ya **jinsia**? **(alama 2)**

(b)Eleza **asili** ya mwanamume kumdharau mwanamke. **(alama 4)**

(c) Toa ushahidi wa kuthibitisha kuwa mwanamke ana **uwezo** sawa na mwanamume. **(alama 4)**

(d) Taja mambo matatu **yaliyodunisha** mwanamke katika jamii. **(alama 3)**

(e) Eleza **maana** ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa . **(alama 2)**

(i) aushini

(ii) inasawiriwa

2. UFUPISHO **(Alama 15)**

<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.</u>

Otieno ni profesa wa Kiswahili. Ilivyo ni kwamba aligundua siri ya mafanikio maishani miaka mingi iliyopita. Anaelewa fika kuwa ikiwa mtu anataka kufaulu maishani lazima ajue kuwa ana amali kubwa sana inayomsubiri. Kulingana naye, mtu hana budi kuikabili vilivyo kazi hiyo husika kwa kutumia mbinu mbalimbali ili kuimarisha aushi yake. Ukimuuliza atakueleza kuwa watu wengi ulimwenguni hustawi baada ya kupitia vizingiti vingi. Kila mtu ana wajibu wa kujitahidi kutenda mazuri kuliko anayoyaona. Kwa mujibu wa Otieno, hakuna mtu anayefaa kutosheka na yaliyotendwa na waliomtangulia. Ikiwa kila mwananchi atakuwa na moyo kama huo nchi yetu itaendelea na kuimarika kwa kasi ya ajabu.

Ili mtu aweze kupiga hatua maishani, anafaa kutenda mambo kadhaa. Itambidi awe na mlahaka mwema na watu wengine kwani kofi hazilii pasi na viganja viwili. Pia, ikiwa ni kijana au mtoto,itamlazimu awe na ushirikiano na wazazi wake ambao watamwelekeza vyema kitabia. Kwa upande wao, wazazi wanafaa kuwaelewa watoto wao na wawape radhi ambayo hukithiri mali.Pana haja ya watoto kujua wanachohitaji na wawe na shabaha maishani mwao. Wanafaa kujikaza kisabuni ili wapate wanachokitaka na wakatae kujihusisha na maovu kama vile wizi. Ikiwa ni wanafunzi, wanastahili kujikakamua masomoni bila kulazimishwa au hata kubembelezwa.

Wanastahili kujua kuwa kulazimishwa na kubembelezwa watekeleze wajibu wao hakuna manufaa yoyote yale. Alipo Otieno, ukimuuliza kuhusu jukumu la watoto la kuhakikisha kuwa maisha ya kesho ni shwari, atakueleza kinagaubaga kuwa mtoto anahitajika kufanya bidii maishani ili kuboresha mustakabali wake; anafaa kujua kuwa asipojifunga kibwebwe kuuboresha mustakabali atapata madhara na atakuwa amechelewa kujaribu kuamsha fikira zake ili kuboresha maisha yake. Kila mtu hasa watoto hawafai kuridhika na kichache wapewacho na wazazi wao ama watu wengine. Hakuna mtu anayefaa kutegemea vitu vya kupewa hata kama ametoka katika jamaa ya wakwasi. Kama ametoka katika jamaa ya matajiri anafaa kujitahidi ili atajirike zaidi. Kwa upande mwingine, ikiwa familia yao ni ya walalahoi, hafai kufa moyo bali anastahili kufanya kazi kwa bidii ili kuboresha maisha yake; aelewe kuwa bidii huweza kumfanya awapiku wakwasi watajika.

Watu wote, hasa vijana wanafaa kujua kuwa nidhamu ndicho chimbuko la mafanikio maishani. Hii ina maana kuwa, vijana wana jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa wąna heshima ya kiwango cha juu. Kila mtu anastahili kujiamini na kuwapuuzilia mbali wanaojaribu kumvunja moyo. Hakuna mtu anayestahili kutamauka maishani licha ya hali ngumu inayomkabili; yafaa ieleleweke fika kuwa baada ya dhiki faraja. Ni dhahiri shahiri kuwa aghalabu fanaka hutokana na jitihada; bahati ni chudi. Kwa upande wao, wanafunzi hawana sababu yoyote ile ya kuwabeza walimu au wenzao, wajue kuwa mafanikio yao masomoni hutegemea washikadau hawa muhimu. Itawabidi vijana wakubali kukosolewa na kuomba msamaha wa makosa yao. Isitoshe, kila binadamu hafai kuthamini vitu vya anasa kama mavazi ya bei ghali ikiwa hana uwezo wa kuvipata. Wanafaa kuwa wavumilivu kwa kuwa subira huvuta heri na siku moja watapata kila watakacho kulingana na bidii yao. Kulingana na Profesa Otieno, penye nia pana njia na muhimu ni kutokufa moyo.

Maswali

1. Fupisha aya ya kwanza kwa maneno 40 **.** **(alama 5, mtiririko 1)**

Matayarisho

Jibu

2. Bila kupotosha ujumbe uliokusudiwa na mwandishi, fupisha aya mbili za mwisho . (maneno 95-100 ; alama 10, mtiririko 1)

Matayarisho , Jibu

3) MATUMIZI YA LUGHA **(Alama 40)**

(a) Taja **sauti** zilizo na sifa zifuatazo**:** **(Alama 2)**

(i) sauti ya wastani na nyuma ya ulimi. ……..

(ii) kikwamizo cha ufizi ……..

(iii) hutamkiwa koromeo ……

(iv) hutamkwa ncha ya ulimi inapojipigapiga haraka kwenye ufizi …….

(b) Andika **wingi** wa sentensi **:** **(Alama 2)**

Tajiri aliweka pesa zake kwenye sefu.

(c) Ainisha **viambish**i katika neno: **(Alama 3)**

Aliyemlisha

(d) Andika sentensi moja katika **wakati uliopita hali timilifu.** (A**lama 2)**

(e) Jaza mapengo kwa **vihisishi** mwafaka **(Alama 2)**

(i)……..…… hivyo ni sawa.

(ii) …… mlango u wazi.

(f) Tambulisha aina ya **vitenzi** vilivyotumika katika sentensi hizi. (**Alama 2)**

(i) Kazi hii ni nzuri.

(ii) Gari letu lilikuwa linataka kuuzwa.

(g) Andika katika **udogo,** hali ya **wingi**. **(Alama 2)**

Mvulana huyu mdogo ameangushwa na kigari kile.

(h) Dhihirisha matumizi ya **na**: **(Alama 2)**

Kem alitaka kuwa na pesa za kubadilishana nao.

(i)Tofautisha matumizi ya **po** ya wakati katika sentensi hizi. **(Alama 2)**

(i)Alipomwona alimhoji.

(ii)Amwonapo humhoji.

(j) Bainisha matumizi ya kiambishi **ku.** **(Alama 2)**

Amani atakutengenezea mpini wa jembe kisha aelekee kule kwao.

(k) Tumia vihusishi kudhihirisha hali zifuatazo: (**Alama2)**

(i) kiwango

(ii) wakati

(l) Ainisha **virai** katika sentensi: **(Alama 2)**

Wiki ijayo watavuna mahindi.

(m) Tumia vitenzi vya **silabi moja** kutunga sentensi katika kauli zilizoandikwa: **(Alama 2)**

(i) wa (kauli ya kutendwa)

(ii) nya (kauli ya kutendea)

(n) Ainisha **yambwa** katika sentensi: **(Alama 3)**

Watoto walimjengea mama yao nyumba kwa matofali.

(o) Eleza **maana** mbili zinazopatikana katika sentensi: **(Alama 2)**

Mwalimu alimwambia mwanafunzi kuwa hawataenda nyumbani.

(p) Changanua sentensi ifuatayo kwa **matawi**: **(Alama 4)**

Yohana ameingia ndani ya chumba hicho.

(q) Eleza matumizi yoyote mawili ya alama ya **mkato** katika sarufi ya Kiswahili. **(Alama 2)**

(r) Tumia **visawe** vya maneno yaliyopigiwa mstari kuandika tena sentensi ifuatayo. **(Alama 1)**

<u>Shamba</u> hili limelimwa na msichana aliyepewa <u>zawadi</u> jana.

(s) Andika **methali** moja inayotokana na maelezo yafuatayo**:** **(Alama 1)**

Tabia ya kuchelewachelewa kutenda mambo humletea mtu umaskini kwani yeye hukosa nafasi zote muhimu.

4) <u>ISIMU JAMII</u>

(a) Eleza kwa ufupi jinsi mambo yafuatayo yanavyodhibiti mitindo ya lugha:

(i) mada **(Alama 2)**

(ii) hali ya mtu**.** **(Alama 3)**

(b) Fafanua sifa zozote tano za sajili ya **shuleni**. **(Alama 5)**

Huu ndio ukurasa wa mwisho uliopigwa chapa.

KCSE 2026 TOP SCHOOLS' MOCKS

(JARIBIO LA KUMI)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3 (FASIHI)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
c) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
d) *Swali la* ***kwanza*** *ni la lazima.*
e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu* ***nne*** *zilizobaki yaani: Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.*
f) *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja.***
g) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
I	20	
	20	
	20	
	20	
JUMLA		

SEHEMU A: USHAIRI

1. LAZIMA

T. Arege: Wimbo wa Kichaa

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Bustani za jadi
Maua ya kuchezea vipepeo
Na pua kufurahisha
Sasa ni mabaki ya kumbukumbu
Za yaliyojiri hapa
Na kukiacha Kijiji kinywa wazi.

Hapa walimpiga mwereka
Dada yangu; mdogo wangu
Shuleni akitoka
Na mkoba wa kilo nzito za vitabu
Chini akakandamiziwa
Wakachana mbuga na wake ubikira!

Pale kando ya mto
Walimvizia na kumburura shangazi
Binamu zangu wadogo wakiona
Marinda wakamchania
Kabla ya kumtia kidonda shangazi
Naye ami kumchania kovu moyoni!

Ni hapa kando ya barabara kuu
Ambapo nyanyangu walimshika mkono
Uchochoroni wakamburuta
Na kumfanya kujutia
Bahati mbaya ya kuishi kwingi
Akaganda uchochoroni
Hadi alipoletwa nyumbani kesho yake
Na wachungaji wa muchungani.

Si hapa walipomshurutisha mama
Chini wakamkanyagia
Kama kuku wa kuchinja
Baada ya yake sidiria kuikata?
Si hapa sebuleni mwetu?
Si hapa sokoni

Nilipopata vazi la stara
La wangu mke mpendwa
Lilikatwa yake mihimili?

Yule kichaa wa mwetu sokoni.
Akawa kichwani amelivaa
Na kuimba wimbo wa maombolezi
Huku wanakijiji wakimpuuza
Na watoto kumcheka?

Ni hapa ambapo usiku ulipoingia
Hawakusita kuhakikisha kuwa
Yule kichaa amewazalia mtoto
Na kujitia kundini kushangaa
Kilichomtuma atake kujifungua!

Maswali

(a) Tambulisha **nafsineni** katika shairi hili**.** **(alama 2)**
(b) Eleza **dhamira** ya mshairi. **(alama 2)**
(c) Fafanua mbinu za **kimtindo** zinazojitokeza katika shairi hili. **(alama 5)**
(d) Eleza aina za **taswira** zinazojitokeza katika shairi hili. **(alama 4)**
(e) Bainisha **toni** ya mshairi. **(alama 2)**
(f) Onyesha matumizi ya **mishata** katika shairi hili. **(alama 1)**
(g) Fafanua **muundo** wa shairi hili. **(alama 4)**

SEHEMU B: RIWAYA

SHEMU YA C:Riwaya ya Nguu za Jadi-Prof Clara Momanyi

Jibu swali la 2 au la 3

2.Soma dondoo kisha ujibu maswali yanayofuta ;

Watategemewa na nani maishani? Hiki ndicho kizazi cha kesho au kizazi kilichopotea tayari?

a)Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama 4)**

b)Tambua toni katika mazungumzo haya. **(alama 2)**

c)Onyesha ni vipi kizazi cha leo na cha kesho kilivyopotea. **(alama 12)**

AU

3.Fafanua ufaafu wa anwani ya ,'Nguu za Jadi'. **(alama 20)**

SEHEMU C: TAMTHILIA

T.M. Arege: Bembea ya Maisha**;**Jibu swali la 4 au la 5

4 a) Changanua **mtindo** katika kifungu kifuatacho (alama 10)

‘‘Mwanangu usitake sana kuhoji alacho kuku. Utachafukwa roho umchukie kuku bure. Wala usitake kujua nyuki ameitengenezea nini asali. Hutaila. Maadamu yameshakuja,yapokee. Mtoto akinyea kiganja hakikatwi wala hatuulizi kwa nini. Ni maumbile. Maumbile hayo,sawa na vidole, hayafanani. Sawa na watoto wachezeao bembea, tumeicheza na tungali tunaicheza sehemu yetu kwa zamu. Haidhuru iwe ya kamba au chuma. Muhimu ni kwamba tumeshirikiana kusukumana kwenye bembea ya maisha. Upo wakati inakuwa raha tele na upo wakati inakatika na kutubwaga. Hiyo ndiyo raha hasa ya maisha. Ni sawa na chombo kinachomenyana na mawimbi katika bahari. Hutufanya kuwa macho katika safari…”

b) Fafanua namna <u>mandhari</u> ya dondoo hili yalivyochangia usukaji wa tamthilia. **(alama 10)**

5. ‘‘Walishasema baada ya dhiki ni faraja, Faraja ni zao la dhiki. Leo hii kikapu cha mama kimejaa ndago.”

a) Eleza **muktadha** wa dondoo hili. **(alama 4)**
b) Eleza vipengele **viwili** vya kimtindo kwenye dondoo**.** **(alama 4)**
c) Eleza maudhui **mawili** yanayodokezwa kwenye dondoo. **(alama 2)**
d) Eleza **sifa** za msemaji**.** **(alama 5)**
e) Kwa kutolea mifano mwafaka eleza dhiki alizopitia mama ambaye sasa kikapu chake kimejaa ndago**.** **(alama 5)**

SEHEMU D: HADITHI FUPI

D.W Lutomia na P. Muthama (Wah): *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

Jibu Swali la 6 au La 7

6. *R.Wangari*: Fadhila za punda

Anwani ‘Fadhila za Punda’ inaafiki hadithi hii” Thibitisha. **(alama 20)**

7. *W.N Ogeche*: Sabina

a) Changanua mtindo katika dondoo lifuatalo; **(alama 6)**

‘Athari ya mawazo yake ilijiandika dhahiri shahiri usoni mwake. Alianza kwa kuachia tabasamu pana mithili ya msafiri aliyefika salama. Baada ya dakika chache machozi yalianza kumtoka njia mbilimbili huku kajishika tama. Alifikiria kuhusu mtihani uliodhamiriwa kuanza siku ya Jumanne. Mtihani ambao ungemwezesha kupata ufadhili katika shule ya upili ya bweni ikiwa angepita vyema. Hili ndilo wazo lililozua tabasamu. Lakini, angefeli je?Hatima yake ingekuwa ipi? Maswali haya yalimliza yakamwacha akisinasina kama mgonjwa wa mafua. Akiwa katika hali hii, aliyakumbuka maneno ya mwalimu mkuu, ‘‘mizizi ya elimu ni michungu ila matunda yake ni matamu. Ikiwa mnataka kuyaonja matunda ya elimu, lazima mtie bidii kwani mtaka cha mvunguni sharti ainame.”

b) Bainisha mbinu **mbili** zinazoweza kutumiwa kutambua sifa za mhusika Sabina kwa kurejelea hadithi *Sabina*. **(alama 2)**

c) Taja na ueleze aina **mbili** za taswira zinazojitokeza kwenye dondoo hili. **(alama 2)**

d) Kwa kutolea mifano mwafaka eleza matatizo yanayomkumba mwanamke katika hadithi *Sabina*. **(alama 10)**

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8(a) Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.

Kila kukicha mashaka
Ni kero hili si huba
Mimi pendo la viraka, heri demu la mkoba
Mimi mno nataka, kuishi nawe muhiba
Pendo viraka viraka
Litanishinda kuziba
Kamwe sitoshughulika
Nawaje wenye kuziba
Viumbe wanosifika, kwa fedha, chuma na shaba
Walostarabika, si mimi wa tobatoba
Pendo viraka viraka
Litanishinda kuziba

Naapa sitojitweka
Limenichosha si haba
Nasomba vyangu viraka, nitie kwenye mkoba
Sikuye ya kuzinduka, mjinga hawi ni juba
Pendo viraka viraka
Litanishinda kuziba

i.Huu ni wimbo wa mapenzi. Thibitisha**.** **(alama 2)**

ii.Eleza sifa **mbili** za nafsi nenewa katika wimbo huu. (**alama 2)**

iii.Fafanua mbinu **tatu** ambazo nafsineni ametumia kufanikisha uwasilishaji wake. (**alama3)**

iv.Eleza faida **nne** za kurithisha wimbo huu kwa vizazi vijavyo. **(alama 4)**

(b)Unanuia kufanya utafiti kuhusu utungo wa maigizo :-

(i) Eleza hatua **tatu** utakazofuata katika utafiti wa utungo huu. (**alama 3)**

(ii) Unanuia kutumia **hojaji** kutafitia utungo huu. Eleza **umuhimu** na **udhaifu** wa kutumia njia hii**.** **(alama 6)**

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA

Kupata nakala za majibu, Tafathali wasiliana na;

0746 222 000

0753 222 000

mwalimuconsultancy@gmail.com

kcsepredictions@gmail.com

Hii ni hati miliki ya Mwalimu Consultancy Litmited

Inayoendeshwa na Bw. Isaboke

MAFANIKIO!